# Nipashe

Jumatatu Februari 10, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580150

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US





UKURASA 13



## Mwekezaji mbaroni tuhuma za kuzalisha bangi, kusafirisha nje

UKURASA 4

# Nyanya, vitunguu havishikiki sokoni

• **Walaji**, wauzaji waeleza kilio, wataalamu wa uchumi, kilimo wafafanua... *Endelea ukurasa 2*



Mmoja wa wafanyabiashara Georgina Gabriel kutoka Soko kuu la Shinyanga Mjini, akiuza nyanya na vitunguu katika soko hilo.
**PICHA: MARCO MADUHU**

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

**WAKURUGENZI WAZEMBE MAPATO KUANIKWA JUNI**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo...

UKURASA WA 4

**WAZIRI AAGIZA MAFAO KWA WAKATI PSSSF**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na wenye...

## Nzige wadaiwa kukaribia K'njaro

UKURASA 2

# Familia ilivyouawa usiku wa manane kwa moto kikatili

• **Ni** watu sita waliokufa baada ya nyumba kuchomwa moto wakiwa wamelala.... *Endelea kurasa 2*




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


MICHEZO **JULIO AIONYA SIMBA KUMTIMUA SVEN** UK.31 **MAONI, KATUNI** UK.6

## Nzige wadaiwa kukaribia K'njaro

**Na Mwandishi Wetu**

WILAYA ya Mwanga mkoani Kilimanjaro, imetoa tahadhari kwa wananchi wanaoishi maeneo ya mipakani kuwapo uwezekano wa tishio la nzige.

Taarifa iliyosambaa kwenye mitandao ya kijamii iliyothibitishwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mwanga, Zefrin Lubuva, zilieleza kuwa wadudu hao wako umbali wa kilomita 50.

"Tumepokea taarifa toka mkoani kwamba nzige wapo kilomita 50 toka mpaka wa Tanzania na Kenya. Tunaomba kuwatangazia wananchi kuwa pindi watakapoona makundi makubwa ya wadudu jamii ya panzi kwenye maeneo yao watoe taarifa mapema ili kupeleka taarifa kwenye mamlaka zinazohusika," ilisema taarifa ya Ofisa Kilimo wa Wilaya, Erick Kaaya.

Akizungumza na Nipashe, Lubuva alisema mamlaka sahihi zimeshapatiwa taarifa naa zinafuatilia kwa karibu na kwamba taarifa hiyo imesambazwa kwa viongozi wa vijiji na kata kwa ajili ya kupeleka kwa wananchi.

"Dawa zipo lakini siyo kwa kiasi kikubwa na ndiyo maana tumepeleka taarifa kwa mamlaka za juu ili kupata msaada, pia tunawasiliana na wilaya za jirani pamoja na wananchi ili tushirikiane," alisema.

Vile vile, alisema nchini Kenya suala hilo likuwa la kitaifa na limeendelea kushughulikiwa kitaifa, na kwamba wilaya hiyo imewasiliana na wizara husika kwa ajili ya hatua zaidi.

Akizungumza na Nipashe, Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alisema walipokea taarifa kutoka wilayani humo na kwamba timu ya wataalamu imejipanga vyema kukabiliana na wadudu hao.

"Ndege za kupuliza dawa zipo tayari, tumeandaa watu, dawa na wananchi, tukisikia tu wamekaribia eneo letu tutaanza kupuliza. Tumetuma wataalam wa kutosha kwenye mipaka yetu," alisema.

Hivi karibuni, Waziri Hasunga alisema viuatilifu maalum vya kudhibiti nzige jumla lita 7,000 na wataalamu wapo kwenye mipaka ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga na Mara.

Nzige walianzia nchini Ethiopia wakasambaa kuelekea Somalia baadaye waliingia Kenya na kuathiri zaidi ya majimbo matano na hatua mbalimbali zilichukuliwa.

# Nyanya, vitunguu havishikiki sokoni

**Na Waandishi Wetu**

BEI ya nyanya na vitunguu kwenye masoko mengi nchini imeendelea kupaa kwa takribani wiki tatu na kufikia sado moja kuuzwa kati ya Sh. 10,000 hadi Sh. 15,000.

Wanunuzi wa reja reja wamejikuta wakinunua nyanya moja kati ya Sh. 500 hadi Sh. 700 na zilizokaribia kuharibika maarufu kama masalo zinauzwa kati ya Sh. 400 hadi Sh. 500, kwa moja.

Kwa kawaida msimu wa nyanya bei yake kwa sado moja huuzwa kati ya Sh. 3,500 hadi Sh. 5,000.

Masoko mbalimbali yaliyofuatiliwa nchini, yamebainika kuuza tenga moja la nyanya kati ya Sh. 100,000 hadi Sh. 150,000, na kilo moja ikiuzwa kati ya Sh. 6,000 hadi Sh. 7,000 huku bei za awali zilikuwa Sh. 35,000 hadi Sh. 45,000.

Kwa upande wa vitunguu gunia moja linauzwa kati ya Sh. 450,000 hadi Sh. 500,000, na sado moja kuuzwa kati ya Sh. 10,000 hadi Sh. 16,000 huku kilo moja ikiuzwa kati ya Sh. 3,500 hadi Sh. 7,000.

Sanduku moja la nyanya linakadiriwa kuingia madebe matatu na debe moja linaingia sado tatu, kutegemea na ukubwa wa nyanya.

Gazeti hili ambalo lilifanya ufuatiliaji wa bei za bidhaa hizo kupanda kwa kasi, limeelezwa sababu ya kupanda kwa gharama ni mvua inayonyesha maeneo mbalimbali nchini na kusababisha mafuriko, uharibifu wa miundombinu na mazao hayo, huku mazao hayo yakioza kwa kushindwa kufika sokoni kutokana na miundombinu mibovu.

Hali hiyo imewaweka wafanyabiashara katika wakati ngumu kiasi cha kutafuta viungo mbadala vya kupikia baada ya kushindwa kumudu bei.

MCHUMI

Mtaalamu wa Uchumi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, Profesa Honest Ngowi, akizungumza na Nipashe alisema ongezeko la bei linatokana na kutofautiana kati ya ugavi na utashi sokoni (demand and supply).

Alisema kupanda kwa bei maana yake zipo chache sokoni kuliko mahitaji na kwamba huenda sababu kubwa ni mvua zilizonyesha maeneo mengi nchini.

"Bei kubwa hivi kwenye bidhaa zinazotumiwa na watu wengi itaongeza mfumuko wa bei, na sitashangaa ripoti ya mfumuko wa bei ya mwezi huu ambayo data zake zitapatikana Machi mwaka huu, zitaonyesha zimepanda," alisema.

"Kwa sasa tuko kwenye sarufi moja ya mfumuko wa bei. Upande wa ugavi wa uchumi wametuangusha," alisema.

Kwa mujibu wa Profesa Ngowi, upo uwezekano mkubwa kuwa mvua inayoonyesha maeneo mengi nchini imesababisha mafuriko na uharibifu wa miundombinu kiasi cha wakulima

INAENDELEA UK. 8



Mkurugenzi wa Huduma wa Rotary Club ya Mbezi Beach, Monalisa Sykes, akikabidhi jozi ya viatu kwa mwanafunzi wa Shule ya Msingi Mbezi Beach, Shabani Mgosi, wakati wa hafla ya kukabidhi viatu, vyandarua na zawadi mbalimbali kwa wanafunzi 230 wa shule hiyo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Mkurugenzi wa Club hiyo, Stella Urio, Rais Mtangulizi wa Rotary Club ya Oysterbay, Vikash Shah na mzazi wa mwanafunzi, Amina Shabani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Familia ilivyouawa kwa moto kikatili

**Na Futuna Seleman,** KIBITI

WATU sita, wawili wakiwa ni mama na watoto wamefariki dunia baada ya nyumba waliyokuwa wamelala kuchomwa moto usiku wa manane.

Tukio hilo lilitokea katika kitongoji cha Uponda Kata ya Mjawa wilayani Kibiti mkoani Pwani.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Rufiji, Onesmo Lyanga, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kwamba hadi sasa mtu mmoja anashikiliwa kwa madai ya kuhusika na tukio hilo.

Alimtaja anayeshikiliwa Richard Mathias, mkazi wa Buza jijini Dar es Salaam na Masasi mkoani Mtwara.

Akifafanua kuhusu tukio hilo, Kamanda Lyanga alisema uchunguzi wa awali unaonyesha kuwa chanzo ni wivu wa kimapenzi kati yake na mpenzi wake, Regina Mavondo ambaye kwa sasa ni marehemu.

Alisema Mathias alikwenda nyumbani kwa mpenzi wake Regina usiku wa manane Februari 8, mwaka huu na kudaiwa kuwa alichoma nyumba hiyo, ambayo ndani kulikuwa na watu watano wamelala wakiwamo watoto wawili wa Regina.

Waliofariki ni Mavondo (31), Agnes Taimu (26), Regina Elias (19) ambao walimuita Mavondo mama mdogo.

Wengine ni Frida Francis (22) aliyekwenda kuomba kazi kama kibarua kuuza pombe kwa marehemu Mavondo (mwenye nyumba) na mtoto wa Frida aitwaye Nuru Seleman (4) aliyekumbwa na mauti akiwa amelala na mama yake kwenye nyumba hiyo.

Mwingine ni mtoto aliyetambulika kwa jina moja la Maimuna (3) ambaye ni mtoto wa Agnes Taimu ambaye anamuita mama mdogo marehemu Regina.

"Miili imefanyiwa uchunguzi na daktari aliyefika eneo la tukio na kubainika imeungua vibaya, na kuamuriwa izikwe palepale," alisema Kamanda Lyanga.

Kwa mujibu wa kamanda huyo, eneo la tukio walikuta dumu la lita kumi la mafuta ya petroli linalodhaniwa kuwa lilitumika kuteketeza nyumba hiyo.

Alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa katika kijiji cha Njopeka akiekea jijini Dar es Salaam na kwamba wakati wowote atafikishwa mahakamani.

## HABARI KITAIFA



Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Biashara Tanzania (TNBC), Dk. Godwill Wanga (kushoto), akizungumza kwenye kikao cha kikundi kazi cha misitu kilichoandaliwa na baraza hilo. Katikati ni Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Prof. Adolf Mkenda na kulia ni mwenyekiti mwenza kutoka sekta binafsi, Ben Lusus. Habari Uk. 10. **PICHA: MPIGAPUCHA WETU**

# Wawili wafariki dunia ajali ya magari kuwaka moto

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

WATU wawili wamefariki dunia na mwingine mmoja kujeruhiwa baada ya magari waliyokuwa wakisafiria kugongana uso kwa uso na kuwaka moto eneo la Kidai, barabara kuu ya Morogoro-Iringa.

Ajali nyingine imetokea barabara kuu ya Morogoro-Dodoma katika eneo la Makunganya, na kuhusisha basi la kampuni ya Shukrani likitokea Dodoma kuelekea jijini Dar es Salaam lililowaka moto na kuteketea huku abiria 42 waliokuwamo ndani ya basi hilo wakinusurika.

Taarifa zilizothibitishwa na Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Mugabo Wekwe, zimesema ajali iliyotokea jana, majira ya saa nne asubuhi, eneo la Kidai imehusisha lori lililokuwa limebeba kopa, lenye namba T 644 DNR likikokota tela namba T 574 DMW aina ya Fong mali ya kampuni ya Inara, likitokea Zambia kuelekea Dar es Salaam, likiendeshwa na Amir Kasongo Mkazi wa Dar es Salaam.

Alisema lori hilo liligongana uso kwa uso na gari dogo IT namba 8584 ikiendeshwa na Daniel Kombo mkazi wa Dar es Salaam akitokea jijini humo kwenda Tunduma.

INAENDELEA UK. 8

# Tanzania yaomba kupunguziwa mzigo wakimbizi

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA imeutaka Umoja wa Afrika na Jumuiya za Kimataifa kuongeza jitihada na nguvu katika kuleta amani katika maeneo yenye migogoro barani Afrika hususani nchi za Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) ili kuipunguzia Tanzania mzigo wa wakimbizi uliouebeba kwa muda mrefu.

Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, ametoa kauli hiyo katika siku ya kwanza ya Mkutano wa 33 wa kawaida wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika unaofanyika, Addis Ababa nchini Ethiopia.

Alisema kuwa kaulimbiu ya mkutano wa mwaka huu ya kunyamazisha silaha (silencing the gun) imekuja wakati muafaka kwa kuwa mapigano na kutokuwapo utulivu katika baadhi ya nchi za Afrika zinachelewesha maendeleo katika bara hilo.

Alisema endapo Umoja wa Afrika na Jumuiya za Kimataifa zitaongeza nguvu katika kunyamazisha silaha na kukawapo amani na utengamano, ni dhahiri viongozi wataelekeza nguvu kubwa katika maendeleo endelevu ya wananchi na hivyo kupunguza umaskini katika Bara la Afrika ambalo linaonekana kama lililoghubikwa na migogoro na mapigano.

Samia aliuahidi Umoja wa Afrika kuwa Tanzania itatekeleza kwa kasi mpango wa umoja huo katika mapambano dhidi ya malaria na kwamba Tanzania imedhamiria kuutokomeza kabisa ugonjwa huo ifikapo mwaka 2030.

Katika mkutano huo wakuu wa nchi na serikali wa Umoja wa Afrika wameshuhudia mabadilishano ya uenyekiti kwa Mwenyekiti anayemaliza muda wake Abdel Fattah el-Sisiambae pia ni Rais wa Misri, amekabidhi Uenyekiti kwa Rais wa Jamhuri ya Afrika ya Kusini Cyrill Ramaphosa, ambaye anakuwa Mwenyekiti mpya wa Umoja wa Afrika.

# Udhibiti njia za panya waleta tija

**Na Asraji Mvungi,** ARUSHA

UDHIBITI wa njia za panya zilizokuwa zinatumika kuvusha bidhaa za magendo na raslimali kama madini na mifugo umeanza kuleta tija katika mkoa wa Arusha.

Akitoa taarifa kwa viongozi wa ngazi mbalimbali za kitaifa wakati wa maadhimisho ya miaka 43 ya CCM, Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, ametaja moja ya tija iliyoanza kupatikana kuwa ni mapato katika halmashauri zilizoko pembezoni ikiwamo ya Longido kuongezeka.

Alisema katika wilaya hiyo awbayo ilikuwa haipati hata shilingi kwenye biashara ya mifugo, kwa sasa imekusanya zaidi ya shilingi bilioni moja katika kipindi cha miezi mitatu na yameendelea kuongezeka mafanikio yanayohusishwa na kufunguliwa kwa masoko ya ndani ya mifugo.

"Pamoja na kuimarisha udhibiti wa utoroshaji wa rasilimali hii kwenye mipaka, pia hatua ya kufungua masoko ya ndani imekuwa na tija kubwa kwa kuwa kwa sasa wananchi wanapata maeneo ya kuuzia bidhaa zao kwa uhakika na serikali nayo inapata kodi, na mafanikio haya pia yamejitokeza kwenye sekta ya madini," alisema Gambo. Akizungumzia mafanikio kwa upande wa madini Mbunge wa Simanjiro, James Miliya, alisema pia ujenzi wa ukuta kwenye machimbo ya madini ya Mirerani umeongeza tija kubwa hasa kwenye madini ya Tanzanite suala ambalo pia limeendeelea kuwanufaisha vijana wa jamii za wafugaji.

Akizungumzia mafanikio hayo Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa anayeshughulikia Siasa, Uhusiano na Mambo ya Nje, Ngemela Lubinga, alisema hatua hiyo inaonyesha kuwa Watanzania wanaanza kuelewa umuhimu wa rasilimali zao na kuzitumia kwa manufaa ya nchi.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA

USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II
(S.M.M. 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)
Katika Mahakama ya mwanzo MJINI -TANGA

Usimamizi wa Mirathi NAMBA 14/2020

Ombi la KHALID HILAL HAMAD kuteuliwa Msimamizi wa mirathi marehemu AMINA ABUSHIRI SULTAN

Kwa YEYOTE ANAYEHUSIKA

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 26/2/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 05/02/2020

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
TANGA MJINI

215622702



KUPOTEA KWA KADI YA GARI & LAPTOP

**EVARIST THADEO KAPINGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA HILUXSURF** yenye namba za usajili **T 391 CWN.** Chassis **No.KZN1309034769,** Engine **No.IKZ0089184. LAPTOP** aina ya hp.yeyote atakae viona atoe taarifa kituo cha polisi.Taarifa ya polisi **DOM/RB/1050/2020.**

215622802



C&G CAR and GENERAL

KUPOTEA KWA RISITI

CAR and GENERAL Company tunatangaza kupotelewa na Risiti mbili katika ofisi zetu za Arusha.

Risiti hizo zina namba zifuatazo:
**Risiti Na. 0018950** na
**Risiti Na. 0018700.** Ukiziona toa taarifa kituo cha Polisi kilicho karibu au wasiliana nasi kwa

+255685711002/ +255715699889

215622302

# Wakurugenzi wazembe mapato kuanikwa Juni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amesema ifikapo Juni mwaka huu, ataweka hadharani majina ya wakurugenzi wa halmashauri waliofanya uzembe kwenye ukusanyaji mapato kama itampendeza Rais.

Jafo alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa akitoa taarifa ya ukusanyaji wa mapato ya ndani ya halmashauri kwa kipindi cha nusu mwaka (Julai-Desemba 2019) kwa mwaka wa fedha 2019/20.

Alieleza kuwa kabla ya kuweka wazi atawasilisha majina yao kwa mamlaka ya uteuzi ili ifanye maamuzi.

Aidha, alisema wakurugenzi waliokusanya chini ya kiwango wanapaswa kujitathmini kwa muda uliobaki hadi mwisho wa mwaka wa fedha 2019/20 mwezi Juni mwaka huu.

"Hawa wote ninao wasema ni waliokusanya chini ya asilimia 25 kama ndani ya miezi sita kutoka Julai hadi Desemba halmashauri imeshindwa kukusanya hata asilimia 25 wewe ofisa umepewa halmashauri utaiendesha vipi," alisema.

"Si wakurugenzi pekee bali hata kwa watunza fedha itakapofika mwezi wa sita kwa wakurugenzi tutapendekeza kwa mamlaka ya uteuzi."

Alisema kwa upande wa Wakuu wa Idara ya Fedha kwenye Halmashauri, atawachukulia hatua yeye (Jafo) kwa kuwa lipo chini yake."

"Itakapofika Juni mwaka huu nitakapotoa ripoti ya miezi sita ya kwanza naomba kila mtu ajitathmini sasa tumeingia quarter ya tatu ambayo itaishia Aprili na baadaye tutakuwa na quarter ya nne itakayoishia mwezi Juni 30."

Jafo alisisitiza: "Sitarajii mkurugenzi yeyote au halmashauri yeyote kama haina sababu yoyote ya msingi na ikashindwa kufikia kiwango cha makusanyo."

Alikemea watu wanaochezea mashine za kukusanyia mapato za POS, huku itakapobainika mkurugenzi wa halmashauri husika na mweka hazina wake watachukuliwa hatua.

"Hatutarajii kusikia kuna wizi wa fedha unaendelea, lakini bado kuna tabia ya watu kula fedha mbichi, wanakusanya fedha haziingi hata benki na fedha zinaingia mikononi mwa watu huo ni wizi wa fedha mbichi," alionya.

Waziri Jafo alisema kwa mwaka huo halmashauri zilipanga kukusanya Sh. bilioni 765.48

INAENDELEA UK. 8



Naibu Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, akiwa amebeba ndoo ya maji, baada ya kuzindua mradi wa maji utakaonufaisha wakazi zaidi ya 7,500 katika kijiji cha Makang'wa Jimbo la Mtera mkoani Dodoma juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Waziri aagiza wastaafu PSSSF kulipwa kwa wakati

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, ameliagiza Baraza la Wafanyakazi la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi Umma (PSSSF), kuweka mfumo mzuri wa kulipa kwa wakati mafao ya wastaafu.

Aliyasema hayo jana, jijini Arusha wakati akizindua baraza hilo.

Mhagama alisema amekuwa akipokea malalamiko kutoka kwa baadhi ya wastaafu ya kutokulipwa kwa wakati mafao yao.

Hata hivyo, aliwataka wafanyakazi kutimiza wajibu wao ili kuuwezesha mfuko huo kusonga katika kutekeleza adha ya serikali ya kutoa huduma bora kwa wananchi.

"Kilio kikubwa cha wastaafu ni kulipwa mafao yao kwa wakati, na serikali itahakikisha kilio cha wastaafu kinakwisha kwa kulipa mafao hayo mapema," alisema Mhagama.

Pia aliliagiza baraza hilo, kufungua ofisi za PSSSF, kwenye wilaya zote kwa kuwa wastaafu wengi wamekuwa wakipata shida kufika mikoani kufuatilia taarifa za mafao yao.

"Naomba PSSSF mfungue ofisi kwenye wilaya zote kwa kuwa wastaafu wetu wanaoishi vijijini wamekuwa wakipata shida ya kufika kwenye ofisi za mikoa kufuatilia taarifa za mafao yao," alisema Mhagama.

"Niwaombe wafanyakazi mtambue kuwa hakuna haki bila ya kutekeleza wajibu wenu, hivyo nendeni mkatoe huduma bora kwa jamii, kwa kuwa nimekuwa nikipokea malalamiko mengi ofisini kwangu kuhusu utoaji wa huduma zisizoridhisha na majibu mepesi kwa wateja," aliongeza.

Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF ambaye ni Mwenyekitiki wa Baraza la Wafanyakazi, Hosea Kashimba, alisema baraza hilo, lina wajumbe 59 na wawakilishi wa wafanyakazi na wakurugenzi kutoka kanda zote nchini.

# Mwekezaji mbaroni madai kuzalisha bangi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAKATI baadhi ya wabunge wakipigia chapuo kuruhusiwa kuanza kwa uzalishaji wa kilimo cha bangi ili kuchakata mafuta yake kwa ajili ya matibabu, Mamlaka ya Kupambana na Kuzuia Dawa za Kulevya nchini (DCEA), imemkamata mwekezaji wa kigeni raia wa Poland, Damian Sankowski (40), aliyeanza kazi hiyo ya kuzalisha bangi na kuuza katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

Baada ya kukamatwa, mwekezaji huyo anadaiwa alijaribu kuwashawishi maofisa waliokuwa katika kikosi kazi hicho kupokea Sh. milioni 10 ili mambo yaishe na kuahidi kuwalipa kila baada ya mwezi mmoja Sh. milioni 40.

Sankowsiki aliingia nchini kwa ajili ya kuwekeza katika ujenzi wa hoteli za kitalii, karibu na uso wa Mlima Kilimanjaro, eneo la Njiapanda ya Himo, Wilaya ya Moshi.

Jana Kaimu Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kupambana na Kuzuia Dawa za Kulevya nchini, James Kaji, alithibitisha kukamatwa kwa mwekezaji huyo na rafiki zake watatu akiwamo mkewe.

Mwekezaji huyo anadaiwa kuingiza nchini aina mpya ya mbegu ya bangi kutoka nchini Hispania na kuileta mkoani Kilimanjaro, ambako amekuwa akiivuna katika eneo maalum lililozungushwa uzio mrefu wa tofali na kuichakata kwa kutengeneza malighafi mfano wa 'asali na jam' ambayo huuzwa zaidi katika masoko ya nje, kupitia mipaka ya Pangani na Zanzibar.

"Huyu amekuja kama mwekezaji, sasa baada ya kumkamata kuna dawa nyingine ambayo tumeikamata nyumbani kwake ambayo iko processed (imeshasindikwa), imetengenezwa kama 'Jam' nyingine kama asali ya Australia na iko well packed (imefungashwa vizuri) na amekuwa akiuza sehemu mbalimbali ndani ya nchi na nje ya nchi.

"Tulipata taarifa kwa wananchi wema kwamba kuna mwekezaji mmoja raia wa Poland anayefahamika kwa jina moja la Damian amekuwa akiendesha kilimo, yeye amekuja kwa mwavuli kwamba anafungua kituo cha watoto yatima pia baadaye angejenga hoteli kutokana na kuwa kwenye uso wa karibu na Mlima Kilimanjaro."

Alisema baada ya wao kupata taarifa za kiintelijensia, maofisa wa mamlaka hiyo ya dawa za kulevya waliondoka jana jijini Dar es Salaam na kwenda Kilimanjaro ambako walifanikiwa kuliweka katika uangalizi na kulikamata eneo hilo pamoja na mtuhumiwa.

"Mtuhumiwa alipatikana nyumbani kwake, baada ya upekuzi zilipatikana dawa nyingine ambazo baada ya kupelekwa kwa Mkemia Mkuu wa Serikali pamoja na ku

INAENDELEA UK. 8

TANGAZO

absa

Habari

Leo Barclays Bank Tanzania Limited imebadilika rasmi kuwa
**Absa Bank Tanzania Limited.**

Karibu katika benki inayokusaidia
**kukamilisha malengo yako.**

**absa.co.tz**

Absa Bank Tanzania Limited (yenye usajili namba 38557) inaongozwa na kanuni za Benki Kuu ya Tanzania.

215621602

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Waamuzi wameianika TPLB, mtendaji mpya sasa isafishe

**HABARI** ya mjini katika soka la Tanzania Bara kwa sasa ni kuvurunda kwa waamuzi husuan wanaochezesha Ligi Kuu na Ligi Daraja la Kwanza.

Ni zaidi ya wiki tatu sasa kelele za kuvurunda kwa waamuzi zimetawala kila kona nchini jambo ambalo liliiamsha serikali na kulitaka Baraza la Michezo la Taifa (BMT) kuketi na Shirikisho la Soka nchini (TFF) kutafuta ufumbuzi.

Matukio yanayolalamikiwa zaidi na wadau wa soka ni waamuzi kutochezesha kwa haki ama kwa madai ya kuchukua rushwa au kushindwa kuzitafsiri vema sheria 17 za soka husuan sheria ya kuotea (offside).

Hali hiyo, imechangia baadhi ya timu kupoteza mechi zao za ligi hiyo, na kuzua malalamiko makubwa kutoka kwa viongozi wa klabu, wachezaji, makocha hadi kwa mashabiki na wadau wa soka.

Awali, suala hilo lilionekana kama lipo kwa ajili ya kuwabeba mabingwa watetezi na vinara wa ligi hiyo, Simba pekee kabla ya kubainika pia kwa Yanga, Azam FC na hatimaye kwa kubainika ni kwa klabu zote za Ligi Kuu na uozo huo pia kubobea Ligi Daraja la Kwanza.

Nipashe ambalo limekuwa likifuatilia kwa makini kila mchezo wa Ligi Kuu na ile ya Ligi Daraja la Kwanza, lilishaeleza udhaifu mkubwa wa kutofuatwa kwa sheria 17 za soka kabla hata ya wimbi hilo nzito kutanda.

Hata hivyo, kilio hicho kilisikika baada ya kelele nyingi na kumuibua waziri mwenye dhamana na michezo nchini, Dk. Harrison Mwakyembe, ambaye alipeleka moto BMT, huku Rais wa TFF, Wallace Karia naye akiwahi kwa kuitaka TPLB kuchukua hatua.

Kwa ujumla TPLB ikionekana kulala na kusahau wajibu wake wa kuhakikisha inatatua kero zote katika ligi hizo mbili za juu nchini, hadi ilipokurupushwa baada ya mambo kuharibika.

TPLB ilikurupushwa na kisha kuketi na kuwachukulia hatua baadhi ya waamuzi akiwamo mwamuzi namba mbili, Kassim Safisha wa mechi kati ya Simba na Namungo FC ambaye alifungiwa kwa kipindi cha miaka mitatu.

Hata hivyo, wadau wa soka wameielezea adhabu, hiyo kama ya kimhemuko zaidi kufuatia kuwa kubwa ikilinganishwa na aina la kosa ambalo ni la kushindwa tu kutafsiri vema sheria ya kuotea na kulikubali bao la mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere.

Kadhalika, adhabu hiyo iliwaibua baadhi ya waamuzi ambao hawakuficha kilio chao cha kutolipwa stahiki zao kwa muda mrefu pamoja na kufichua madudu makubwa katika upangwaji wa kuchezesha mechi hizo.


Ingawa ni mengi waliyoeleza, lakini hilo la kutolipwa posho zao na kulimbikiza hadi baadhi kueleza wapo wanaodai kuanzia Sh. milioni moja hadi kumi, linatufikirisha zaidi hasa tukizingatia waamuzi hawana mishahara.

Ingawa awali kabla ya TPLB kukaa na kuchukua hatua hiyo, Rais Karia kupitia radio moja nchini aliulizwa kuhusu uwapo wa tetesi za waamuzi kudai kutolipwa kwa wakati akageuka mbogo, lakini hili linapaswa kutazamwa kwa jicho la tatu husuan wakati huu ambao TFF imemtangaza Mtendaji Mkuu mpya wa TPLB, Almas Kasongo.

Kwa mtazamo wetu, hatutaki kuamini kwamba waamuzi wote wanahongwa ili kukanyaga sheria 17 za soka, bali tunaamini wapo wanaoshindwa kuzitafsiri vema na wengine pia wakiingia uwanjani huku wakiwa na mawazo ya kimaisha kutokana na hali ngumu ya kutolipwa posho zao.

Hivyo, si wakati tu wakuwaadhibu kwa kuwapa vifungo virefu, bali Mtendaji Mkuu wa TPLB, Kasongo aanze kwa kumulika malipo yao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Ratiba Ligi Kuu maumivu kwa wachezaji

Na Adam Fungamwango

**MECHI** ya 'dabi' ya Mwanza kati ya Alliance dhidi ya Mbao iliisha kwa sare ya bao 1-1 Jumamosi, huku wachezaji wa timu hizo mbili wakiwa hoi.

Si kwa sababu ya mechi hiyo tu peke yake, bali pia kwa safari ndefu ya kutoka Mtwara, timu zote mbili zikiwa zimefika Mwanza na kucheza bila kupumzika.

Aliance ilifika mchana wa siku ya kuamkia mechi, lakini wenzao Mbao waliwasili Mwanza usiku na kesho yake kujitupa dimbani kucheza dhidi ya wenzao.

Wachezaji wa timu zote mbili hawakupata muda wa kupumzika, kwani Alliance Februari Mosi ilikuwa kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona mjini Mtwara kupambana na Ndanda FC na baada ya mechi hiyo, ikaanza safari ya kilometa nyingi kwa basi dogo kuwahi mechi dhidi ya Mbao FC. Februari 4, mwaka huu, Mbao FC nayo pia ikawa kwenye uwanja huo huo wa Nangwanda Sijaona kucheza dhidi ya Ndanda, na baada ya mechi ikageuza kwa basi kuiwahi mechi dhidi ya Alliance iliyopigwa kwenye Uwanja wa Nyamagana Mwanza.

Makocha na viongozi wa timu zote mbili baada ya mechi walilalamikia uchovu wa wachezaji wao kuwa hawakupumzika, wala kuweka miili yao sawa na badala yake wamefika tu na kukutana na mechi, huku wakiwa wametoka umbali mrefu, wachezaji wakiwa wamejikunyata garini. Huu ni mfano wa mechi nyingi ambazo zinachezwa baada ya siku mbili au tatu, huku timu zikisafiri umbali mrefu na kusababisha hata mechi zenyewe zisichezwe kwenye kiwango halisi kinavyotakiwa.

Cha kujiuliza hata wasafiri wa kawaida tu wanapotoka kwenda mikoa ya mbali wanapofika wanakuwa wamechoka kwa safari na kuhitaji kupumzika, vipi iwe kwa wachezaji ambao wao wanafika tu na wanatakiwa kucheza?

Kuna watakaosema kuwa mbona Ligi za Ulaya wanacheza mfululizo, timu inacheza Jumanne Ligi ya Mabingwa na Jumamosi inacheza Ligi Kuu, lakini ikumbukwe kwa wenzetu wana miundombinu mizuri, lakini wana uwezo mkubwa kipesa, kiasi cha kuweza kusafiri kwa ndege ili kutowachosha wachezaji wao.

Inatakiwa wachezaji wa Tanzania wacheze mechi nyingi, lakini si zikiwa karibu karibu, huku baadhi ya timu zikiwa zinatoka mbali kwa kusafiri umbali mrefu kwenda kucheza na timu nyingine.

Ndiyo maana kuna baadhi walipendekeza mechi ya Alliance na Mbao basi ingechezwa Nangwanda Sijaona huko huko kwa sababu zote zilikuwa huko, lakini navyojua hii haipo kwenye kanuni ya ligi.

Najua tatizo kubwa hapa ni kwamba Shirikisho la Soka nchini (TFF) na Bodi ya Ligi Tanzania (TPLB) wanakimbizana na muda wa fainali za Kombe la CHAN zitakazoanza Aprili 4 hadi 25, mwaka huu nchini Cameroon, lakini inawaumiza mno wachezaji kwani ni hawa hawa ambao wanakimbizwa mchakamchaka huu, baadhi yao watakiwa kuingia kambini kwa ajili ya michuano hiyo, hivi kweli wanaweza kwenda kucheza kwa viwango vyao kweli huko CHAN?

Halafu hapo hapo watakiwa kurejea tena bila kupumzika, mwezi Mei waendelee kumalizia mechi za Ligi Kuu, hapa naona wachezaji hawatendewi haki. Wanafanywa kama matrekta ambayo ni chuma na yanatumia mafuta, wakati wao ni binadamu wanatumia damu na nguvu za miili yao, wakati wanahitaji pia kupumzika ili miili irejeshe nguvu.

Sitaki kuwaingilia sana TPLB kwenye ratiba zao, lakini ukweli utabaki pale pale kuwa kwa ratiba hii jinsi ilivyo inachosha sana na kuwaumiza wachezaji na kuwafanya wasicheze kwenye viwango vya kawaida.

# BARUA MJADALA

## Tujitahadhari uchafu wa vyakula

**Mhariri,**

*NI kwa kiasi gani vyakula vinaboreshwa katika maeneo yetu? Lazima nikiri, kuwapo vyombo vya ubora wa bidhaa nchini vinavyofanya kazi zao, ikiwamo iliyokuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TBS).*

*Kwa sasa, TBS imefanyiwa mabadiliko kuwa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), jukumu la 'chakula' limehamishiwa katika Shirika la Viwango la Taifa (TBS) kuendeleza jukumu la maboresho kitaifa.*

*Hapo sijaenda mbali kushuhudia kinachofanywa na tume inayosimamia ushindani sawa. Shida kuu imebaki katika namna gani hayo yanafanikishwa.*

*Kwa ujumla, mambo yanayotawala katika maisha yetu kwa jumla ni chakula. Ni vipi tumelimudu hilo? Tunapopita kila mahali kuna maduka ya vyakula yanayotawala sehemu kubwa ya mitaa yetu na yako katika kila aina ya maisha.*

*Pili hiyo imo katika huduma za mlo wa moja kwa moja, iwe mama ntilie, migahawa au hoteli. Simulizi kuu kote ni vyakula.*

*Hapo ndipo nami ninaingiza swali langu, kwamba pamoja na kuwapo nyenzo zote hizo za kutuhakikishia mlo safi, tunaboreshaje huo mlo katika nafasi zetu binafsi?*

*Tukianzia katika maandalizi, mathalani kuoka mkate kwa namna mbalimbali na bidhaa zingine za ngano zinazoandaliwa kwa jumla, ni vipi zinafanyika katika usafi? Hiyo inaweza kwenda mbali katika vyakula vya migahawa na hotelini, hata hatua ya mazingira ya mlo?*

*Majumbani kunajulikana jamii kutofautiana sana kati ya eneo moja na lingine, familia moja na nyingine ambako kukidodoswa kwa kina, uchafu haukosekani na anayewajibika na maboresho ni mkazi mwenyewe.*

**Agustino Fandilo,**
**Dar es Salaam.**

## WASILIANA NASI:

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Waamuzi wamechanganywa, sasa wamechanganyikiwa jumla




**Na Adam Fungamwango**

KWA siku za karibuni kumekuwa na kelele kubwa juu ya waamuzi kuchezesha chini ya kiwango kwenye baadhi ya mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kelele zimekuwa nyingi kwa wachambuzi wa soka, katika mitandao ya kijamii na mashabiki wa soka kwa ujumla.

Kelele na mihemko, ikasababisha hata serikali kupitia Wizara ya Habari Utamaduni, Sanaa na Michezo kuliagiza Baraza la Michezo la Taifa (BMT) kuingilia kati kwa kulitaka kukaa na Shirikisho la Soka nchini (TFF) kuangalia nini kimetokea.

TFF nayo ikakaa na Bodi ya Ligi kuangalia nini kinasababisha malalamiko mengi, ikiwamo mihemko ya mashabiki wa soka ambao wamekuwa wakipiga kelele uchezeshaji mbovu wa baadhi ya waamuzi.

Ndipo tukaona moja ya adhabu kali kabisa kuwahi kutokea kwenye miaka ya hivi karibuni, wakati mwamuzi namba mbili Kassim Safisha akifungiwa kutochezesha soka kwa miaka mitatu kwa kushindwa kutafsiri sheria ya kuotea kwenye mechi kati ya Simba dhidi ya Namungo FC.

Kwa sababu ya mihemko ya mashabiki, Kamati ya Uendeshaji wa Ligi nayo inatumia mihemko hiyo hiyo kumfungia mwamuzi huyo. Kama walidhania kuwa ndiyo dawa ya waamuzi kutofanya makosa walikosea, kwani baada ya hapo hali ndiyo ikazidi kuwa mbaya.

Karibuni mechi zote zilizochezeshwa baada ya hapo zikaripotiwa kuwa na madudu matupu zikiwamo za Simba dhidi ya JKT Tanzania ambapo bao halali la Gerson Fraga lilikataliwa kwa madai kuwa mchezaji huyo aliotea wakati haikuwa hivyo, mechi ya Yanga dhidi ya Lipuli, mwamuzi msaidizi kuamuru kona mpira uliodakwa na kipa wa Yanga Metacha Mnata ambao ulionekana kana kwamba umeshaingia golini, lakini kwa upande mwingine kipa huyo alikuwa ameubananisha kwenye nguzo.

Kwenye Uwanja wa Mabatini Mlandizi mkoani Pwani, Mtibwa Sugar nayo ililalamikia bao la wenyeji wao Ruvu Shooting kwamba halikuwa halali.

Hii inayotokea sasa ni kama waamuzi na wasaidizi wamechanganyikiwa na kushindwa kufanya maamuzi sahihi. Hawajiamini. Wamekuwa wakikataa mabao ya dhahiri kwa kuhisi kuwa kama ikiangaliwa kwenye marudio na kukuta haikuwa hivyo basi wataadhibiwa. Matokeo yake wamekuwa wakiharibu kabisa.

Ni kwa sababu tumeruhusu kelele na mihemko ya mashabiki, badala ya kuliachia soka lifanye kazi yake.

Waamuzi walipaswa waadhibiwe kutokana na kanuni zilizowekwa na si kwa sababu ya kelele za watu.

Leo kafungiwa Safisha, kesho atafungiwa aliyesema kona, keshokutwa aliyekubali bao la Ruvu Shooting, mwishowe watafungiwa wote.

Kwa mawazo yangu ni kwamba duniani hakuna mwamuzi yeyote atakayeweza kuchezesha mechi akafanya maamuzi sahihi kwa asilimia 100 kama vile malaika.

Hata Ulaya haiwezekani ndiyo maana wameleta mashine za Teknolojia ya Video ya Kumsaidia Mwamuzi (VAR). Tumeshuhudia waamuzi wakikubali mabao, halafu baadaye VAR inakataa. Au wanakataa VAR inakubali. Majuzi tumeshuhudia mechi ya Tottenham dhidi ya Machester City, mwamuzi akikataa penalti, lakini baada ya dakika kadhaa VAR ikaamuru kuwa ilikuwa ni penalti halali. Halafu ile iliyoonekana kama ni penalti, VAR ikakataa. Sasa waamuzi wale kama ni huku basi wangefungiwa baada ya watu kuangalia marudio ya kwenye TV, kwa sababu walichokuwa wakiamua sicho.

Kwenye mchezo wa soka, waamuzi hukosea, mastraika hukosa mabao ya wazi, mabeki hujifunga, makipa ufanya uzembe unaogharimu timu, lakini pia hata makocha hufanya mabadiliko ambayo wakati mwingine yanakuwa hayana tija na timu inafungwa.

Haya yote ni makosa ya kwenye soka ambayo yanaitwa ni ya kibinadamu, lakini kwa sasa inaonekana kama vile waamuzi hawatakiwi kabisa kukosea kitu chochote kile, kitu ambacho si kweli.

Inavyoonekana ni mihemko tu ya mashabiki wa klabu zenye wapenzi wengi nchini Simba na Yanga ndiyo wanaosababisha yote haya kwa msaada wa wachambuzi wa masuala ya michezo ambao wamekuwa mara nyingi zaidi wakiangalia makosa machache ya waamuzi na kuwahukumu.

Hakuna anayewatetea waamuzi ambao wanachezesha vibaya, lakini adhabu iangaliwe zaidi kwa waamuzi ambao wanaonekana kabisa kushindwa kumudu mchezo kabisa, kwa kuionea timu wazi wazi au kushindwa kuchukua hatua kwa matukio yanayoonekana wazi yametendeka, lakini si kosa moja au mawili ndiyo ionekane ameshindwa kumudu, watakuwa ni kama wanaonewa kwa sababu hata kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya wanakuwa waamuzi watano, lakini bado kuna makosa machache yanatokea ya kibinadamu.

Serikali na TFF watambue kuwa haiwezi kuridhisha watu wote kwani hata hiyo VAR kwenye Ligi Kuu ya England ambayo ni kompyuta tu, lakini bado inalalamikiwa na mashabiki na wapo wanaoenda mbali zaidi na kudai kuwa eti VAR inaipendelea zaidi Liverpool.

Kusema kweli pamoja na matatizo waliyokuwa nayo, lakini kwa sasa tutashuhudia maamuzi ya ajabu zaidi kwa sababu waamuzi wameshachanganyikiwa na kama kweli wahusika wanataka kusiwe na makosa, basi ni wakati wa serikali na TFF kugharamia uwapo wa VAR kuwasaidia waamuzi kuanzia msimu ujao.

Lakini kwa sasa wakati waamuzi wetu ni kama vile hawajui wanalolifanya, TFF iongee na Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), kuleta waamuzi kutoka Zanzibar ili kuchezesha baadhi ya mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Sidhani kama kutakuwa na kikwazo cha kanuni kwa sababu Bara na Zanzibar yote ni nchi moja na hata miaka ya nyuma kulikuwa na waamuzi kama Hafidh Ally, Juma David na wengineo kutoka Zanzibar waliokuwa wakichezea mechi za Ligi Kuu na walifanya vizuri kwenye ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati.

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed



# Nyanya, vitunguu havishikiki sokoni

INATOKA UK. 2

kushindwa kuyafikia masoko au mazao kuzidiwa na mvua.

**MTAALAMU AELEZA**

Mtaalamu wa kilimo, Profesa Andew Tembu, alisema haitakiwi kushangaa kupanda kwa bei ya mazao ya aina hiyo.

Alisema mabadiliko ya bei hutegemea msimu kwa kuwa kwenye vitabu vya maelezo ya bei kuna nadharia mbalimbali inazonyesha kwamba lazima bei ya zao hilo zitaongezeka na kupungua.

"Mazao hayo yanafanya vyema kwenye msimu wa ukame, ndiyo maana zinapandwa maeneo kama Kilolo, Kilosa na Mbeya ambako wanalima mpunga, yale maji yanayobakia ndiyo wanalima nyanya au vitunguu na msimu wa mvua wakati watu wanapanda mahindi na mazao mengine hayastawi," alibainisha.

Kwa mujibu wa Profesa Temu, msimu wa mvua upandaji wa mazao hayo ni mdogo na mwisho wa msimu au katikati huwa kuna ongezeko la bei kwa kuwa hakuna bidhaa sokoni.

Alisema nchi zilizoendelea nyanya na vitunguu zinazotumika ni zile zilizoongezewa thamani na mtumiaji kutumia kwa bei ile ile isiyoumiza.

Vile vile, alisema cha kujiuliza ni namna ya kupata ufumbuzi wa kilimo hicho ili kiweze kustahimili wakati wote.

"Kama tunataka kweli kusaidia tunapaswa kutumia teknolojia za 'Screen houses' (nyumba za kisasa za kilimo) ambazo unaweza kukadiria kiasi cha maji na kudhibiti magonjwa, hatuna kilimo cha ina hii kwa kiasi kikubwa," alisema.

"Mahitaji ya nyanya wastani wa tani 600,000 hadi milioni moja kwa mwaka, siyo rahisi kuzitengeneza kwa kutumia nyumba za kisasa, ila inapaswa kusindika kwa kuwa kiasi cha nyanya kinachoharibika ni kikubwa, tutumie njia za kuziweka nzima kwenye vifungashio na kuhifadhi kwa dawa zinazokubaliwa na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ili ziwezwe kutumiwa kwa nyakati zote," alisema Profesa Temu.

**HALI SOKONI**

Nipashe ilifanya ufuatiliaji katika masoko mbalimbali nchini na kujionea hali halisi ya bei ya bidhaa hizo, huku wengine wakitafuta namna ya kuendelea kupata mlo wa siku bila kutumia nyanya za shambani.

**DAR ES SALAAM**

Jijini Dar es Salaam, bidhaa hizo zimekuwa adimu na zinauzwa kwa bei ya juu kwenye masoko yote.

INAENDELEA UK. 26



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Butata, Kata ya Bukima, Musoma Vijijini mkoani Mara, wakimwagilia maji matofali juzi, ambayo yameandaliwa kwa ajili ya ujenzi wa madarasa mapya ili kukabili uhaba wa vyumba vya madarasa unaoikabili shule hiyo. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Mwekezaji mbaroni madai kuzalisha bangi

INATOKA UK. 4

chukua specimen (aina ya mmea) ikagundulika ni zao la bangi. Kwa mujibu wa Kamishna Jenerali Kaji, kuna baadhi ya wateja wa dawa hiyo inayozalishwa na mwekezaji Sankowsiki, wanakuja kutoka Ulaya, si kwamba ni kwa ajili ya dawa, ila ni matumizi ya kilevi.

**WAWILI WATOROKA**

Alisema wakati wa ukamataji wa eneo hilo na mwekezaji wake, wafanyakazi wawili waliokuwa wanahudumia shamba hilo walitoroka.

"Imetushangaza kidogo kwamba mamlaka za hapa hazifahamu jambo hili, lakini amekuwa ni mtu wa rushwa, tangu walipokuja kukamata alitoa ahadi ya kutoa milioni 10 na alizileta pale ili mambo yaishe; na akatoa ahadi kwamba watakapokubaliana wachukue contact (mawasiliano) yake kwamba kila baada ya mwezi mmoja atakuwa anatoa milioni 40.

Alisema Kaimu Kamishna Jenerali Kaji: "Sasa mwone ni jinsi gani wanavyotuhadaa kwa sababu watakuja kwa nia nzuri na maneno mazuri, mifano mingi tu tuna wawekezaji kwenye madini."

**AZUNGUMZIA WABUNGE**

Baada ya Februari 3, mwaka huu, baadhi ya wabunge kutaka bangi iruhusiwe kuzalishwa nchini ili kuchakata mafuta ya bangi, Kaimu Kamishna Jenerali Kaji ameeleza:

"Katika jamii hivi sasa kuna malumbano makubwa ya kutaka kuruhusu kilimo cha bangi kwamba tunalima kwa ajili ya dawa, lakini nitoe angalizo tu kwamba ni vyema na tunajitahidi sisi kutoa elimu ili wananchi waweze kuelewa. Lakini kutokana na tatizo hili ambao sisi kama mamlaka inatupa ugumu kwa kipindi hiki kukubaliana na hicho kitu ni kwa sababu bado tunaendelea kuzuia na kupambana kudhibiti kilimo ambacho si halali."

## Wawili wafariki dunia ajali ya magari kuwaka moto

INATOKA UK. 3

Alisema, baada ya ajali, magari yote mawili yaliwaka moto na kusababisha vifo kwa madereva wote wawili na majeruhi kwa abiria wa lori, Neema Dick Malasusa (37) mkazi wa Songwe aliyekuwa kwenye lori.

Katika eneo la Makunganya katika barabara kuu ya Morogoro-Dodoma, mwandishi wa habari hizi alifika na kushuhudia jitihada za kuzima moto kwenye basi la Shukrani, lenye namba za usajili T 414 ASG aina ya Scania, likitokea Dodoma kuelekea jijini Dar es Salaam, zikiendelea kufanywa na gari ya kubeba maji ya kuwasha inayotumiwa na Askari wa Kikosi cha Kutuliza Ghasia, FFU, wakati huo gari ya zimamoto ikiwa inaondoka kwenda kufuata maji mengine huku kwenye buti la gari zikionekana mboga za majani aina ya chinese zikiwa zimeungua na baadhi ya mizigo ikiwa nje ya basi.

Dereva wa basi hilo Hashibu Issa, (50), alisema alisikia mlio wa tairi kupasuka na kulazimika kusimamisha gari, na baadaye kushuhudia moto ukianza kuwaka eneo lilipopasuka tairi na kuanza kuokoa abiria na mali zao na hakuna mali iliyoteketea, wala kifo au majeruhi.

Wekwe aliyekuwa eneo la ajali, alikiri ajali hiyo kutokea, majira ya saa 5.40 asubuhi eneo la kwa Makunganya na hakuna kifo wala majeruhi na kwamba chanzo cha ajali hiyo ni kupasuka kwa tairi ya ndani ya kulia mwa basi, na wamezima moto na kusogeza basi hilo barabarani ili magari na watumiaji wengine wa barabara waweze kuendelea kuitumia barabara hiyo.

Baadhi ya abiria waliokutwa eneo la Makunganya ilipotokea ajali, Tumaini Hezron na Neema Shadrack, kwa nyakati tofauti walidai kusikia mlio wa kupasuka tairi upande wa kulia mwa basi na dereva alisimamisha gari na kondakta kuwataka washuke na ghafla walianza kusikia harufu ya moshi na kuona moto ukianza kutoka katika tairi iliyokuwa imepasuka hivyo kuhamisha haraka mizigo yao.

# Wakurugenzi wazembe mapato kuanikwa mwezi Juni

INATOKA UK. 4

kutoka kwenye vyanzo vyake vya ndani na hadi kufikia Desemba mwaka jana zimekusanya Sh. bilioni 356.81 ambayo ni asilimia 47 ya makisio ya mwaka.

Alisema uchambuzi umeonyesha kwa kipindi hicho halmashauri 63 kati ya halmashauri 185 zimekusanya mapato ya ndani kwa asilimia 50 na zaidi ya makisio na halmashauri 122 zimekusanya chini ya asilimia 50 ya makisio ya mwaka.

Kwa upande wa mikoa, Waziri Jafo alisema Mkoa wa Geita unaongoza kiasilimia, ambapo umekusanya wastani wa asilimia 63 huku wa mwisho ni Tanga ambao umekusanya wastani wa asilimia 36 ya makisio ya mwaka ya halmashauri za mkoa huo.

Aidha, alisema kwa kigezo cha wingi wa mapato, Mkoa wa Dar es Salaam umekusanya Sh. bilioni 83.86, huku mkoa wa mwisho ni Katavi ambao umekusanya Sh. bilioni 4.68.

Jafo alisema Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imeongoza kundi la majiji kwa kukusanya mapato kwa asilimia 71 ya makisio yake ya mwaka. Huku Halmashauri ya Jiji la Dodoma imekuwa ya mwisho kwa kukusanya asilimia 41.

Kwa upande wa Halmashauri ya Manispaa, alisema Manispaa ya Ilemela imeongoza kwa asilimia 75 huku Manispaa ya Kigoma imekuwa ya mwisho ambapo imekusanya kwa asilimia 26.

Pia, alisema Halmashauri ya Mji wa Njombe imeongoza kwa kukusanya kwa asilimia 88, huku Babati ikiwa ya mwisho kwa kukusanya asilimia 30.

Alisema Halmashauri za Wilaya za Tunduru na Kibondo zimekusanya mapato kwa asilimia 104 kwa kipindi hicho na Halmashauri za Wilaya za Mafia, Ukerewe na Gairo zimekusanya asilimia 18 tu ya makisio yake kwa muda huo.

Kuhusu kigezo cha wingi wa mapato, alisema Halmashauri ya Jiji la Dodoma imekusanya mapato mengi zaidi kuliko halmashauri zote kwa kukusanya Sh. bilioni 29.75, huku Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imekuwa ya mwisho kwa kukusanya Sh.bilioni 6.03.

Kwa upande wa Halmashauri za Manispaa ya Ilala imeongoza kwa kukusanya Sh.bilioni 29.13 huku Kigoma ikiwa ya mwisho kwa kukusanya Sh. milioni 694.93.

"Halmashauri ya Mji wa Geita imeongoza kwa wingi wa mapato kwa kukusanya Sh. bilioni 4.64 na Halmashauri ya Mji wa Nanyamba imekuwa ya mwisho katika kundi hili kwa kukusanya Sh. milioni 459.44," alisema.

Alibainisha Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze imeongoza kwa kukusanya Sh. bilioni 3.89 huku Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli imekuwa ya mwisho kwa kukusanya Sh. milioni 186.08.

HABARI KITAIFA

# Mhagama aagiza wilaya, mikoa mazingira biashara

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Vijana, Wanawake na Watu wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, amezielekeza halmashauri za wilaya na ofisi za mkoa kutekeleza maazimio yanatokana na mikutano ya majadiliano kati ya sekta binafsi na sekta ya umma kati ngazi zao ili kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini.

Waziri Mhagama aliyasema hayo katika ziara ya kukagua miradi ya maendeleo iliyofadhiliwa na Ubalozi wa Denmark kupitia Mradi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (LIC) kwa uratibu wa Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) ambao umelenga kuwakwamua kiuchumi wananchi wa Mkoa wa Dodoma.

"Lazima tuhakikishe maazimio yaliyofikiwa katika mikutano ya majadiliano katika ngazi ya Mkoa au Wilaya yanafanyiwa kazi ili kuboresha mazingira ya biashara nchini hali itakayoonyesha tija ya uwepo wa mikutano hii," alisema.

Alisema TNBC linafanya kazi nzuri ya kuhakikisha mabaraza ya wilaya na mikoa inafanyika na kuhakikisha maamuzi yanayofikiwa katika ngazi hizo na yale yanayohitaji utatuzi kwa ngazi ya taifa yanafikishwa kwenye mkutano wa Baraza la Taifa ambalo mwenyekiti wake ni Rais John Magufuli.

Aliongezea kuwa kumekuwa na malalamiko mengi kuwa watendaji wa halmashauri kuwa hawaketelezi majukumu yao ikiwa ni pamoja na kutotenga muda wa kushiriki katika mikutano ambayo inafanyika katika maeneo yao.

"Sote tunafahamu kauli mbiu ya serikali ni kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo mwaka 2025, hivyo kupitia mikutano hii inayokutanisha sekta binafsi na sekta ya umma inasaidia kuibua changamoto na kupatiwa ufumbuzi na utekelezaji utasaidia kuboresha mazingira ya biashara," alisema. Waziri Mhagama alisisitiza kuwa uwapo wa majadiliano ya mara kwa mara kati ya sekta binafsi na sekta ya umma yatasaidia kujadili changamoto na kutatuliwa katika ngazi ya wilaya au mkoa hali itakayosaidia kupunguza majadiliano marefu katika mkutano wa Baraza la Taifa.

Katibu Mtendaji wa TNBC, Dk. Godwill Wanga, alisema baraza lake limejipanga kushirikiana na ofisi za mikoa na wilaya kuhakikisha mabaraza katika ngazi hizo yanafanyika kwa kufuata ratiba zitakazoandaliwa. "Tunaandaa kalenda ya mwaka ya mikutano ya majadiliano kwa ngazi ya wilaya, mkoa na ule wa taifa ili kuwe na ufuatiliaji wa urahisi kwa mabaraza haya kufanyika kwa wakati," alisema Dk. Wanga.

Aliongezea kuwa lengo ni kuhakikisha unapofanyika mkutano wa Baraza la Taifa basi yatajwe mafanikio ambayo yatatokana na kuwapo kwa majadiliano katika ngazi ya wilaya na mkoani ambapo changamoto zote zimetatuliwa huko.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama (kushoto), akisindikizwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Hosea Kashimba, baada ya kuzindua Baraza la Wafanyakazi la Mfuko huo jijini Arusha mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Walimu wafunguka chanzo wanafunzi kufeli

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

WAKUU wa shule za sekondari Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, wamebainisha sababu za wanafunzi wilayani humo kufeli mitihani yao ya kitaifa ya kidato cha nne.

Sababu hizo zimetajwa kuwa ni utoro sugu kwa wanafunzi, umbali mrefu wa shule, upungufu vyumba vya madarasa, viti, meza na ukosefu wa walimu hasa masomo ya sayansi.

Walibainisha hayo juzi kwenye kikao cha tathmini cha matokeo ya mitihani ya kitaifa ya kidato cha pili na nne, kilichoitishwa na idara ya elimu ya halmashauri hiyo ya Wilaya ya Shinyanga, kwa lengo la kujadili changamoto na kuzitatua zinazosababisha wanafunzi kufanya vibaya kwenye mitihani ya taifa hasa kidato cha nne.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Lyabukande, Ernest Stephen, alisema wanafunzi kwenye halmashauri hiyo hawataweza kufanya vizuri mitihani yao, ambapo wengine wanasoma wakiwa wamekaa kwenye matofari, hakuna walimu wa kutosha, wanatoka umbari mrefu na kusababisha utoro sugu.

Naye Ofisa Elimu wa Shule za Sekondari Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Stewat Makali, alikiri kuwapo na tatizo la upungufu wa walimu 159, wa masomo ya biashara nane, Kiingereza 46, na Sayansi 105, ambapo vyumba vya madarasa upungufu 23, viti 5,625, meza 5,761, na maabara 61.

Aidha, alitaja matokeo ya kidato cha nne, kuwa mwaka (2018) walishika nafasi ya 41 kati ya halmashauri 175 nchi nzima, ambapo mwaka (2019) wameshuka na kushika nafasi ya 83 kati ya halmashauri 195, na kuwataka walimu wajitahidi kufundisha wakati changamoto zao zikiangaliwa namna ya kutatuliwa.

Mdhibiti ubora wa shule katika halmashauri hiyo, Beatus Manumbu, alisema licha ya wakuu wa shule kubainisha changamoto hizo pia ni wazembe kusimamia taaluma, ambapo baadhi ya walimu wanafundisha kimazoea.

00000

## Shirika lapiga jeki shule vifaa maabara

**Na Julieth Mkireri**

SHULE ya Msingi Kawawa katika kata ya Mabibo Manispaa ya Ubungo, jijini Dar es Salaam, imepatiwa vifaa vya maabara kutoka Shirika la Leap Learning, ambao utuwezesha mwanafunzi kuhitimu elimu ya msingi akiwa anajua kusoma, kuandika na kuhesabu.

Mradi huo umefadhiliwa na Shirika la Leap Learning kwa kushirikiana na Shirika la Ocode linalojishughulisha na mambo ya kijamii ikiwamo elimu.

Akizungumza katika hafla ya makabidhiano ya maabara hiyo iliyofanyika mwishoni mwa wiki, mwalimu mkuu wa shule hiyo Aron Athanas, alisema, mradi huo utakuwa mkombozi kwa watoto wenye uelewa wa taratibu darasani katika hatua ya kusoma, kuandika na kuhesabu.

Athanas alisema katika shule yake ambayo ina wanafunzi 2,800, kati yao 100 wanakadiriwa kuwa hawajui kusoma na kuandika.

Alisema, sababu inayokwamisha baadhi ya wanafunzi kufika darasa la saba wakiwa hawajui kusoma na kuandika ni pamoja na mazingira ambayo baadhi ya wazazi hawaipi kipaumbele elimu.

Mkurugenzi wa Leap Learning Kanda ya Mashariki, Anna Nigicser, alisema wameshafanya mradi huo katika maeneo ya Pemba, Sengerema, Kasulu na Ngorongo wakilenga zaidi watoto wa kike walio nje ya shule.

Mkurugenzi wa Shirika la Ocode, Joseph Jackson, alisema, mradi huo wameufikisha shuleni hapo kwa majaribio, na kwamba kinachohitajika kwa shule ni kutenga darasa ambalo litakuwa maabara ya kujifunzia.

## Bil. 39/- kutumika Mkuranga

**Na Yasmine Protace, MKURANGA**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, imepitisha bajeti ya Sh. bilioni 39 ambayo itatumika katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021.

Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mkuranga, Juma Abeid, katika kikao maalumu cha baraza la bajeti.

Alisema kiasi hicho cha fedha kimetokana na ruzuku kutoka serikali kuu, mapato ya ndani na fedha kutoka kwa wahisani.

Wakati huo huo, Abeid alisema kuwa wilaya hiyo inatarajia kufungua zahanati saba.

"Tunafungua zahanati saba kutokana na idadi ya watu kuongezeka kila siku," alisema.

## NMB kusaidia serikali mitaa

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imeahidi kutumia bidhaa na huduma zake kuzisaidia serikali za mitaa kufikia malengo yake ya maendeleo na kuchangia ukuaji wa uchumi.

Ikiwa tayari imefikisha huduma za kibenki kwa zaidi ya asilimia 99 ya wilaya zote nchini kupitia mtandao wa matawi 224, zaidi ya ATM 800 na NMB Wakala, inafanya benki hiyo iweze kutoa huduma za kibenki kwa serikali za mitaa ziweze kutekeleza na kusukuma mbele agenda ya maendeleo.

Hayo yalielezwa mwisho wa wiki katika hafla fupi iliyoongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Sophia Mjema, ikiwakutanisha wafanyakazi wa manispaa na wafanyakazi wa Benki ya NMB.

Mkuu wa Kitengo cha Biashara za Serikali wa NMB, Vicky Bishubo, amesema benki hiyo imejizatiti kuendelea kufanya kazi na serikali za mitaa katika kusukuma mbele miradi mbalimbali yenye lengo la kuboresha maisha ya watu.

"Tunafanya kazi na manispaa na halmashauri mbalimbali katika maeneo ya ukusanyaji mapato ya serikali, kutoa mikopo kwa wajasiriamali wadogo wadogo na wa kati, wafanyakazi wa serikali na kupitia sera ya Benki ya majukumu ya kijamii kwa kusaidia huduma za elimu, afya na majanga mbalimbali," alisema.

Kwa mfano, Benki ya NMB NMB mwaka jana ilitoa zaidi ya dhamana 500 kwa makandarasi wazawa ili kuwawezesha kugharamia miradi mbalimbali ya ujenzi nchini.

Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Mjema aliwataka wafanyakazi wa manispaa na wananchi wote wa wilaya hiyo kutumia fursa mbalimbali zinazotolewa na Benki ya NMB katika kuendeleza shughuli mbalimbali za kiuchumi na nyingine kama mikopo ya nyumba.

"Tunatakiwa kuwahusisha kwa karibu wataalamu wa Benki ya NMB katika kutoa ushauri wa kitaalamu na kukopesha baadhi ya miradi inayotekelezwa na manispaa yetu," alisema huku akiipongeza Benki ya NMB kwa kusaidia shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii katika wilaya yake.

Naye Meneja wa NMB Kanda ya Mashariki, Badru Idd, alisema kwa miaka yote tangu ianze kutoa huduma, Benki ya NMB imekuwa ikitumia rasilimali na juhudi zake kutoa huduma za kibenki kuwafikia wale ambao bado hawajapata huduma za kibenki hasa wale wa vijijini.

"NMB imejipanga kiteknolojia kuweza kutolea majibu matatizo mbalimbali ya wananchi katika kupata huduma za kibenki na kuchangia katika ukuaji wa uchumi," alisema.

Meneja Uhusiano, Kitengo cha Wafanyabiashara wa kati na wadogo, Lilian Malekia, alisema wanajipanga inajipanga kuzindua huduma yake mpya kliniki za kibiasha ambazo kupitia klabu za wafanyabiashara wataweza kupokea na kutoa majibu changamoto mbalimbali zinazowakabili wajasiriamali.

"Zaidi ya wajasiriamali ya 300 watashiriki katika kliniki hii ya kibiashara ambayo itaendeshwa sehemu mbalimbali nchini kupitia klabu za kibiashara ambapo taasisi mbalimbali kama Shirika la Viwango nchini TBS, Mamlaka ya Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) na nyinginezo ili kukutana na wafanyabiashara hawa," alisema.

Naye mtaalamu wa bima wa NMB, Catherine Joshua, amewahimiza zaidi ya wateja milioni tatu wa NMB na wengine kuchangamkia huduma za NMB zinazopatikana katika matawi yote ya benki nchini.

# Mkenda aeleza nafasi ya misitu uchumi wa viwanda

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Prof. Adolf Mkenda, amesema misitu ikitumika vizuri ina nafasi nzuri ya kuchagiza ukuaji wa uchumi na ujenzi wa viwanda hapa nchini, jambo ambalo litapunguza tatizo la ajira kwa vijana.

Akizungumza baada ya mkutano wa wadau katika sekta ya misitu kilichoandaliwa na Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) mwishoni mwa wiki ambacho Prof. Mkenda ni Mwenyekiti wa kikosi kazi cha misitu chini ya baraza, alisema misitu mchango wake ni mkubwa sana katika kufanikisha azma ya serikali kufanikiwa ifikapo 2025.

"Huu ni mkutano wa kikosi kazi cha misitu ambacho kinaundwa kwa ushirikiano wa serikali na sekta binafsi ili kuangalia changamoto zinazoikabili sekta hii kwa pamoja. Serikali kazi yetu kuweka mazingira mazuri kwa watu wengine wa sekta binafsi na wadau wa maendeleo wanaojihusisha na biashara ya misitu wafanye biashara yenye tija ambayo itaongezea serikali mapato kupitia kodi," alisema Prof. Mkenda.

Prof. Mkenda alisema wameshafanya vikao vingi kati ya serikali na sekta binafsi na kupitia utafiti mbalimbali za kitaalamu ambazo zinaweza kuunganisha sekta hii mtambuka na ukuaji wa viwanda nchini.

"Ushirikiano wetu na sekta binafsi unaleta manufaa makubwa sana katika kuifanya sekta ya misitu inakua kichocheo muhimu katika maendeleo ya watu na taifa kwa ujumla. Tumekuwa na vikao vingi ambavyo tumekuwa tukipokea na kujadili tafiti mbalimbali za namna ya kuona sekta hii mtambuka inaweza kuchagiza maendeleo ya ukuaji wa viwanda kwani taifa letu limekuwa wazalishaji wakubwa wa malighafi za misitu," alisema.

Alisema kuwa ushirikiano baina ya serikali na sekta binafsi umekuwa mkubwa na wenye tija katika kufikia malengo ya pamoja ambayo ni kuongeza thamani ya mazao ya misitu.

"Mwelekeo wetu kwa pamoja kati ya serikali na sekta binafsi umekuwa mzuri na tunaamini kwamba tunao uwezo wa kufanyia kazi baadhi ya changamoto zilizopo na kuifanya sekta hii kuwa moja ya sekta ambayo

itachangia sana ukuaji wa uchumi," alieleza.

Mwenyekiti mwenza wa kikosi kazi cha misitu kutoka sekta binafsi, Ben Sulus, alishukuru kwa namna ambavyo serikali ya awamu tano inavyoangazia fursa mbalimbali zilizopo hapa nchini ili ziwe kichochea kwa maendeleo ya Tanzania.

"Huko nyuma mijadala ya ushirikishwaji wa watu wa sekta binafsi ulikuwa mdogo hali ambayo ilitufanya tutumie zaidi jitihada zetu binafsi katika kufikia malengo yetu, lakini hali imeimarika sasa, tunapata nafasi ya kutoa maoni yetu, tunashiriki kufanya tafiti mbalimbali na pia tumehamasika vya kutosha kiasi cha kutoa michango yetu ya hali na mali kwa kuwa tunaona mwanga wa kufikia uchumi wa viwanda," alisema Sulus.

Naye Katibu Mkuu Mtendaji wa TNBC, Dk. Godwill Wanga, alisema kuwa baraza litaendelea kuwaleta pamoja wadau wote wa misitu ili kwa pamoja waweze kuangalia changamoto zinazoikabili sekta hiyo muhimu kwa maendeleo ya nchi.




Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo (kushoto), akiwa na Rais wa Shirika la Nutrition International, Joel Spicer (kulia), wakifunua kitambaa ikiwa ni ishara ya ufunguzi rasmi wa ofisi mpya ya shirika hilo jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watumishi lawamani kuwapa siri wanasiasa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama mkoani Shinyanga Michael Matomora, amesikitishwa na baadhi ya watumishi wa halmashauri hiyo ambao wamekuwa wakitoa siri za ndani za halmashauri na kuwapelekea wanasiasa na kuzungumza ndani ya kikao cha Baraza la Madiwani.

Matomora aliyabainisha malalamiko hayo juzi kwenye kikao cha robo ya pili wa mwaka wa fedha wa 2019/20 cha Baraza la Madiwani cha Halmashauri hiyo, na kusema vitendo hivyo sio vya kiugwana na wahusika wanatakiwa kuchukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa sheria za utumishi.

Alisema kuwa moja ya kazi ya wakuu wa idara wa halmashauri ni kumshauri mkurugenzi hasa pale mambo ya maendeleo yanaposhindwa kwenda vizuri nasio kutoa siri za ndani za halmashauri na kuwapelekea madiwani na kuja kuyazungumza ndani ya vikao vya madiwani.

"Mwenyekiti, tabia iliyofanywa na baadhi ya wakuu wa idara wangu ya kutoa siri za halmashauri na kuwapelekea madiwani wako ni jambo la aibu sana...nitafanya uchunguzi wa nani anayewapelekea madiwani siri za ndani na nitahakikisha ninamchujkulia hatua za kidhani," alisema Matomora.

Aidha, Matomora alisema mtambo wa utengenezaji na ufunguzi wa barabara kwenye baadhi ya kata unaposimama kutokana na sababu mbalimbali, watumishi wanapoulizwa na madiwani wanasema mkurugenzi anakwamisha kazi kwa kushindwa kutoa fedha za urekebishaji wa mitambi hiyo.

Hoja hiyo iliibuka baada ya Diwani wa Sabasabini, Emanuel Makashi, kumlalamikia mkurugenzi kwa kuchelewa kuidhinisha fedha za urekebishaji wa mitambo ya utengenezaji na ufunguzi wa barabara mpya kwenye baadhi ya kata.





# Mwarobaini utoboaji bomba maji wapatikana

**Na Novatus Makunga,**
ARUSHA

KAZI ya kujenga mabirika ya kunyweshea mifugo katika vijiji vya Longido mkoani Arusha imeanza, ili kudhibiti vitendo vya utoboaji wa bomba linalopeleka maji makao makuu ya wilaya hiyo vinavyofanywa wakati wa kiangazi na jamii ya wafugaji.

Hayo yalisemwa juzi na Kaimu Meneja wa mradi wa maji Longido, Mhandisi Frederick Mageni, kwa wanahabari waliotembelea mradi huo, ambao umegharimu zaidi ya Sh. bilioni 15.8 na kusimamiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jiji la Arusha (AUWSA).

Alisema mradi huo unakabiliwa na changamoto kubwa wakati wa kiangazi kutokana na chanzo cha maji kuwa Mto Simba uliopo katika Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro na kusafirishwa kwa kilometa 70 hadi katika Mji wa Longido, hivyo jamii ya wafugaji hutoboa bomba katika maeneo linakopita.

Mhandisi Mageni alisema kuwa kuwapo kwa mabirika hayo, kutaondoa tatizo la mahitaji ya maji kwa ajili ya mifugo katika Vijiji vya Sinya, Tingatinga na Elerai.

Katika hatua nyingine, Mhandisi Mageni alisema kazi ya upembuzi yakinifu wa kupeleka maji katika Mji wa Namanga uliopo katika mpaka wa Tanzania na Kenya imeshakamilika na upo katika hatua za mwisho kuanza kuvuta bomba kutoka Mji wa Longido. Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, Namanga ina watu 9,189 huku Longido ikiwa na wakazi 2,285 katika wilaya hiyo yenye jumla ya wakazi 123.153. Akizungumzia mradi huo ambao jiwe la msingi liliwekwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, Septemba 21, mwaka 2017, Mhandisi Mageni alisema una uwezo wa kuzalisha lita zaidi ya milioni 2.1 kwa siku ambapo kwa tangi linalotumika sasa linachukua lita 450,000 tu.

Alisema tangi hilo linasambaza maji kupitia mtandao wa mabomba yenye urefu wa jumla ya kilometa 50 katika Mji wa Longido pamoja na vijiji vya Orbomba, Engikaret, Ranchi na Ortepes.

Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Toba Nguvilla, alisema kukamilika kwa mradi huo kumeongeza kasi ya shughuli za kiuchumi katika wilaya hiyo iliyokuwa nyuma kimaendeleo pamoja na kasi ya ujenzi wa nyumba na miradi ya jamii.

Nguvilla alisema wameanza ujenzi wa hospitali ya wilaya ambayo imetengewa zaidi ya Sh. bilioni 1.9 na ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) ambao umetengewa zaidi ya Sh. bilioni 1.5



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru, Emmanuel Mkongo, akizungumza wakati wa mkutano wa Halmashauri Kuu ya CCM uliofanyika katika ukumbi wa mikutano wa halmashauri hiyo, ambapo alisema halmashauri hiyo kupitia wataalamu wake itaendelea kutekeleza shughuli za serikali kwa uadilifu na kuendana na kasi ya Mheshimiwa Rais inayolenga kuwaletea maendeleo wananchi hususani wanyonge. **PICHA: WOINDE SHIZZA.**

# Wananchi watakiwa kuomba ushauri kisheria

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

HAKIMU Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Longido, Aziza Temu, ameeleza kuwa maadhimisho ya Siku ya Sheria nchini yanatoa mwanya kwa wananchi kusaidiwa elimu ya sheria, hivyo vema wakatumia fursa hiyo kupata ushauri kwenye maeneo yanayowatatiza ili wawe na uelewa juu ya masuala ya sheria.

Alisema Wiki ya Sheria iliyoanza Januari 31 na kuhitimishwa Februari 5, wametoa elimu juu ya sheria kwa wakazi wa Kata ya Sinya Kijiji cha Ildonyo, shule mbalimbalia za sekondari wilayani hapo na kusikiliza na kutatua kero mbalimbali za wananchi kwa kutoa ushauri wa kisheria.

Akizungumzia kauli mbiu ya mwaka 2020, Temu alisema ni wajibu wa mahakama na wadau wote kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji. Alifafanua kuwa uwekezaji ni njia ya kufanya fedha zako zizae zaidi kwa kufanya shughuli ya kuingiza mapato.

Temu alisema, mahakama imepewa mamlaka kikatiba ya kuwa na kauli ya mwisho katika kutoa haki nchini kama ilivyoainisha Ibara ya 107 (A) ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kwamba, katika kutekeleza wajibu wake mahakama inayowajibu wa kulinda utawala wa sheria, utulivu na ustawi wa nchi kwa kuhakikisha haki inapatikana kwa wakati na kutatua migogoro kwa amani.

Aidha, alisema utoaji haki kwa wakati hususani kwa mashauri yanayohusu migogoro ya kibiashara bila kujali nafasi ya mtu kwenye jamii, kuzingatia sheria na kanuni, kufanya usuluhishi pale inapowezekana ni nguzo muhimu katika kuweka mazingira bora na wezeshi kwa kuvutia uwekezaji na biashara kwenye taifa huru linalozingatia haki. "Hivyo ni jukumu la Mahakama kuhakikisha migogoro ya biashara na uwekezaji inatatuliwa kwa wakati na weledi wa juu ili kuhakikisha uchumi wa nchi na uchumi wa mtu binafsi hauwezi kudorora," alisema Temu.

Alisema Mahakama ya Tanzania katika kutekeleza jukumu lake la msingi la utoaji haki limejiwekea mpango mkakati wamiaka mitano, utakaoifanya mahakama kuwa chombo kinachowajibika zaidi kwa wananchi, ikiwa ni kubadili mtazamo wa wananchi kuhusu taswira ya mahakama katika utoaji haki ili kuongeza imani ya wananchi na wadau.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Frank Mwaisumbe, akitoa salamu kwa wananchi walihudhuria maadhimisho hayo, alisema serikali inawajibu wa kuandaa mazingira mazuri ya uwekezaji, pamoja na kuwataka wawekezaji kufuata sheria za nchi na kuheshimu maeneo waliyowekeza shughuli zao.

"Pamoja na kuhitaji wawekezaji wanatakiwa kufuata sheria za nchi na kuangalia haki za msingi za wananchi wa sehemu aliyowekeza," alisema Mwaisumbe.

# Watakiwa kuhama kwenye mafuriko

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Karatu, Theresia Mahongo, ametoa wito kwa wananchi waliojenga na wanaoendelea kujenga nyumba katika mikondo ya maji kuondoka maeneo hayo, kwa sababu si salama.

Alitoa wito huo juzi alipofanya ziara ya kuwatembelea na kuzungumza na waathirika wa mafuriko yaliyotokea Kata ya Mang'ola, akiwa ameambatana na kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya.

Mahongo alitembelea Kijiji cha Langharerir ambacho wananchi 15 nyumba zao zimebomolewa na mvua zinazoendelea kunyesha na katika kijiji cha Malechand wananchi 30 nyumba zao zimeathirika na mafuriko ya pamoja na Mang'ola Barazani nyumba 44 zimebomoka kutokana na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha.

"Nawaomba wananchi kujenga nyumba za kudumu katika maeneo ambayo hakuna mikondo ya maji na watu wanaoishi mabondeni na kwenye mikondo ya maji wachukue tahadhari na kuondoka maeneo hayo," alisema.

Mahongo aliwaagiza watu waliojenga kwenye miteremko ya maji kuondoka kwa sababu wanachangia wenzao kupata mafuriko yasio ya lazima.

Aliwapongeza wananchi wa Malechand kwa kuchukua tahadhari mapema ya kuondoka maeneo yenye mafuriko na kutafuta makazi ya muda.

"Nilipoambiwa wananchi wa eneo hili wameondoka niliekeza uongozi wa Malechand kukaa kikao cha kijiji ili kuweka utaratibu wa waathirika kuweka makazi ya muda katika ofisi za maji," alisema.

Mahongo alisema pamoja na wananchi hao kukaaa katika eneo hilo la muda ameelekeza viongozi wa kijiji kuweka katika maandishi mkataba na kuwapa waathirika hao eneo, ili wakae kwa muda kwenye eneo hilo lililotengwa kwa makazi ya dharura.

Alisema lengo la kuandikisha waathirika hao ili kuepusha mkanganyiko siku za usoni juu ya namna walivyopewa idhini ya kuweka makazi ya muda katika ofisi za maji zilizopo Malechand.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Malechand, Marco Yoyo, alisema kitendo cha kuwasiliana na wananchi wenzao walio nje ya Malechand kimewasaidia kuwapa taarifa mapema hivyo kunusuru athari za mafuriko.

Yoyo alisema kwa kushirikiana na Ofisa Tarafa walipiga mbiu kuwapa tahadhari juu ya mafuriko huku akibainisha kuwa watu wasio na makazi walienda kujisitiri kwa ndugu jamaa na marafiki na hakuna mifugo iliyokwenda na maji.



# Kinapa yachangia miradi ya maendeleo bil. 4.4/-

**Na Mary Mosha,** MOSHI

HIFADHI ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro (KINAPA), imechangia miradi ya maendeleo 48 yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 4.4 katika vijiji vinavyozunguka mlima huo, kwa kipindi cha miaka 10.

Lengo la hatua hiyo limeelezwa ni utekelezaji wa mpango wake wa ujirani mwema.

Aidha, katika bajeti ya hifadhi hiyo kwa mwaka 2019/2020 jumla ya miradi 25 yenye thamani ya Sh. milioni 899.5 inaendelea kutekelezwa kwenye vijiji mbalimbali vinavyopakana na mlima huo.

Kamishna wa Kanda ya Kaskazini, wa Shirika la Hifadhi za Taifa nchini (TANAPA), Herman Batiho, alisema hayo alipokuwa akitoa taarifa kwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, kwenye ufunguzi wa vyumba vitatu vya madarasa na ofisi ya walimu katika Shule ya Msingi Mweka wilayani Moshi.

"Mradi huu umelenga kuboresha kiwango cha elimu katika shule hii ambayo ilikuwa na changamoto za upungufu wa madarasa, madawati na ofisi ya walimu, umegharimu Sh. milioni 123.3, ambapo Tanapa imetoa Sh. milioni 120.4 na michango ya wananchi Sh. milioni 2.8," alisema.

Kamishna Batiho alisema baadhi ya miradi ni awamu ya pili ya utekelezaji kwa miradi ya mwaka 2018/2019 katika Wilaya ya Moshi ambapo inatekelezwa katika vijiji 10 katika wilaya hiyo.

Alivitaja vijiji hivyo ni Mowo, Kokirie, Mahoma, Arisi, Mshiri, Kinyamvuo, Mbahe, Omarini, Kimanganuni na Lyasongoro.

"Lengo la Tanapa katika kutekeleza miradi hii ni kutimiza azma yake ya kutoa sehemu ya mapato yake kwa jamii ili wananchi wapate manufaa yatokanayo na shughuli za uhifadhi," alisema.


Kamishna Batiho alisema miradi yote ni matunda ya idara ya ujirani mwema kwani hifadhi hiyo imepakana na vijiji 92 katika wilaya za Hai, Moshi, Rombo, Siha na Longido ambapo pia vimepewa elimu kuhusu hifadhi ya mazingira.

Akizindua madarasa hayo, Mghwira alitaka viongozi wa vijiji na Kinapa kutoa elimu ya uhifadhi wa mazingira kwa watoto na faida za uwepo wa mlima kwa ajili ya utalii.

Alitaka hifadhi kutoruhusu watoto kuingia msituni kwa ajili ya kuokota kuni kwani kwa kufanya hivyo ni sehemu ya uharibifu wa mazingira na wanaweza kudhurika kwa kuingia humo bila utaratibu.

Mghwira alimwomba katibu tawala wa mkoa kuandaa safari ya kutwa ya kupanda Mlima Kilimanjaro kwa ajili ya kubaini changamoto za mlima pamoja na kuona maeneo korofi kutafuta ufumbuzi.

Pia, safari hiyo itatoa fursa ya kutoa maelekezo ya wapi wananchi wasifike na wapi wafike kwa maslahi ya hifadhi ya mazingira.



Mwakilishi wa Benki ya CBA, Gloria Njiu (kushoto), akimkabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 10 mshindi wa shindano la promosheni ya Tunza Utunzwe na M-Pawa, Joseph Mkombozi kutoka Kijiji cha Makole, Muheza mkoani Tanga, hafla hiyo ya makabidhiano ilifanyika viwanja vya Zakhem Mbagala jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Chanjo ya mifugo yatolewa Siha

**Na Mary Mosha,** SIHA

SERIKALI wilayani Siha imetoa chanjo ya magonjwa ya kimeta, miguu na midomo, mdondo na kichaa cha mbwa.

Jumla ya ng'ombe 16,822, kuku 58,040, kondoo 1,400 na mbwa 2,150 wamechanjwa kwa gharama ya Sh. 24,400,000.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Onesmo Buswelu, aliyasema hayo jana wakati akitoa taarifa yake ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi kwa Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Kilimanjaro, Jonathan Mabihya.

Alisema serikali imechukua hatua ya kuendeleza sekta ya mifugo kwa kuzuia kuenea kwa magonjwa na kuweza kupunguza vifo vitokanavyo na magonjwa ya mifugo kwa asilimia 20.

"Serikali imeamua kuboresha ng'ombe wa maziwa kwa njia ya uhamilishaji ambapo ndama 1,450 walizalishwa kwa Sh. 21,750,000 kuongeza uzalishaji wa maziwa kutoka wastani wa lita sita hadi nane kwa siku kwa ng'ombe mmoja." Buswelu alisema hatua hiyo ipo sambamba na kuboresha mfumo wa maziwa na soko la maziwa kwa kuanzisha vyama vya ushirika wa maziwa vilivyosajiliwa na imetoa mafunzo bora ya uzalishaji wa ng'ombe wa maziwa na utunzaji wa maziwa kwa wafugaji 850 kwa gharama ya Sh. 17,000,000.

"Serikali imeboresha soko la maziwa kwa kuhamasisha wanunuzi wa maziwa kuwa na matangi ya kupoozea maziwa katika maeneo ya wafugaji ambapo hadi sasa matangi manne yameshawekwa Kilingi, Sanya Juu na Kishisha yenye thamani ya Sh. milioni 96," alisema.

Aliongeza kuwa serikali imetoa mafunzo ya usindikaji maziwa kwa vikundi vinne vya ukusanyaji maziwa venye wafugaji 96 na kusaidia vijana wanaojishughulisha na utengenezaji malisho bora kwa mifugo (SILAGE) kwa kuwaunganisha na wadau wa maziwa na kufanikiwa kupata mashine ya kusindika vyakula vya mifugo yenye thamani ya shilingi 13,5000,000 .

"Tumefanikiwa kuanzisha mashamba darasa ya malisho 12 kwa kushirikiana na wafugaji wenye maeneo ya malisho katika maeneo ya Gararagua, Nganony, Kishisha, Sabuko, Merari, Nasai, Sanya Juu, Kilingi na Wanri," alisema.

Alisema hatua hiyo pia imefanikisha kuanzisha kilimo cha malisho ya mifugo (Hai) kupitia shamba la ranchi ya taifa Narco iliyopo West Kilimanjaro na kufanikiwa kuongeza idadi ya mifugo na ufugaji wa farasi katika ranchi hiyo.

Mmoja wa vijana, Nelson Nko alisema ununuliwaji wa mashine ya kusindika malisho sanjari na elimu ya usindikaji wa maziwa, huku serikali ikiboresha soko la maziwa nchini kutaweza kusaidia kutokomeza tatizo la ajira nchini.

"Tunaiomba wizara kuangalia namna ya kuwekeza katika usindikaji wa maziwa na utengenezaji wa malisho bora. Kutaweza kuwasaidia vijana wengi kwenye tatizo la ajira nchini," alisema Nelson.

## Waziri akunwa ujenzi kiwanda

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, ametembelea na kukagua ujenzi wa majengo ya kiwanda kipya cha bidhaa za ngozi kinachojengwa katika eneo la Gereza Kuu Karanga, Manispaa ya Moshi mkoani Killimanjaro na kuridhishwa na hatua kubwa zilizofikiwa.

Utekelezaji wa ujenzi wa mradi huo wa ubia kati ya Jeshi la Magereza na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa PSSSF upo katika awamu na umefikia asilimia 60 ya ujenzi wa majengo yote manne ambapo unatarajiwa kukamilika Machi 2, 2020, hivyo, kuwezesha ufungaji wa mashine mbalimbali za kiwanda hicho.

"Nimefarijika sana kwa hatua zilizofikiwa za ujenzi, leo makamanda kwa kweli niwapongeze kwa kazi hii endeleeni kusimamia ujenzi huu kwa kasi kwani kiwanda hiki kina umuhimu mkubwa kwa upande wa serikali na manufaa ya kiwanda hicho ni ya kiuchumi," alisema Mhagama.

Waziri Mhagama aliongezea lengo la serikali ni kuhakikisha kuwa kiwanda hicho kinakamilika mapema kwani kina manufaa makubwa kwa taifa ikiwemo kutoa fursa nyingi za ajira kwa watanzania pamoja na kuongeza mapato serikalini.

Aidha, Waziri Mhagama amemwagiza Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu), Andrew Massawe, kuhakikisha anaandaa mpango kazi wa utekelezeji wa mambo yote muhimu yanayohusiana na kiwanda hicho ili kuanza uzalishaji baada ya ujenzi wake kukamilika.

"Tunapoendelea na ujenzi wa kiwanda hiki ni lazima twende sambamba na mambo mengine muhimu ikiwamo upatikanaji wa maji ya kutosha, usimikaji wa miundombinu ya umeme pamoja na kufanya maandalizi ya masoko ya bidhaa zitakazokuwa zikizalishwa na kiwandani," alisisitiza Mhagama.

Mhandisi wa mradi huo, Mrakibu wa Magereza, Julius Sukambi, alisema kuwa utekelezaji wa mradi unafanyika usiku na mchana kwa kutumia wataalamu wa Jeshi la Magereza, wafungwa na mafundi raia wa fani mbalimbali ikiwa ni jitihada za kuwezesha kukamilisha mradi huo kama ilivyokusudiwa.

NIPASHE JUMATATU FEBRUARI 10, 2020

Nipashe

Spotika



NYOTA 10 EPL WENYE THAMANI ZAIDI KWA SASA UK. 16&17



# MSHIKEMSHIKE...

Mshambuliaji wa Yanga, David Molinga (kushoto), akimiliki mpira huku akipata kashikashi kutoka kwa mchezaji wa Ruvu Shooting, Zuberi Badi, katika mchezo wa Ligi Kuu uliochezwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam juzi. Yanga ilishinda bao 1-0. HABARI UK. 18. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## ISIKUPITE

MABAO mawili aliyofunga Mohamed Salah wakati Liverpool ikishinda 4-0 dhidi ya Southampton kwenye Ligi Kuu England wiki moja iliyopita yanamaana kuwa sasa amefunga mabao mengi (12) akiwa uwanja wa nyumbani, Anfield kuliko mchezaji yeyote katika ligi hiyo msimu huu. Wanaomfuata kwa karibu ni Marcus Rashford (10) na Sergio Aguero (8).



SOKA

# NJIA 3 ZA SOARES KUISAIDIA ARSENAL



CEDRIC SOARES

**LONDON,** England

ARSENAL walionekana kuwa 'bize' sana kwenye usajili wa dirisha la Januari, ingawa walisubiri hadi dakika ya mwisho kabisa kuweza kusajili wachezaji. Walimsajili Pablo Mari kutoka Klabu ya Brazil ya Flamengo na pia wakamsajili dakika za majeruhi, Cedric Soares kutoka Southampton, wote wakiwa wametua kwa mkopo hadi mwishoni mwa simu.

**Cedric ni mlinzi wa pembeni mwenye kipaji ambaye alitengeneza jina lake nchini England tangu alipowasili pale Southampton mwaka 2015. Na sasa akiwa kwenye mwaka wake wa mwisho wa mkataba, atacheza kwa 'Washikabunduki' hao wa London hadi mwishoni mwa msimu.**

Chini ya Mikel Arteta, muda utakuwa wa kuvutia zaidi kwa Soares kwani atakuwa ameingia kwenye mradi mpya. Arsenal itamhakikisha raia huyo wa Ureno kupata mechi nyingi za kucheza kwa sababu amenunuliwa wakati ambao wanakabiliwa na majeruhi kwenye safu yao ya walinzi wa pembeni.

Hapa tunaangalia njia tatu ambazo Cedric Soares atainufaisha Arsenal...

**1. UZOEFU WA KUTOSHA**

Kitu kimoja ambacho Soares atawapa faida kubwa Arsenal ni uzoefu wake, ingawa si mwenye umri mkubwa. Beki huyo ameichezea timu kama Inter Milan, Southampton, Sporting CP na bila shaka timu ya Taifa ya Ureno. Katika timu zote hizo amecheza pamoja na wachezaji wakubwa kwenye mchezo huo akiwamo Cristiano Ronaldo.

Hivyo ni sawa na kusema raia huyo wa Ureno ataleta uzoefu wa kutosha zaidi kwa timu ya Arsenal, kikosi ambacho kina wachezaji wengi vijana. Anaweza kuonekana kama mchezaji mwingine kijana wa Arsenal, akiwamo Bukayo Saka ambaye ameng'ara kwenye nafasi yake ya ulinzi.

Soares amejifunza mengi kuhusu mchezo huo kwa kucheza na wachezaji wenye uzoefu na ambao amejifunza mengi kutoka kwao.

**2. UWEZO WA KUCHEZA NAFASI ZAIDI YA MOJA**

Kitu kinachoisumbua Arsenal ni majeruhi ya mara kwa mara kwa wachezaji wake. Kwa kawaida timu ya madaktari wao imekuwa bize zaidi kwani mara nyingi imekuwa kawaida kuona mchezaji mmoja akiumia wakati wowote.

Kwa sasa Arsenal itakabiliwa na uhaba wa mabeki, kwani Calum Chambers, Sead Kolasinac na Kieran Tierney wote ni majeruhi na hilo ndilo lililomshawishi Cedric Soares kujiunga na Arsenal. Wanamhitaji kuziba nafasi ya majeruhi hao.

Habari njema kwa Arsenal ni kwamba, Cedric ana uwezo wa kucheza zaidi ya nafasi moja, iwe beki zote, kiungo au nafasi ya winga. Nafasi anayopendelea kucheza ni kulia, lakini hiyo itakuwa na Hector Bellerin, hivyo ikihitajika Arteta anajua kwamba Mreno huyo atamchezesha beki ya kushoto.

**3. UWEZO WA KUKABA**

Cedric anachukulia kama tishio katika watatu wa mwisho na hilo halina shaka kabisa. Na kitu cha kufurahisha zaidi kutoka kwake ni kupenda kucheza kwa ushirikiano. Kiutamaduni yeye ni beki wa pembeni na amekuwa na uwezo mkubwa wa kusaidia kusukumiza mashambulizi mbele.

Hilo litamfanya aishinde mioyo ya mashabiki wa Arsenal kama ilivyokuwa kwa nyota Mesut Ozil na Hector Bellerin ambao sasa wanaonekana kuchokwa, ingawa wawili hao wameanza kuimarika chini ya utawala mpya.

Cedric hana hofu linapokuja suala la kutumia mwili wake kulinda mashambulizi langoni mwake. Wakati Arteta akiangalia namna ya kurudisha ubora wa safu ya ulinzi ya Arsenal uwezo wa beki huyo utaisaidia zaidi Arsenal. Na kwa namna moja au nyingine Cedric atakuwa nguzo muhimu kwa Arsenal katika kukaba na kuzuia mashambulizi langoni mwao


**JE, WAJUA?**

TANGU kuanza kwa msimu wa 2016-17, ni Jamie Vardy pekee aliyefunga mabao mengi (6) dhidi ya timu ya Pep Guardiola, Manchester City kuliko mshambuliaji wa Spurs, Son Heung-min (5) katika mashindano yote.



## MICHEZO

# SABABU 4 SIMBA KUSHUKA KIWANGO



Kiungo mshambuliaji mpya wa Simba Luis Miquissone, anayetarajiwa kuiamsha timu hiyo, akikokota mpira mbele ya mabeki wa JKT Tanzania kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa Ijumaa iliyopita na kuchapwa bao 1-0. **PICHA: MAKTABA**

**Na Adam Fungamwango**

TANGU ilipocheza mechi dhidi ya Yanga Januari 4, mwaka huu, timu ya Simba haijarejea tena kwenye kiwango chake cha kawaida.

**Kuanzia hapo ilionekana kuwa na kiwango kibovu kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi Zanzibar mpaka kwenye mechi ya Kombe la FA dhidi ya Mwadui FC.**

Baada ya hapo ikicheza mechi za Ligi Kuu, dhidi ya Mbao FC na kushinda mabao 2-1, dhidi ya Alliance FC ikashinda 4-1, dhidi ya Namungo ikashinda 3-2, na Coastal Union ikashinda 2-0, huku dhidi ya Polisi Tanzania ikishinda 2-1, kabla ya kukutana na kipigo cha bao 1-0 dhidi ya JKT Tanzania.

Kwa jinsi kila mechi za Simba zilivyozidi kusonga mbele, ilionekana kabisa kuwa kuna mechi itakuja kupoteza siku za karibuni kutokana na ushindi wake ambao ilikuwa ikiupata kwa mbinde, zingine ikisubiri dakika za mwisho au majeruhi.

Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck amesema walipoteza mchezo wa Ijumaa dhidi ya JKT Tanzania kutokana na kukosa bahati kwani walitengeneza nafasi nyingi.

Aidha, Sven amesema wachezaji wote wa Simba ni wazuri na yeyote anaweza kumtumia na wakapata matokeo.

Mbelgiji huyo ametoa kauli hiyo baada ya kutupiwa lawama kuwa haeleweki katika upangaji wa timu. "Kilichotokea ni sehemu ya mpira hakuna wa kumlaumu, ni kweli tulibadilishiwa uwanja kutoka Taifa hadi Uhuru na pia tuliwakosa baadhi ya wachezaji kutokana na kuwa majeruhi, lakini huwezi kusema ndicho kilichosababisha kupoteza mchezo. Timu yetu ina wachezaji wazuri ambao wanaweza kucheza mechi yoyote na wakaipa Simba ushindi," alisema.

Sven pia amelaumu ukaribu wa michezo jambo linalosababisha 'fatiki' (kuchoka) kwa wachezaji. Labda ambacho hajakielewa kocha huyo ni kwamba msimu uliopita Simba ilipotoka kucheza mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika, ilikuwa ikicheza mechi zake za viporo kila baada ya siku mbili, tena zingine ikitakiwa kusafiri, lakini ilifanya vizuri.

Lawama zimekuwa nyingi kwa wanachama na mashabiki wa Simba, nyingi wakizielekeza kwa kocha na zingine kwa wachezaji.

Mwandishi wa makala haya ameorodhesha baadhi ya sababu ambazo zimeifanya timu hiyo iliyokuwa bora kabisa kwa Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati kushuka kiwango ghafla tu.

### HAINA KIKOSI CHA KWANZA CHA KUDUMU

Simba ya safari hii inaonekana haina kikosi cha kwanza cha kudumu, badala yake wachezaji wengi wamekuwa wakibadilishwa mara kwa mara na kusababisha kutoelewana.

Kocha Sven ni kama bado anajaribu wachezaji ili kila mmoja aangalie ubora wake, lakini hilo nalo ni moja ya jambo linalomgharimu kwa sasa.

Anajaribu mabeki na akiona mechi hii wamefanya makosa, mechi ijayo anawajaribu wengine ambao nao wanakuwa bado hawajazoeana, hivyo makosa kuwa ni yale yale ya siku zote.

Upande wa viungo nako amekuwa akifanya hivyo hivyo, wakati mwingine wakiweka viungo wawili au watatu ambao hawana kasi, kitu ambacho kinasababisha kuchelewesha mpira bila sababu za msingi. Hata anapoweka viungo wenye kasi kama Francis Kahata na Hassan Dilunga na timu ikacheza vema, mechi inayofuata anabadilisha tena na kurudi kule kule.

### KUCHEZESHWA KWA STRAIKA MMOJA

Moja kati ya mambo ambayo Sven anafeli ni kumchezesha straika mmoja tu na kuweka viungo wengi ambao mara nyingi hawana msaada mkubwa zaidi ya kupaka rangi mipira na kufurahisha jukwaa tu.

Viungo ambao nimewaona kwa sasa Simba ambao wana uwezo wa kuchezesha timu ukaona inacheza na kuleta kashikashi golini kwa wapinzani ni Hassan Dilunga na Francis Kahata.

Wengine wakipata mpira ni kama vile wapo mazoezini au wanafanya 'jogging'. Wanachukua muda mrefu kujivutavuta na kusababisha wapinzani kurudi nyuma na kujipanga vizuri kwenye kuzuia.

Kocha kwa sasa anamchezesha Meddie Kagere peke yake mbele ambaye anakosa msaada wa straika mwenzake mmoja ili mabeki wote wasiwe wanamkaba yeye pekee.

Msimu uliopita walipokuwa wakianzishwa na Bocco, mabeki wanagawana majukumu kwa sababu Bocco naye si straika wa kukabwa na beki mmoja, hivyo Kagere anakuwa amepunguziwa mabeki na kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kufunga.

Kumbuka kuwa Simba pia ilikuwa na kiungo mshambuliaji au winga, Emmanuel Okwi aliyekuwa akiogopewa na mabeki, mwenye uwezo na ujuzi wa kupiga chenga za maudhi, kasi na uwezo wa kufunga pia, hivyo alikuwa akiwasababishia Kagere na Bocco wakati mwingine kuwa huru zaidi kwenye eneo la hatari la wapinzani.

Viungo wote wa sasa Simba hawana uwezo kama Okwi, ongeza na kuwekwa straika mmoja tu mbele ambaye anaangaliwa muda wote na mabeki.

Ndiyo maana hata krosi zikipigwa kwa sasa hazina madhara kwa sababu, kama Kagere akiwa amekwenda pembeni, hakuna hata kiungo mmoja wa Simba anayeonekana yupo golini akipambana kutaka kufunga mipira ya vichwa, labda mara moja moja Gerson Fraga tu ambaye ni kiungo mkabaji.

Hata kwa mabeki, Simba ina tatizo la beki tangu msimu uliopita, lakini lilikuwa halionekani sana hasa kwenye mechi za Ligi Kuu, au Ligi ya Mabingwa inapocheza nyumbani kwa sababu viungo wake wanakuwa wanakaa sana na mpira, huku mastraika nao wakiwa tishio, hivyo kuwapa nafasi mabeki kupumua na kutoshambuliwa sana.

### KUTOKUWA NA STAMINA, KUSHINDWA KUKABA

Inashangaza kuona kikosi cha Simba kikiwa na makocha wawili wa mazoezi ya viungo, lakini hawana stamina kwa siku za karibuni na kusababisha kushindwa kunyang'anya mipira inapokuwa kwa wapinzani wao.

Wachezaji wa Simba wanaonekana kushindwa kuupata mpira wanapokuwa mmoja kwa mmoja na mchezaji wa timu pinzani, isipokuwa Fraga, Kapombe na kidogo Paschal Wawa.

Waliobaki wanashindwa kupambania mpira unapokuwa haupo kwenye himaya yao na kusababisha matatizo makubwa kwa mabeki.

Utimamu wa mwili kwa siku za karibuni ni tatizo kubwa kwa kikosi hicho, kiasi kwamba wengi wanajiuliza kama huwa wanakaa kambini au wanatokea majumbani.

### KUCHEZA KAMA WAMERIDHIKA, AU DHARAU

Kwa sasa inaonekana wachezaji wa Simba wanachezea jina la timu, au uwezo wa kipesa wa klabu yao na wanazolipwa unaonekana kama unawapa kiburi na dharau dhidi ya timu pinzani.

Wachezaji wa Simba wanapoanza mpira wanaonekana kama kucheza kwa dharau hivi, wakiona kama vile wanacheza na timu ambazo si zaidi yao. Unapotaka kuamini hivyo, angalia inapobaki dakika kama 20 hivi halafu wamefungwa, hapo ndiyo wanaanza kupambana na unaona uwezo halisi wa wachezaji hao.

Unajiuliza kama wangeanza kucheza hivyo tangu mwanzo, si wangepata mabao mengi ya mapema?

Dakika 20 za mwisho ndiyo ambao wachezaji wanakimbia zaidi kuliko kunyata kama wanavyofanya kipindi cha kwanza. Cha ajabu hata kocha Sven karibuni kila siku mpira ukiisha akihojiwa na waandishi wa habari utasikia anasema kipindi cha kwanza tulicheza taratibu, lakini kipindi cha pili tuliamka. Ni mechi ya sita sasa hali inakuwa hivyo hivyo, lakini harekebishi na yeye ndiye kocha, lakini cha ajabu na yeye pia analalamika.

### NJE YA UWANJA

OLEKSANDR Zinchenko amekuwa mchezaji wa tatu Manchester City kutolewa nje ya uwanja kwa kadi nyekundu kwenye Ligi Kuu England msimu huu, hakuna timu ambayo wachezaji wake wamezawadiwa kadi nyekundu nyingi zaidi kama kikosi hicho cha Pep Guardiola msimu huu wa 2019-20.



# NYOTA 10 EPL WENYE THAMANI ZAIDI KWA SASA




Mohamed Salah na Sadio Mane wa Liverpool wakipongezana. **PICHA: MTANDAO**

**LONDON,** England

LIGI Kuu ya England imekuwa ikipokea wachezaji nyota kutoka sehemu mbalimbali duniani kote.

Kutokana na umaarufu wake, ligi hiyo imeshuhudia wachezaji wa madaraja mbalimbali wakitua hapo, huku wengi wao wakiwa ni wale wa daraja la juu kabisa.

**Si jambo la ajabu kushuhudia wachezaji wa daraja la juu wakicheza katika timu zilizopo katikati ya msimamo wa Ligi Kuu, na hii ina maana moja tu, kwamba ni kwa namna gani ligi hiyo ilivyo na ushindani mkubwa.**

Makala haya yanakuchambulia wachezaji 10 wenye thamani kubwa zaidi kwa sasa katika Ligi Kuu ya England msimu huu wa 2019/20...

### 10. VIRGIL VAN DIJK (LIVERPOOL) – PAUNI MIL. 90

Mashabiki wengi wa soka walishangazwa sana na uamuzi wa Liverpool kutumia pauni milioni 75 kumnunua Virgil van Dijk kutoka Southampton. Beki huyo wa kati alikuwa mzuri, lakini hakuna aliyefikiria kama angekuwa bora zaidi.

Van Dijk ndani ya miaka yake miwili amejithibitishia mwenyewe kwamba ni mmoja wa mabeki bora zaidi kwa sasa duniani. Hata ile fedha aliyonunuliwa sasa inaonekana kuwa ilikuwa ndogo kutokana na kiwango bora kabisa anachokionyesha pale Anfield huku washambuliaji wakubwa duniani wakishindwa kumpita kwa urahisi.Na sasa anatajwa kwamba ana thamani ya pauni milioni 90 sokoni na unaweza kujikuta ukitakiwa kulipa fedha nyingi zaidi kama timu hiyo ikitaka kumuuza.

### 9. LEROY SANE (MANCHESTER CITY) – PAUNI MIL. 90

Leroy Sane amecheza mchezo mmoja tu kwa Manchester City katika Ligi Kuu ya England msimu huu kabla ya kupatwa na majeruhi yaliyomuweka nje ya dimba hadi sasa, lakini hilo halijapunguza thamani yake. Kila mmoja anamtarajia kuwa bora kama alivyokuwa kabla hajaumia, kwa sababu ana kipaji cha aina yake.

Ongeza na umri wake, kwani ndio kwanza ana miaka 24, na ana nafasi kubwa sana ya kuendelea kuwa bora na hivyo haiwezi kushangaza ukitajiwa bei yake kuwa ni zaidi ya pauni milioni 100.

Sane alijiunga na Manchester City mwaka 2016 kwa ada ya pauni milioni 45 akitokea Schalke, ingawa thamani yake sokoni ilikuwa ni pauni milioni 27. Katika kipindi cha miaka minne tangu atue hapo, thamani ya Sane ilipanda hadi kuwa pauni milioni 63. Lakini sasa thamani yake sokoni imepanda zaidi kufikia pauni milioni 90.

### 8. BERNARDO SILVA (MANCHESTER CITY) – PAUNI MIL. 90

Sidhani kama kuna mtu yeyote kwa sasa anaweza kuhoji ubora wa mchezaji Bernardo Silva. Thamani yake ya pauni milioni 90 kwa sasa sokoni inatoa taswira namna gani kiwango chake kilivyo bora na hasa ukizingatia kwamba ndio kwanza ana umri wa miaka 25.

Man City walilipa pauni milioni 45 kwa Monaco ili kumsajili wakati wa kipindi cha majira ya joto mwaka 2017 - na sasa hawafikirii tena kumuuza mchezaji huyo. Katika mechi 20 alizoichezea City msimu huu, Silva amefunga mabao matano na kutoa pasi za mwisho nne.

### 7. TRENT ALEXANDER-ARNOLD (LIVERPOOL) – PAUNI MIL. 99

Mwaka mmoja uliopita, Trent Alexander-Arnold aliingia rasmi kwenye kikosi cha kwanza cha Liverpool na kujithibitishia kuwa yeye ni beki wa kulia chaguo la kwanza na wakati huo alikuwa na thamani ya pauni milioni 40. Mwaka mmoja baadaye, yeye ni mmoja wa mabeki bora zaidi wa Liverpool na pia amejipambanua mwenyewe kuwa mmoja wa mabeki bora wa kulia duniani kwa sasa na thamani yake sokoni imefikia pauni milioni 99.

### 6. KEVIN DE BRUYNE (MANCHESTER CITY) – PAUNI MIL. 135

Kiwango cha Kevin De Bruyne pale Manchester City kimekuwa cha kuvutia zaidi kwa misimu ya hivi karibuni. Chelsea kwa sasa watakuwa wanajilaumu wenyewe kwa kutompa nafasi ya kutosha raia huyo wa Ubelgiji wakati akicheza pale kuanzia mwaka 2012 hadi 2014. Alinunuliwa kutoka Wolfsburg kwa pauni milioni 20 na kabla hajasajiliwa pale City, thamani yake sokoni ilipanda hadi kuwa pauni milioni 65.

Akiwa na umri wa miaka 28 kwa sasa, De Bruyne thamani yake ni pauni milioni 135.

### 5. HARRY KANE (TOTTENHAM HOTSPUR) – PAUNI MIL. 135

Nahodha huyu wa Spurs ameendelea kuwa na wakati bora zaidi wakati huu akicheza kwenye Ligi Kuu ya England, lakini mshindi huyo wa Kiatu cha Dhahabu kwenye Kombe la Dunia mwaka 2018, thamani yake imezidi kupanda kila mwaka. Thamani yake ilikuwa pauni milioni 90 kabla ya mashindano hayo, lakini haraka ikapanda hadi pauni milioni 110 baada ya kumaliza kuwa mfungaji bora. Sasa ni miaka miwili imepita, thamani ya Kane imepanda hadi pauni milioni 135.

### 4. MOHAMED SALAH (LIVERPOOL) – PAUNI MIL. 135

Mohamed Salah, kama ilivyokuwa kwa Kevin De Bruyne, ni mchezaji ambaye Chelsea wanajutia sana kumuuza haraka. Blues hao walimuuza Salah kwenda Roma mwaka 2016 kwa thamani ya pauni milioni 13, na Liverpool ikamsajili baada ya mwaka moja kwa pauni milioni 35.

Salah msimu wake wa kwanza kurudi tena EPL aliipiku rekodi ya Cristiano Ronaldo ya kufunga mabao 31 katika mechi 38, huku yeye katika mechi hizo akifunga mabao 32. Tangu hapo ameendelea kuwa nguzo muhimu ya mafanikio ya Liverpool na sasa Salah thamani yake imepanda na kuwa pauni milioni 135.

### 2. SADIO MANE (LIVERPOOL) – PAUNI MIL. 135

Sadio Mane ni mmoja wa wachezaji wengi wenye vipaji waliosajiliwa Liverpool kutokea Southampton kwa miaka michache iliyopita. Mane amekuwa nguzo muhimu ya kufunga mabao tangu aliponunuliwa kwa pauni milioni 40 kipindi cha majira ya joto mwaka 2016.

Sadio Mane, pamoja na Firmino na Salah, wametengeneza safu bora zaidi ya ushambuliaji pengine duniani kote kwa sasa.

Kwa sasa anashikilia rekodi ya kufunga 'hattrick' ya haraka zaidi kwenye Ligi Kuu ndani ya dakika mbili na sekunde 56 (katika ushindi wa 6-1 dhidi ya Aston Villa msimu wa 2014/15). Lakini sasa thamani ya Mane imepanda sana sokoni na kuwa pauni milioni 135.

### 1. RAHEEM STERLING (MANCHESTER CITY) - PAUNI MIL. 144


Raheem Sterling ndiye mchezaji mwenye thamani kubwa zaidi sokoni katika Ligi Kuu ya England kwa sasa sokoni anatamba kwa pauni milioni 144.

Sterling ndio kwanza ana umri wa miaka 25, ni mchezaji aliyekamilika ambaye kila klabu ni ndoto kuwa naye.

Sterling alikuwa na kiwango cha kuvutia akiwa na England kwenye Kombe la Dunia mwaka 2018, na thamani yake ikapanda kutoka pauni milioni 81 hadi pauni milioni 108. Na sasa thamani yake imezidi kupanda na kufikia pauni milioni 144.

## Nukuu

"Nafikiri wakati unapowazungumzia wachezaji, unatakiwa kuwataja majina, kwa sababu bila ya hivyo inaonekana wote tunahusika wakati si jambo la kweli," **Lionel Messi akimshukia Mkurugenzi wa Soka wa Barcelona, Eric Abidal, baada ya kueleza baadhi ya wachezaji walikuwa hawajitumi vya kutosha na kusababisha kutimuliwa kwa Ernesto Valverde.**



"Tunapaswa kuzingatia Ligi Kuu pia, na si mashindano mengine pekee, kama hatuwezi kuendelea tunaweza kutolewa nje ya nne bora, hivyo tunahitaji kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa msimu ujao. Tutazingatia kuhusu makombe na Ligi ya Mabingwa pia, lakini sisi ni wanataaluma, tunahitaji kuonyesha tabia yetu hadi mwishoni mwa msimu na kumaliza ligi katika njia sahihi inayowezekana," **Kiungo wa Manchester City Fernandinho**



"Ametupa kila kitu. Nafikiri alianza katika mechi nane zilizopita mwezi uliopita, na pengine akikimbia kwa asilimia 20 zaidi ya aliyofanya wakati nilipokuja hapa, nina uhakika atafunga tu, kwa sababu ni kawaida kwake kufanya hivyo na nina imani kubwa juu yake," **Kocha wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer akitetea ubutu wa mshambuliaji wake, Anthony Martial.**



## Michezo




# MOLINGA KAMA 'JIWE LILILOKATALIWA NA WAASHI'

**Na Adam Fungamwango**

UNAMKUMBUKA Kocha wa zamani wa Yanga, Mwinyi Zahera? Yeye ndiye aliyemleta David Molinga. Akasema atafunga mabao mengi sana huku mashabiki wa timu hiyo wakimbeza. Awali ilionekana kama kichekesho hivi. Ni kutokana na mchezaji mwenyewe jinsi alivyokuja. Alionekana ni kama meneja fulani hivi na si mcheza soka. Ilionekana kama vile ni mtu aliyeacha kucheza soka zamani.

**Na hata mechi nyingi za mzunguko wa kwanza hakuwa kwenye kiwango chake cha kawaida. Alibezwa si na mashabiki wa timu pinzani tu, bali hata na mashabiki wa Yanga wenyewe.**

Ndiyo maana alikuwa mmoja kati ya wachezaji waliotangazwa kuachwa kwenye kipindi cha dirisha dogo. Lakini ghafla ni kama kuna kitu kiliwashtua viongozi wa Yanga. Wakamrudisha haraka.

Kurudishwa tu, tayari ameanza kuwatendea haki, si waliomrudisha tu, bali wanachama na mashabiki wote wa Yanga waliopiga kelele arudishwe. Ni kama 'jiwe lililokataliwa na waashi kugeuka kuwa jiwe kuu la pembeni'.

Kwa sasa amekuwa ni kama mkombozi wa Yanga, kwani kuna mechi ambazo mabao yake yamekuwa yakiamua mshindi. Jumamosi iliyopita alifunga bao pekee lililoipa ushindi Yanga wa bao 1-0 dhidi ya Ruvu Shooting.

Molinga, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo amefikisha bao la saba kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu na kuanza safari ya kuwafukuza walio juu ya orodha ya wanaowania Kiatu cha Dhahabu.

Februari 2, mwaka huu, alifunga bao pekee kwenye mechi dhidi ya Mtibwa Sugar, Yanga ikiibuka pia na ushindi wa bao 1-0.

Januari 22 mwaka huu, alifunga bao moja kwenye Uwanja wa Liti, akiisaidia timu yake ya Yanga kupata ushindi wa mabao 3-1 ikiwa ugenini dhidi ya Singida United.

Hayo ni mabao aliyoyafunga kwenye kipindi ambacho amerudishwa, siku chache baada ya kutangazwa kutemwa kipindi cha dirisha dogo.

Molinga alianza kufungua akaunti yake ya mabao msimu huu Novemba 22, mwaka jana, alipofunga bao moja kwenye mechi dhidi ya JKT Tanzania, Yanga ikishinda mabao 3-2, na wiki moja baadaye kwenye Uwanja wa CCM Kirumba Yanga ikiichapa Alliance FC, alifunga bao moja, na kufunga mabao mawili kwenye mechi ya Oktoba 3, mwaka jana, Yanga ilipotoka sare ya 3-3 dhidi ya Polisi Tanzania.

Mchezaji huyo mwenye umbile kubwa, kwa sasa ndiye kinara wa ufungaji katika kikosi cha Yanga, na pamoja na usajili wa mastraika wengi kama vile Ditram Nchimbi, Tariq Seif, Yikpe Gnamien na wengine, kipindi hiki cha dirisha dogo, bado wote wameonekana hawajafikia kiwango cha Molinga aliyebezwa.

Kwa mwendo anaouonyesha haitoshangaza kama akitwaa Kiatu cha Dhahabu kwani ni mchezaji anayeonekana kutishia zaidi ufungaji bora wa Meddie Kagere wa Simba mwenye mabao 12, lakini kwa mechi za hivi karibuni amekuwa hana mwendelezo mzuri kama ilivyokuwa zamani.

### NAJUA WAJUA



USHINDI wa mabao 2-0 iliyoupata Tottenham dhidi ya Manchester City, unamfanya kocha Jose Mourinho kushinda mara sita katika mashindano yote dhidi ya timu inayonolewa na Pep Guardiola na ni Jurgen Klopp pekee ambaye amemfunga Mhispania huyo mara nyingi zaidi (mara 8). Hata hivyo, Mourinho sasa ameshinda dhidi ya timu ya Guardiola akiwa na timu nne tofauti (Inter Milan, Real Madrid, Manchester United na Spurs), idadi ambayo ni kubwa zaidi kuliko kocha yeyote.

## SOKA



# WANAOONUKIA KUKOSA EURO 2020 ENGLAND

**LONDON,** England

HUKU michuano ya Euro 2020 ikiwa imebaki miezi kadhaa kuanza, wachezaji wa Uingereza wamekuwa kwenye wakati mgumu wa kujaribu kumshawishi kocha, Gareth Southgate kuwamo kwenye ndege ya kwenda kucheza kwenye mashindano hayo.

**Wachezaji wengi Waingereza wamekuwa kwenye kiwango kizuri msimu huu, huku watano wakiwa katika 10 bora ya wafungaji bora kwenye Ligi Kuu ya England. Si Ligi Kuu ya England pekee ambayo wachezaji Waingereza wameng'ara msimu huu, lakini pia kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, Jadon Sancho amekuwa na wakati mzuri kwa kufunga mabao 29.**

Hata hivyo, kiwango cha wachezaji Waingereza duniani kote kitamweka njia panda Southgate kuchagua kikosi chake cha kucheza kwenye Euro 2020. Makala haya yanakuchambulia wachezaji watano Waingereza ambao wanaweza kukosa kuitwa kucheza kwenye michuano ya Euro 2020.

### 5. CALLUM HUDSON-ODOI

Kwa sasa amekuwa hana namba kwenye kikosi chake na hilo linaweza kumgharimu, Callum Hudson-Odoi kuitwa katika kikosi cha England. Hata hivyo, uzoefu wake wa kucheza mechi nne katika kikosi cha taifa kunaweza kumfanya aitwe na Southgate. Zaidi ukweli ni kwamba England tayari ina wachezaji wa kutosha kwenye nafasi yake kama Jadon Sancho, Marcus Rashford na Raheem Sterling wote wanapigania nafasi ya winga. Kwa kuongezea hili, uwapo wa wachezaji wenye uzoefu kama Danny Ings, kunaweza kumfanya Hudson-Odoi asipate hata nafasi ya kuwa benchi.

### 4. ROSS BARKLEY

Baada ya kupoteza nafasi yake pale Chelsea, Ross Barkley naye hana uhakika wa kuitwa kwenye kikosi cha England kwa ajili ya michuano ya Euro kipindi cha majira ya joto. Kiungo huyo wa Chelsea amezidiwa kiwango na Jack Grealish na James Maddison msimu huu kwa kuonyesha kiwango cha kuvutia pale Aston Villa na Leicester City. Hivyo nafasi yake kwenye kikosi cha Southgate ni ndogo.

### 3. DANNY ROSE

Baada ya kukumbwa na msimu wa majeruhi pale Tottenham Hotspurs, Danny Rose alikamilisha uhamisho wa mkopo kutua kule Newcastle ambako ataangalia namna ya kuimarisha upya kipaji chake. Hata hivyo, licha ya kupata uhakika wa namba chini ya kocha Steve Bruce, Rose pengine anaweza kukosa huruma ya Gareth Southgate kwenye kikosi cha England. Southgate pengine ataamua kumtumia zaidi Ben Chilwell kuliko Rose. Chilwell amekuwa na msimu wa kuvutia kule Leicester City ambao wanapambana kumaliza kwenye nne bora.

### 2. MASON MOUNT

Baada ya kuwa na mwanzo mzuri kwenye Ligi Kuu ya England, wengi waliamini kuwa Mason Mount angeweza kupata namba kwenye kikosi cha England. Hata hivyo, baada ya kuchangia bao moja kwenye mechi zake nane za Ligi Kuu, nafasi ya Mount kwenye kikosi cha England ipo shakani. Jack Grealish na James Maddison wanaonekana kuchukua nafasi ya nyota huyo wa Chelsea.

WAN-BISSAKA

### 1. AARON WAN-BISSAKA

Aaron Wan Bissaka ameshika nafasi ya tatu kwa ukabaji bora katika Ligi Kuu ya England msimu huu.

Licha ya kuwa na msimu wa kuvutia pale Manchester United msimu huu hadi sasa, ushindani wa namba unaweza kumgharimu Wan-Bissaka katika kikosi cha Gareth Southgate kwenye Euro 2020. Kwa kuongezea hilo, atataka kubeba mabeki wanne na hivyo kumuacha Wan-Bissaka kwenye nafasi finyu ya kupata nafasi. Mchezaji huyo wa zamani wa Crystal Palace anagombea namba pamoja na Kyle Walker, Trent Alexander-Arnold na Kieran Trippier kwenye kikosi ambacho kitawajumuisha mabeki wa kulia wawili. Na tatizo ni kwamba, Wan Bissaka anakabiliwa na ushindani dhidi ya Alexander-Arnold na Kyle Walker ambao wana uzoefu mkubwa kwenye michuano mikubwa.

Staili ya Southgate anayochezesha walinzi inamwondoa Bissaka kwenye kikosi hicho. Kwa kumalizia, Southgate atakuwa anaangalia kiwango cha kushinda wakati atakapokuwa akichagua kikosi chake kwa ajili ya Euro 2020.

BAO alilofunga Cristiano Ronaldo Jumamosi iliyopita kwenye mechi ya Serie A dhidi ya Hellas Verona, limemfanya kuweka rekodi mpya Juventus kwa kuwa mchezaji wa kwanza katika klabu hiyo tangu David Trezeguet mwaka 2005, kufunga kwenye mechi tisa mfululizo za ligi hiyo.



NDANI YA 18



LIGI Kuu ya England imekuwa ikipokea wachezaji nyota kutoka sehemu mbalimbali duniani kote.

Uk. 16&17

# 5-BORA YA USAJILI GHALI JANUARI 2020



FERNANDES

**LONDON,** England

WAKATI klabu nyingine Ulaya zikiwa hazina mpango wa kusajili kwenye dirisha dogo la Januari, zikiamini kwamba ni ngumu kupata mchezaji mwenye thamani sawa na kiwango cha fedha kwenye soko la katikati ya msimu, nyingine zinaamini ni wakati mwafaka.

Kama inavyokuwa katika kipindi kingine cha dirisha la usajili, wachezaji wengi wanakuwa wanahusishwa na usajili wa Januari. Baada ya kufungwa kwa pazia la usajili wa kipindi cha majira ya baridi cha Januari, hapa tunaangalia usajili wa wachezaji watano uliokuwa na thamani kubwa zaidi Januari 2020...

**5. STEVEN BERGWIJN (PSV – TOTTENHAM HOTSPURS): PAUNI MIL. 25**

Tottenham Hotspur ilifanikiwa kumsajili winga wa Uholanzi, Steven Bergwijn kwa pauni milioni 25 akitokea Klabu ya Ligi Kuu ya nchini humo, Eredivisie, PSV Eindhoven. Baada ya kutumia misimu tisa akicheza pale PSV, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, akafanikiwa kutua kwenye Ligi Kuu ya England.

Bergwijn pia anaweza kucheza katika nafasi yoyote ya ushambuliaji. Wakati wake akicheza kule Eredivisie, alikuwa anatengeneza pasi kamili kwa wastani wa 2.8 kwa mchezo na pia anaweza kutengeneza nafasi za kufunga kwa wachezaji wenzake. Bergwijn ni mmaliziaji mzuri akitoke sehemu yoyote nje ya bosi la 18.

Katika umri wake wa miaka 22, Bergwijn anaweza kuwa bidhaa muhimu zaidi kwa kikosi cha Mourinho kwa kipindi kirefu.

**4. REINIER JESUS (FLAMENGO - REAL MADRID): PAUNI MIL. 25.6**

Baada ya kuwaongeza Rodrygo na Vinicius miaka michache iliyopita, Real Madrid kwa mara nyingine wametumia pauni milioni 25.6 kwa ajili ya kumsajili kinda wa maajabu wa Brazil, Reinier ambaye anatajwa kama Neymar ajae. Katika umri wake wa miaka 18, winga huyo pia amekuwa akilinganishwa na gwiji wa Brazil, Ricardo Kaka.

Ni wachezaji wachache wanaokuwa na kiwango cha kuvutia katika umri wao kama ilivyo kwa Reinier. Wakati akicheza pale Flamengo, winga huyo alikuwa na kiwango cha kuvutia akiwa na wastani wa kufunga bao katika kila dakika 118 kwenye Ligi Kuu ya Brazil, Serie A, akizidiwa na Gabriel Barbosa (bao moja kila dakika 102).

Msimu uliopita, aliisaidia Flamengo kutwaa taji lake la kwanza la ligi kwa kipindi cha miaka 10. Winga huyo tayari alikuwa mwenye uwezo mkubwa wa kubadili mchezo kwa Flamengo, na sasa anakwenda kuonyesha maajabu yake pale Los Blancos.

**3. GIOVANI LO CELSO (REAL BETIS – TOTTENHAM HOTSPUR): PAUNI MIL. 30**

Baada ya awali kusajili kwa mkopo kutoka Real Betis msimu uliopita, Giovani Lo Celso alionyesha kiwango cha kuvutia kwa miamba hao wa London Kaskazini. Na matokeo yake Spurs wameamua kumnunua mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina kipindi cha majira ya baridi Januari kwa thamani ya pauni milioni 30 pamoja na bonasi.

Lo Celso ana uwezo mkubwa wa kutengeneza nafasi za kufunga na sasa atakuwa mrithi sahihi wa Christian Eriksen ambaye amesajiliwa kwenda Inter Milan ya Italia. Lo Celso alikuwa amepoteza namba kwa raia huyo wa Denmark.

Na sasa ni wazi kwamba Lo Celso anaweza kuwa nyota mkubwa hapo Tottenham kwa miaka michache ijayo.

**2. DEJAN KULUSEVSKI (ATALANTA - JUVENTUS): PAUNI MIL. 30**

Dejan Kulusevski ana nafasi ya kuja kuwa mchezaji mkubwa zaidi kwa siku za usoni na Juventus waliamua kutumia pauni milioni 30 kwa ajili ya kumsajili kiungo huyo kinda wa kimataifa wa Sweden mwanzoni mwa Januari. Ingawa amepelekwa kwa mkopo kule Parma, mchezaji huyo anatarajiwa kujiunga na miamba hao wa Italia kipindi cha majira ya joto kijacho.

Akiwa amekulia kutoka kwenye akademi ya Atalanta, kiungo huyo alionyesha kiwango cha kuvutia.

Kwa mujibu wa makocha waliomnoa, mchezaji huyo ana kila kitu cha kumfanya kuwa bora zaidi kwa siku za usoni.

**1. BRUNO FERNANDES (SPORTING CP - MANCHESTER UNITED): PAUNI MIL. 55**

Ulikuwa ni usajili uliosubiriwa kwa muda mrefu na hatimaye Bruno Fernandes alisajiliwa Manchester United siku ya mwisho kabisa ya kufungwa kwa dirisha la usajili. 'Mashetani Wekundu' walilipa ada ya awali ya pauni milioni 55 pamoja na bonasi inayowezekana kuwa pauni milioni 25 kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno kutoka pale Sporting Lisbon.

Kiungo huyo ana nguvu, kitu ambacho kilikuwa kinakosekana kwenye safu ya kiungo ya United. Kiungo huyo amecheza mechi za kuvutia kwenye Ligi Kuu ya Ureno akifunga mabao na kutoa pasi za mwisho zaidi ya 40 msimu uliopita.

Ingawa inasubiriwa kuona kiwango chake kitakavyokuwa kwenye Ligi Kuu ya England, usajili wa kiungo huyo unaonyesha ishara nzuri zaidi kwa Manchester na anaweza kuja kuwa mmoja wa wachezaji bora kabisa kwenye EPL.

**USILOLIJUA**




TANGU Mohamed Salah alipojiunga na Liverpool Agosti 2017, amefunga mabao 44 katika uwanja wa nyumbani, Anfield sawa na mshambuliaji wa Bayern Munich, Robert Lewandowski na ni tofauti ya mabao saba tu kabla ya kumfikia straika wa Barcelona, Lionel Messi mwenye mabao 51 pale Camp Nou.





Baadhi ya vijana wakifyatua tofali katika Shule ya Sekondari Kiwanja wilayani Chunya kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali katika shule hiyo ukiwamo uzio pamoja na vyoo. **PICHA NA NEBART MSOKWA**

# Wanunuzi dhahabu kwa wachimbaji waonywa

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

SERIKALI wilayani Chunya, Mkoa wa Mbeya, imewatahadharisha wafanyabiashara wa madini wanaonunua dhahabu moja kwa moja kwa wachimbaji wadogo nje ya masoko yaliyofunguliwa na serikali kuacha.

Tahadhari hiyo ilitolewa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Maryprisca Mahundi, wakati wa ziara yake ya kutembelea masoko yaliyofunguliwa kwenye migodi ya wachimbaji wadogo na kusema wamebaini kuwa bado kuna dhahabu inauzwa nje ya masoko hayo.

Aliwataka viongozi wa vijiji kushirikiana na viongozi wa masoko yaliyofunguliwa kudhibiti uuzwaji wa dhahabu kiholela nje ya soko kwa kuwazuia wanunuzi wote wanaofanywa hivyo.

Alisema endapo wafanyabiashara wataachwa waendelee kuuza dhahabu nje ya masoko hayo, kuna uwezekano madini yakaendelea kutoroshwa na hivyo mapato kuporomoka.

“Haya masoko yameanzishwa kisheria na hivyo hakuna anayeruhusiwa kununua dhahabu nje ya soko, atakayekamatwa atashughulikiwa kwa mujibu wa sheria zetu zinazosimamia masoko haya, hivyo nawaomba viongozi wa vijiji na masoko muwe mabalozi wazuri,” alisema Mahundi.

Aliwataka watendaji wote wa halmashauri kuendelea kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo kuhusu taratibu za uuzaji wa madini ili waepuke kulaghaiwa na wafanyabiashara wasiokuwa wazalendo.

Baadhi ya wanunuzi wa dhahabu wanaonunua kwenye masoko maarufu kwa jina la ‘Madeallers’ walikiri masoko hayo kuwa na manufaa kwao na kwa serikali kutokana na mfumo unaotumika kuwa rasmi.

Katibu wa Soko la Dhahabu la Sangambi, Ezekiah Lwosha, alisema matatizo yanayowakabili ni ushindani kati ya wanunuzi rasmi na ambao sio rasmi wajulikanao kwa jina la ‘wamachinga’ ambao wanawavizia wachimbaji. Alisema wanunuzi hao wasio rasmi wanafanikiwa kwa sababu walio rasmi ni wachache na wakati mwingine ni vigumu kwa mchimbaji wa kawaida kuwatofautisha.

“Sisi tunalipa kila tozo zinazohitajika serikalini, sasa hawa wenzetu ambao sio rasmi hawalipi kwa sababu wananunua vichochoroni na ni sehemu ya serikali kupoteza mapato yake, hivyo tunaomba hawa wadhibitiwe,” alisema Lwosha.

Aliwataka wanunuzi wasio rasmi kufuata taratibu za kupata vibali ili na wao wawe rasmi badala ya kuendelea kufanya kazi kinyemela kama ilivyo sasa.

Ofisa Madini wa Wilaya ya Chunya, Godson Kamianda, alisema lengo la serikali kufungua masoko karibu na migodi ya wachimbaji wadogo ni kusogeza huduma kwa wananchi na kuwapunguzia adha ya kusafiri umbali mrefu.

Vilevile alisema utaratibu huo unalenga kuisaidia serikali kupata takwimu sahihi za dhahabu inayozalishwa katika kila eneo ili kurahisisha kukokotoa mapato yatokanayo na rasilimali hizo.

Alisema kutokana na manufaa ya masoko hayo ambayo yanapatikana kwa sasa, wataendelea kuimarisha masoko pamoja na kutoa elimu kwa wachimbaji ili wafuate taratibu za kuuza madini hayo.

# Tofari yabaini ukosefu wa madini kwenye udongo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UTAFITI uliofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Misitu nchini (Tafori), umebaini kuwa baadhi ya maeneo ya mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini udongo wake hauna madini ya Boron hali ambayo inasababisha miti ya kupandwa kushindwa kustawi vizuri.

Akizungumza na waandishi wa habari mkoani Mbeya, Kaimu Mkurugenzi wa Tafori, Dk. Revocatus Mshumbushi, alisema utafiti huo waliufanya kwenye maeneo mbalimbali ikiwamo misitu inayomilikiwa na Wakala wa Huduma za Misitu (TFS), ambako walikuta miti hiyo imedumaa.

Alisema moja ya mashamba yaliyokuwa yanakabiliwa na tatizo hilo ni la Kawetere ambalo linamilikiwa na TFS na kwamba walipelekewa taarifa na meneja wa shamba hilo akiwaomba kufanya utafiti ili kujua tatizo lililopo.

Alisema baada ya kuchunguza na kubaini ukosefu wa madini hayo walishauri yaongezwe kwenye udongo ama kwenye mmea wenyewe na baada ya kutekelezwa kwa ushauri huo yametokea mabadiliko mazuri kwenye miti iliyokuwa imedumaa.

Dk. Mshumbushi alisema madini hayo ni muhimu kwa ukuaji wa miti ya aina yoyote na kwamba yakikosekana wakulima wanaingia hasara kwa sababu miti hiyo haiwezi kukua.

“Madini hayo yanaanza kuongezwa kwenye miti hii ikiwa bado ipo kwenye bustani, yanawekwa kwenye kiriba ili mmea uanze kufyonza ukiwa bado mdogo, lakini kwa ile iliyopo shambani inaongezwa ikiwa hapo hapo shambani,” alisema Dk. Mshumbushi.

Alisema upatikanaji wa madini hayo ni rahisi kwa maelezo kuwa ni aina ya mbolea kwenye maduka ambazo zimeongezwa madini hayo na hivyo wananchi wakiyahitaji wanaweza wakapata kirahisi.

Mhifadhi Mkuu wa shamba la miti la Kawetere, Arnord Shoo, alisema baada ya kupokea ushauri kutoka Tafori wameinusuru miti ya shamba hilo ambayo ilikuwa imedumaa na kwamba kwa sasa inaendelea vizuri. Alisema baadhi ya miti hiyo ilikuwa imeanza kunyauka na kwamba awali wao walikuwa hawajui chanzo cha kukumbwa na tatizo hilo mpaka walipoambiwa na wataalamu kuwa ni kukosa madini hayo mhimu ya boron.

Shoo, alisema walianza kuyatumia madini hayo katika msimu wa mwaka 2016/2017 na mpaka sasa wanaendelea kuyatumia kwenye miti yote ambayo inabainika kuwa na tatizo.

“Tunawashauri wakulima wa miti katika maeneo mengine wanaokabiliwa na tatizo hili la miti yao kudumaa au kunyauka, watembelee ofisi zetu ili tuwashauri kama tulivyoshauriwa sisi,” alisema Shoo.

Hata hivyo, mtafiti wa udongo kutoka katika Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (Sua), Paulo Lyimo, alisema katika baadhi ya maeneo wamebaini kuwa pamoja na kuongezwa madini hayo, kuna tatizo.

Alisema kutokana na tatizo hilo waliamua kuchukua sampuli za udongo kwenye maeneo hayo kwa ajili ya kwenda kuchunguza zaidi ili kubaini chanzo kingine cha tatizo la miti hiyo kutokukua.

# Wananchi waiomba Tarura kukarabati barabara

**Na Nebart Msokwa**, MBEYA

WANANCHI wa Kijiji cha Ipinda kilichopo katika Kata ya Ihango, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameomba serikali kupitiwa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura), kuwaboreshea barabara katika kijiji hicho ili kuwarahisishia huduma za usafiri na usafirishaji.

Wakizungumza wakati wa sherehe waliyoiandaa kwa ajili ya kuishukuru serikali kwa kuwapelekea huduma ya umeme, wananchi hao walisema barabara inayoanzia katika Gereza la Kawetere kwenda katika kijiji hicho ni mbovu na haipitiki mwaka mzima.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Mathias Mayemba, alisema barabara hiyo ambayo inawaunganisha na barabara kuu ya Mbeya- Chunya ni muhimu kwa ajili ya huduma za kijamii, lakini kipindi cha mvua haipitiki.

Mayemba alisema huduma nyingi wanategemea katika Jiji la Mbeya, lakini tatizo ni usafiri kwa maelezo kuwa kutokana na ubovu wa barabara hiyo hata gharama za usafiri ni kubwa.

“Kwa sasa mvua ikinyesha bajaji haiwezi kuingia hapa na ukitaka kutumia pikipiki gharama yake ni kubwa ikilinganishwa na uchumi wetu, sasa tunaomba serikali itusaidie maana kipande hiki hakifiki hata kilomita mbili,” alisema Mayemba.

Alisema serikali imewasaidia kuimarisha sekta ya elimu katika kijiji hicho kwa kuiboresha shule shikizi ya msingi Ipinda pamoja na kuwapelekea umeme na hivyo kilichobaki ni huduma ya barabara.

Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, Fadhill Mwangupili, alisema kijiji hicho hakina zahanati na wajawazito wanapata shida ya kwenda kujifungulia kwenye vijiji jirani.

Alisema kutokana na ubovu wa barabara hiyo wana hofu ya kuwapoteza wagonjwa wao endapo itatokea wakazidiwa usiku, akaomba wasaidiwe kuboreshewa barabara hiyo.

Mwangupili alisema uchumi wa wananchi wa kijiji hicho unategemea kilimo cha viazi mviringo na kwamba kutokana na uchumi huo hawawezi kutengeneza barabara hiyo isipokuwa wanachangia shughuli zingine ndogo.

“Kwa sasa tunapambana kuboresha miundombinu ya shule yetu, tuliletewa fedha na rais kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na sisi tumejichanga kwa ajili ya ujenzi wa matundu ya vyoo,” alisema Mwangupili.

Alisisitiza kuwa endapo wataboreshewa barabara hiyo kuna uwezekano hata soko la viazi wanavyozalisha likaboreka kwa maelezo kuwa kwa sasa bei zinakuwa ndogo kwa sababu wanunuzi wanasingizia ubovu wa barabara.





# Dodoma yabuni namna ya kupaisha ufaulu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma, imeanzisha mpango mkakati wa ufundishaji utakaojumuisha shule za sekondari za serikali na binafsi mwaka huu ili kuboresha na kupandisha ufaulu.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Ofisa Elimu Sekondari wa Jiji hilo, Martin Nkwabi, alipokuwa akitoa tathmini ya ufaulu wa wanafunzi wa kidato cha pili na cha nne kwa mwaka wa masomo wa 2019 kutokana na shule za jiji hilo kutofanya vizuri.

Alifafanua mpango huo ni pamoja na kuhakikisha hakuna kipindi kinachopotea bila walimu kuingia darasani kwa kisingizio chochote na wanafunzi wanawasili shule kwa wakati.

"Kumekuwa na baadhi ya tabia zilizozoeleka, lakini zinatugharimu kila siku, shule nyingi hasa za serikali wanafunzi wanachelewa sana kuwasili shuleni kwa kisingizio cha wiki ya kwanza shule inapofunguliwa hawafundishwi, nimewaagiza wakuu wa shule na maofisa elimu kata kuhakikisha hiyo ratiba inafutwa mara moja na masomo yaanze kufundishwa siku hiyo hiyo shule inapofunguliwa," alisema.

Alisema hivi sasa kuna utaratibu mpya wa ufundishaji katika shule zote, mpango kazi wa masomo yote unafanana kuanzia ratiba za vipindi na nini kinatakiwa kufundishwa ndani ya muda huo.

"Pia mitihani kuanza pamoja ili tuweze kujitathmini na kuona kwa shule ambazo bado zipo nyuma kuzifanyia marekebisho mara moja," alisema.

Aliwataka walimu kuingia kwenye vipindi vyao hata kama kuna mwanafunzi mmoja darasani.

"Nimewapiga marufuku wale wanaotoa sababu za uchache wa wanafunzi kama sababu ya kutokuingia madarasani na badala yake wafundishe hata kama mwanafunzi aliyefika shuleni ni mmoja, tumekuwa tukikwama hapo mara nyingi, lakini ukifuatilia mambo hayo kwa upande wa binafsi hayapo," alisema Nkwabi.

Kadhalika, alisema mkakati mwingine ni pamoja na kutowavumilia walimu wazembe na kwasasa kuna utaratibu maalumu wa kutambua mwalimu yupi hawajibiki ipasavyo kwenye ufundishaji wake.

"Sitovumilia, nitawawajibisha, kila mmoja, mwalimu ambaye atafanya kazi kwenye nafasi yake kwa kuzembea, na ninawahakikishia kutokana na mpango huu tutafika mbali katika uboreshaji wa elimu katika jiji letu la Dodoma," alisema Ofisa Elimu Sekondari.

Pia alisema mpango huo umeanza ili kuongeza ufaulu bila shule yoyote kuachwa nyuma.

Hata hivyo, aliwashukuru wazazi na walezi wa wanafunzi kwa kufanikisha matokeo mazuri yaliyopunguza idadi ya ziro waliruhusu watoto wao kukaa kwenye makambi kwa ajili ya kujisomea.

Alitoa wito kwa wamiliki wa shule binafsi kuhakikisha wanawekeza zaidi katika uboreshaji wa vitendea kazi na ubora wa elimu wanayoitoa ili kupata wanafunzi bora na kuinua kiwango cha ufaulu.

"Wakuu wote wa shule hakikisheni mnasimamia masomo kwa vitendo kwa masomo ya sayansi ili yawe yanafanyika," alisema.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge (kushoto), akisalimiana na mstahiki Meya wa Jiji la Dodoma, Prof. Davis Mwamfupe, walipokutana eneo la Miyuji jijini humo jana, kukagua miradi ya maendeleo. Katikati ni Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kati, Nsolo Mlozi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wanaotupa taka ovyo kupewa kibano

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAFANYABIASHARA wanaotupa taka ovyo nje ya masoko za vifungashio vya nyanya na ndizi wameonywa na atakayebainika kufanya hivyo atapigwa faini kuanzia Sh. 50,000 hadi Sh. 300,000.

Akizungumza mwishoni mwa wiki na waandishi wa habari jijini hapa, Ofisa Masoko wa jiji hilo, James Yuna, alisema kwa mujibu wa sheria ya uingizaji wa taka zinazotokana na vifungashio kwenye masoko, faini yake ni kiasi hicho cha fedha.

"Faini hizi ni zile za vifungashio ambavyo vinatumika kufunga ndizi na nyanya, wafanyabiashara wamekuwa wakitupa taka ovyo nje ya masoko na kusababisha kusambaa, sasa watakaokiuka watalazimika kulipa faini," alisema.

Alisema wafanyabiashara hao wanatakiwa kuondoka na taka hizo na kuzipeleka dampo lililopo Chidaya ambalo limetengwa kwa ajili ya kuhifadhi taka.

"Sisi halmashauri tunahusika na taka ambazo zinazalishwa ndani na wafanyabiashara na wananchi wenyewe ndio tunaziondoa, hivyo kwa wale wanaoleta na vifungashio kutoka nje wanatakiwa kuziondoa wenyewe.

"Lengo la jiji ni kuona mji wake unakuwa safi na haulemewi na wingi wa taka za kutoka nje, hivyo ninawataka wafanyabishara hao kuzingatia sheria na kanuni na wakikiuka watalazimika kulipa faini hiyo," alisema.

Aliwataka wafanyabiashara na wakazi wa jiji kutoa ushirikiano wanapoona taka hizo zikitupwa kwenye maeneo yasiyo rasmi ili wahusika wachukuliwe hatua za kisheria.

Alisema ushirikiano huo utadhibiti uchafu hasa kipindi cha mvua na wanaweza kujiepusha na magonjwa ya mlipuko.

Aliwahimiza kuzingatiaji usafi kwa kufanya biashara kwenye maeneo yaliyosafi.

## Serikali yaendelea kuwasaka wanunuzi wa zao la shayiri

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WIZARA ya Kilimo imesema bado inaendelea kutafuta wanunuzi wa zao la shayiri kwa kuwa waliopo wanahitaji kununua kwa kilo kwa Sh. 550 badala ya Sh. 800 kama ilivyokuwa awali.

Hivi karibuni wakulima wa shayiri mkoani Manyara waliomba serikali kuwatafutia wanunuzi tani 432 za shayiri ambazo zipo kwa muda mrefu tangu kampuni ya TBL ivunje mkataba na wakulima hao.

Akizungumza mwishoni mwa wiki jijini hapa, Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, aliwataka wakulima hao kuvuta subira kwa kuwa wanunuzi waliojitokeza kununua zao bado bei yao ni ndogo.

"Nawaomba wakulima wa zao hili wawe na subira bado serikali inaendelea kutafuta wanunuzi, baada ya kufanya mazungumzo na TBL walisema mkataba waliokuwa na wakulima hao umefikia mwisho hivyo hawawezi kuendelea tena kununua," alisema.

Alisema serikali ilifanya mazungumzo na kampuni ya bia ya Serengeti bila mafanikio na wanaendelea kutafuta wanunuzi ambao watafikia bei ya kuuza yenye faida.

Akizungumza kuhusu usajili wa wakulima wa awamu ya pili kwa kutumia mfumo wa kidijitali, Hasunga alisema utaanza Februari 15 hadi Aprili 14, mwaka huu.

"Usajili wa awamu ya kwanza hadi kufikia Januari 31, mwaka huu tulifanikiwa kusajili wakulima 1,279,884,"alisema.

Kuhusu zao la pamba, Waziri Hasunga alisema katika msimu wa ununuzi 2019/20, jumla ya tani 348,901 zimezalishwa zenye thamani ya Sh. bilioni 419 sawa na ongezeko la asilimia 57 ikilinganishwa na msimu uliopita.



## HABARI ZANZIBAR

# Watoa huduma msaada kisheria wafundwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora Zanzibar, Haroun Ali Suleiman, amewataka watoa huduma wa msaada wa kisheria kufanya kazi kwa uadilifu na kuacha kufikiria maslahi binafsi.

Alisema wananchi wana matumaini makubwa na watoa huduma wa msaada wa kisheria, hivyo wanatakiwa kufanya kazi kwa kuzingatia maadili na uwadilifu wa kazi zao.

Akizungumza juzi katika maadhimisho ya Wiki ya Msaada wa Kisheria yaliofanyika Mjini Zanzibar, Waziri Haroun alisema kwamba jamii inakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zinahitaji kutatuliwa kisheria.

Alisema wasaidizi hao wa sheria wanatakiwa kujikita zaidi katika kutoa msaada wa kisheria na si kufikiria kufanya biashara ya huduma wanazozitoa.

Aidha, alieleza kuwa watoa huduma wa msaada wa kisheria ni wajibu wao kutoa huduma hizo kwa kuzingatia misingi ya utawala bora.

Alisema wananchi wanashindwa kupata haki zao kutokana na kuongezeka kwa rushwa ambayo inachangia kwa kiasi kikubwa kupotea kwa haki za wananchi na watendaji wanaohusika huzifanya kazi zao kibiashara, hali inayodumaza ustawi wa jamiii.

Waziri huyo alieleza kuwa mfumo wa usajli wa watoa huduma za msaada wa kisheria kwa njia ya kielektroniki utaweza kusaidia katika upatikanaji wa taarifa na takwimu kwa usahihi katika matukio ya udhalilishaji na dawa za kulevya na migogoro ya ardhi ambayo yanawasumbua wananchi ambao hawana uwelewa juu ya sheria. Waziri huyo alizitaka Mahakama, Jeshi la Polisi, vituo vinavyotoa huduma za kisheria na Chuo cha Mafunzo (Magereza) kuwa waadilifu katika kazi zao ili kuwapatia haki zao wananchi bila ya muhali na ubaguzi.

Naye Waziri wa Katiba na Sheria, Khamis Juma Mwalim, alisema serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali katika kuhakikisha wananchi wanapata msaada wa kisheria kwa changamoto ambazo zinawakabili.

Alisema moja ya jitihada hizo ni kuanzisha mfumo ambao utawawezesha watoa huduma za msaada wa kisheria Unguja na Pemba kutambulikana na sehemu walipo.

Mkurugenzi wa Idara ya Msaada wa Kisheria Zanzibar, Hanifa Ramadhan Said, alisema kesi za udhalilishaji, jinai, dawa za kulevya hazina msaada wa kisheria, jambo linalopelekea vitendo hivyo kuongezeka, hivyo uwapo wa mfumo wa msaada wa kisheria utaweza kuleta mabadiliko katika upatikanaji wa haki kwa wananchi.

Alisema tokea kuanzishwa kwa idara hiyo tayari mafanikio yameanza kupatikana kutokana na kuwapo kwa ushirikiano mzuri kutoka kwa wadau pamoja na taasisi mbalimbali zinazofanya kazi za kisheria.

Hanifa alisema kazi inayofanywa na wasaidizi wa msaada wa kisheria wa kutoa huduma kwa jamii zinafanywa bila ya malipo, hivyo wananchi watoe mashirikiano ya karibu na wadau wa sheria katika kupata haki zao za msingi.

Mratibu wa Mfuko unaotoa ruzuku kwa watoaji wa msaada wa sheria (LSF), Joseph Magazi, aliyomba serikali kuongeza nguvu za kutoa elimu zaidi kwa wananchi ambao hushindwa kufika kwenye vyombo vya sheria wanapopata matatizo ambayo yanahitaji msaada wa sheria hasa yale ya udhalilishaji kwa watoto.



Mratibu wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania Kanda ya Unguja, Makame Ali Haji, akizungumza wa wananchi wanaofaidika na mpango wa kunusuru kaya maskini Shehia ya Kajengwa Makunduchi Mkoa Kusini Unguja. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wawakilishi waishauri SMZ udhibiti wa dawa za kulevya

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAMATI ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi imeishauri serikali kuhakikisha inaishirikisha taasisi ya kupambana na rushwa na uhujumu uchumi kufuatilia kesi za dawa za kulevya ili kudhibiti uingizaji na utumiaki wake.

Akiwasilisha hotuba ya ripoti ya kamati hiyo, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Mwenyekiti wa kamati, Panya Ali Abdallah, alisema kushirikishwa kwa taasisi hiyo kutasaidia kuondoa changamoto ya baadhi ya kesi zinazofikishwa mahakamani kutopewa uzito unaostahiki. Alisema, baadhi ya watuhumiwa wamekuwa wakipewa dhamana wakati makosa hayo hayana dhamana na kusababisha kutoroka.

Aidha, alisema, ni vyema kuwapo marekebisho ya sheria ya dawa za kulevya ili kuondoa tatizo la kuzorota kwa kesi hizo.

Wakichangia ripoti hiyo, wajumbe wa Baraza la Wawakilishi walisema wanaunga mkono mapendekezo yaliyotolewa na kamati hiyo na kuiomba serikali kuwapo kwa mpango wa serikali kwa ajili ya kutoa ruzuku kwa watu wenye ulemavu ili kuweza kuwasaidia kuendesha shughuli zao.

# ZEC yakumbuka makundi maalum

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TUME ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), imesema imeandaa utaratibu maalum wa kutokupanga foleni kwa watu wenye mahitaji maalum wakiwamo wenye ulemavu, wajawazito na wanaonyonyesha katika zoezi la uandikishaji na uhakiki taarifa za kupiga kura.

Akifungua mafunzo kuhusu elimu ya uandikishaji na uhakiki wa piga kura kwa makundi maalum ya wanawake, vijana na wenye ulemavu Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji mstaafu Hamid Mahmoud, alisema wameamua kuweka utaratibu huo ili kila mwananchi anaitumia haki yake katika kushiriki zoezi hilo.

Alisema kupitia watendaji wa vituo husika watapatiwa miongozo maalum kwa makundi yaliyotajwa na hawataweza kumruhusu asiyehusika kuhudumiwa bila ya kupanga foleni.

Aidha, Mwenyekiti huyo, aliwataka wadau wa uchaguzi kushirikiana na tume katika kuwaelimisha wananchi umuhimu wa kujiandikisha na kuhakiki taarifa zao katika daftari la kudumu la wapigakura.

Alisema hatua hiyo itawawezesha wananchi kushiriki kikamilifu kutumia haki yao ya msingi ya kupiga kura katika uchaguzi mkuu wa mwaka.

Kadhalika, alisema makundi maalum na asasi za kiraia ni wadau wakubwa katika masuala ya demokrasia ambao wanaweza kupeleka mbele maendeleo kwa kasi pale ambapo watasimamia vyema nafasi yao.

Mwenyekiti Hamid aliwahakikishia wananchi kuwa tume haitamwacha mtu yeyote ambaye atakuwa na sifa ya kujiandikisha katika daftari hilo la kudumu la wapigakura.

Akiwasilisha mada ya dhana ya wadau wa uchaguzi, Ofisa Elimu ya Wapigakura Habari na Mawasiliano, Juma Sanif Sheha, alisema ushirikishwaji wa wadau huleta ufanisi katika masuala ya uchaguzi ikiwamo kupima kiwango cha utawala bora na uwazi katika nchi.

Alisema ushirikishwaji wa wadau wa uchaguzi katika mchakato wa uchaguzi ni moja ya njia za kuudhihirisha umma sifa moja ya tume huru za uchaguzi na kiashiria cha kuwa na chaguzi huru za haki na kuaminika.

Washiriki waliipongeza tume kwa kujenga utamaduni huo na kushauri wakati utakapofika kuimarisha vituo vya kuandikisha kwa kuweka mazingira rafiki hasa kwa watu wenye ulemavu.

Pia waliitaka tume hiyo kuandikisha wananchi ambao hadi sasa hawajapatiwa vitambulisho vya Mzanzibari kwa kutumia namba za risiti walizopewa na wakala wa matukio ya kijamii ili nao kutumia fursa hiyo.

# Mvua yakwamisha miradi 36 barabara

**Na Julieth Mkireri,** KISARAWE

KAIMU Meneja wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) Wilaya ya Kisarawe, Godfrey Mbena, amesema, miradi 36 ilivyopangwa kutekeleza kuanzia Oktoba mwaka 2019 imesimama kutokana na mvua zinazoendelea.

Mbena amebainisha hayo mwishoni mwa wiki wilayani Kisarawe, alipokuwa anaelezea kuhusiana na hali ya barabara kwa sasa pamoja na mikataba ambayo imeshasainiwa na makandarasi.

Mbena alisema, wananchi hawakupaswa kupata shida wanazopata kwa sasa kutokana na ubovu wa barabara na kwamba hali hiyo imesababishwa na mvua ambazo zinazuia matengenezo kuendelea.

Akiwa katika barabara ya Homboza Masaki ambayo ina ukubwa wa kilomita 18.5, alisema, barabara hiyo ilitengewa kiasi cha Sh. milioni 53, lakini hadi sasa ukarabati wake haujafanyika kutokana na mvua.

Aidha, alisema, kutokana na hali ilivyo katika barabara hiyo na uharibifu uliochangiwa na magari ya mchanga, wamelazimika kuongeza bajeti kwani iliyotengwa haiwezi kukidhi hali iliyopo.

"Wananchi hawakupaswa kupata shida wanayokumbana nayo kwa sasa, lakini kazi zinashindwa kufanyika kutokana na mvua, na malori yamechangia uharibifu wa barabara hii na hivyo daladala kushindwa kupita katika kipindi hili, alisema.

Kaimu meneja huyo alisema, malori ya mchanga yamesimama kupita katika njia hiyo na pindi itakaporekebishwa wanarudi na kupitisha mizigo ambayo ni mikubwa ukilinganisha na uwezo wa barabara hiyo.

Alisema pamoja na changamoto zinazowakabili wananchi katika kipindi hiki, wanatakiwa kuvumilia na pindi mvua zitakapokata utekelezaji wa miradi yote utaanza. Baadhi ya watumiaji wa barabara ya Homboza-Masaki waliomba serikali kuzuia magari ya mchanga kutumia njia hiyo, kwani ndio yanayochangia uharibifu.

Hamisi Juma, alisema, malori yanatakiwa kusimamishwa na kuelekezwa eneo mbadala ya kufuata madini ya mchanga kwani yanasababisha kero kwa watumiaji wa barabara hiyo.

Mwanahamis Mengo, alisema, wanalazimika kutumia kiasi cha Sh. 7,000 kwa nauli ya pikipiki kwa siku ukilinganisha na daladala ambayo wanalipa Sh. 2,500 kutoka Chanika hadi Msimbu.

Naye Anna Nduguru, alisema, adha wanayokumbana nayo wakazi wa Msimbu ni kubwa kwani wapo kinamama wanajifungulia barabarani wakiwahishwa hospitali kutokana na hali ya barabara hiyo.




Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Sophia Mjema, akizungumza wakati wa ushiriki wa kifungua kinywa cha pamoja na wafanyakazi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na Benki ya NMB jijini Dar es Salaam. Wa pili kutoka kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa ya Ilala, Jumanne Shauri, Meneja wa Kanda ya Dar es Salaam, Badru Iddi, Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Serikali NMB, Vicky Bishubo na Katibu Tawala wa Manispaa ya Ilala, Charagwa Selemani. **MPIGAPICHA WETU**

# Zungu apigia debe fursa bomba mafuta

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limekabidhi cheti cha Tathmini ya Athari kwa Mazingira kwa Kampuni ya Total inayosimamia mradi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika

Mashariki (EACOP) kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mradi huo nchini.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu, amewataka Watanzania kuchangamkia fursa za bomba hilo.

Akizungumza kwenye hafla fupi ya makabidhiano ya cheti hicho jijini Dodoma mwishoni mwa wiki,

Waziri Zungu aliwahimiza Watanzania kutumia fursa za kiuchumi zinazojitokeza wakati wa utekelezaji wa mradi, lakini pia aliwataka walilinde bomba hilo, lisihujumiwe.

Makabadhiano hayo yalifanyika kati ya Mkurugenzi wa NEMC, Dk .Samuel Gwamaka na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Total, Martin Tiffen na viongozi mbalimbali wa serikali waliudhuria hafla hiyo.

"Matumaini yetu ni kuwa mradi utakwenda kutekelezwa pasipo kuleta athari katika mazingira na utakwenda kuchochea uchumi katika maeneo yote ambapo bomba litapita, hivyo wananchi wajitokeze kuchangamkia fursa hii," alisema Waziri Zungu.

Alisema katika mradi huu zipo fursa nyingi ambazo wananchi wakizitumia wanaweza kunufaika ikiwamo nyumba za wageni, chakula na dawa ni vitu

muhimu ambavyo kama wananchi watawekeza kwenye maeneo hayo watajipatia fedha na kupata maendeleo zaidi.

"Mradi huu unataraji kuajiri zaidi ya watu 1,000 wa moja kwa moja na ajira 20,000 ambazo sio za moja kwa moja ni fursa kwa Mtanzania katika kufanya biashara na watu hao walioajiriwa kujiingizia kipato," alisema.

Waziri Zungu alieleza eneo la mradi litakuwa Tanzania na kufanya zaidi ya mikoa nane, wilaya zaidi ya 20 na vijiji zaidi ya 100 kupitiwa na mradi huo, jambo ambalo ni fursa kibiashara na kuchochea maendeleo.

"Nampongeza Rais John Magufuli kwa kukubali mradi na kuonyesha mfano wa ushirikiano kati ya nchi yetu na Uganda, na kwa upande mwingine ni mfano mzuri wa ushirikiano kati ya sekta binafsi na sekta za umma katika nchi hizi," alisema Waziri Zungu.

"Cheti cha EIA kinatupa mwanga kuwa mradi utakwenda kutekelezeka kwa kuzingatia utunzaji wa mazingira, na tunaamini mkandarasi amejipanga kuhakikisha mradi unakamilika kwa kuyaacha mazingira salama," alisema

Waziri Zungu. Kwa upande wake, Waziri wa Nishati Dk. Medard Kalemani, alisema kufikiwa kwa hatua hiyo kutawezesha sasa zoezi la ulipaji fidia liweze kufanyika ambapo tayari tathmini ilishafanyika.

"Kilichobaki ni mkandarasi kuanza kazi na pia kulipa fidia kwa wananchi wenye maeneo ambayo mradi utapita kutokea Tanga mpaka Uganda," alisema Kalemani na kuongezea kuwa mradi huu utakuwa chachu ya kukua kwa uchumi kwa nchi hizi mbili.

Akitoa shukrani baada ya kupokea cheti hicho cha EIA, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Total, Martin Tiffen, ambaye ndio watekelezaji wa mradi huo, aliishukuru serikali kwa kuiamini kampuni hiyo kuipa mradi na kuahidi kwenda kutekeleza mradi, huku akikumbusha faida za kiuchumi watakazopata wananchi wanaopitiwa na mradi huo.

# 'Mazingira zuizi kikwazo uwekezaji'

**Na Lucy Ogutu,** MTWARA

MKUU wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, amesema ni vigumu kukuza uwekezaji kwa mazingira zuizi hasa ya bidhaa zinazozalishwa na wazawa zikiwamo pombe za kienyeji ambazo baadhi zimeonekana kuwa ni halifu, hivyo kutoa fursa ya uingizaji vileo kutoka nje ya nchi.

Byakanwa amesema kwa maoni yake ni vema yakawekwa mazingira wezeshi na wataalamu kuwa sehemu ya kuboresha bidhaa hizo itasaidia kukuza viwanda vya ndani.

Alitoa kauli hiyo katika maadhimisho ya Siku ya Sheria ambapo maudhui ya siku hiyo mwaka huu ilikuwa ni uwekezaji wa biashara wajibu wa mahakama na wadau kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji nchini.

Alisema katika kukuza biashara kunahitaji mapinduzi ya kifikra na utendaji wa makusudi, vinginevyo hatuwezi kufika tunapotaka iwapo ubunifu wa watazania katika utengenezaji wa bidhaa utaendelea kuonekana haufai, hivyo kuendelea kuua viwanda vya ndani.

Lakini amesema kuendelea kuingiza bidhaa toka nje ya nchi vikiwamo vileo na kutovipa kipaumbele vile vinavyozalishwa na wazawa, kuna hatari ya kushindwa kufikia malengo ya kuwa na uchumi wa kati ifikapo kwa 2022.

Akitoa maoni yake kwa Jeshi la Polisi amesema ifike wakati RPC mnapokamata pombe za kienyeji hakuna haja ya kuwazuia wasiendelee kuuza, bali kuzifikisha kwenye mamlaka husika ili ziweze kupimwa kiwango cha ubora na kusimamiwa katika uzalishaji wa bidhaa hiyo na kusisitiza viwanda vingi vya konyagi vimekufa kutokana na kukosekana kwa usimamizi mzuri wa kisheria.

Alisema sheria zenye ukakasi hazinabudi kuboreshwa ili ziwe sehemu ya kuhamasisha Watanzania kujiajiri kwa wingi katika ubunifu wa kuzalisha bidhaa mbalimbali badala ya kuwa sehemu ya kukatisha tamaa.

## HABARI KIMATAIFA

# Idadi waliofariki na corona yafikia 800

**BEIJING,** China

IDADI ya watu waliokufa kutokana na maambukizi ya virusi vya corona nchini China imeongezeka kwa vifo 89 na kufikia watu 811.

Idadi hiyo ya watu waliokufa kutokana na maambukizi ya virusi hivyo sasa imezidi idadi ya waliokufa kutokana na ugonjwa wa homa ya Sars mnamo mwaka 2002 na 2003 nchini China na kwamba watu 800 walikufa duniani kote.

Shirika la Afya Duniani (WHO) limesema hadi sasa kuna maambukizi 34,800 duniani kote. China ndio iliyoathirika zaidi mpaka sasa imethibitishwa kwamba watu 27,000 wameambukizwa.

Juzi, Ubalozi wa Marekani ulitoa taarifa kuhusu raia wake mwenye umri wa miaka 60 aliyefariki baada ya kuambukizwa virusi vya corona.

**Hospitali ya dharura ya pili imekamilika na imefunguliwa katika Jiji la Wuhan, linalokabiliana na mlipuko wa virusi vya corona.**

Waliokufa wengi wanatoka katika mkoa wa kati wa Hubei, ambako virusi vya corona viligunduliwa kwa mara ya kwanza. Raia watano wa Uingereza akiwamo mtoto wamegundulika kuwa na virusi hivyo nchini Ufaransa.

Waziri wa Afya wa Ufaransa, Agnes Buzyn alisema waliambukizwa na raia mwingine wa Uingereza ambaye katika siku za hivi karibuni alikuwa nchini Singapore.

Hospitali ya dharura ya pili imekamilika na imefunguliwa katika Jiji la Wuhan, linalokabiliana na mlipuko wa virusi vya corona.

Hospitali hiyo iitwayo Leishenshan ina wodi za kulaza wagonjwa 32 na vitanda 1,500 pamoja na chumba kimoja cha upasuaji. Kikosi cha kwanza cha madaktari kilifika siku ya Jumamosi asubuhi.

Jiji la Wuhan linabadilika kwa haraka wakati ambapo majengo kadhaa yanageuzwa kuwa hospitali ili kukabiliana na idadi kubwa ya watu walioambukizwa virusi vya corona.

Hospitali nyingine iliyojengwa kwa muda mfupi yenye vitanda 1,000 ilifunguliwa Jumatatu na ujenzi wake ulichukua siku 10.

Kufikia Jumamosi, mkoa wa kati wa Hubei pekee uliorodhesha idadi ya watu 27,100 waliokuwa wameambukizwa virusi vya corona, watu 780 wameshafariki dunia kwenye mkoa huo.

Wakati huohuo, Rais wa China, Xi Jinping amesema nchi yake inamatumani ya kuushinda ugonjwa huo ambao kwa sasa umeleta hofu duniani.

Katika mazungumzo kwa njia ya simu, Xi Jinping alimwakikishia mwenzake wa Marekani, Donald Trump kwamba nchi yake itatokomeza ugonjwa huo na kueleza kuwa China ina imani kuhusu uwezo wake wa kuliangamiza janga hilo.

Kutokana na kauli hiyo, Rais Trump aliipongeza China kwa kufanya juhudi za kukabiliana na ugonjwa huo hasa kwa kuchukua hatua madhubuti za kuangamiza. **DW**



Wahudumu wa afya nchini China wakiwa katika harakati za kuwahudumia waathirika wa ugonjwa wa corona. **PICHA: ALLIANCE**

## Aua raia 20 kwa risasi

**BANGKOK,** Thailand

JESHI la Polisi Thailand limesema takribani watu 20 wamefariki baada ya kupigwa risasi kiholela na mwanajeshi katika mji wa Nakhon Ratchasima.

Msemaji wa Wizara ya Ulinzi alisema kwamba Jakraphanath Thomma, ofisa wa madaraka ya chini alimshambulia mkuu wake kabla ya kuiba bunduki na risasi kutoka katika kambi ya kijeshi.

Inaelezwa kuwa baadaye aliwafyatulia risasi waumini waliokuwa katika hekalu na duka la jumla katika mji huo.

Picha zilizochapishwa katika mitandao ya kijamii zimekuwa zikionyesha eneo ambalo ufyatuaji huo wa risasi ulifanyika karibu na duka la jumla.

Picha za vyombo vya habari zinaonekana zikionyesha mshukiwa huyo akitoka katika gari moja katika eneo moja la duka hilo la jumla katika Wilaya ya Muang na kuwafyatulia watu risasi kiholela.

Picha nyingine zilionyesha moto nje ya jengo hilo huku kukiwa na ripoti kwamba ulisababishwa na gesi iliolipuka baada ya kupigwa risasi.

"Mwanajeshi huyo alitumia bunduki ya rashasha kuwapiga risasi watu wasio na hatia na kuwajeruhi wengi huku wengine wakifariki," alisema Krissana Pattanacharoen ambaye ni msemaji wa serikali.

Msemaji wa Idara ya Ulinzi, Luteni Jenerali Kongcheep Tantravanich alisema kwamba watu 20 waliuawa katika tukio hilo kabla ya kufikishwa hospitali.

Moja ya machapisho yake ya mitandao yanaonyesha picha ya selfie yake huku moto ukiwaka nyuma yake.

Mamlaka nchini Thailand imekizunguka kituo hicho huku ikijaribu kumtafuta mshukiwa ambaye anasemekana kuwa bado alikuwamo ndani ya jumba hilo. **BBC**

## Rais Trump awafuta kazi watumishi waliomchongea

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Donald Trump (pichani) amewafuta kazi maofisa wawili waandamizi waliotoa ushahidi dhidi yake katika kesi ya kutokuwa na imani naye iliyokuwa inamkabili.

Balozi wa Marekani kwa Muungano wa Ulaya, Gordon Sondland, alisema: "Nimeambiwa kwamba Rais anataka nirudi nyumbani mara moja."



Awali, Luteni Kanali Alexander Vindman, mtaalamu mkuu katika masuala ya Ukraine, alisindikizwa kutoka nje ya Ikulu ya Marekani.

Taarifa kutoka Ikulu ya Marekani inaeleza kuwa Rais Trump anataka kufanya mabadiliko baada ya Bunge la Seneti kumwondolea mashtaka yaliyokuwa yanamkabili wiki iliyopita.

Katika kura ya kihistoria iliyopigwa, Bunge la Seneti liliamua kutomwondoa rais huyo wa 45 wa Marekani madarakani kwa madai yaliyokuwa yameibuliwa dhidi yake kutokana na mahusiano yake na Ukraine.

Kaka yake Luteni kanali Vindman ambaye ni pacha mwenzake, Yevgeny Vindman, wakili mwandamizi katika Baraza la Usalama la Taifa pia alirejeshwa katika idara ya jeshi Ijumaa.

Katika taarifa iliyotolewa na wakili wake, Sondland alisema: "Nimearifiwa hii leo kwamba Rais anataka nirudi nyumbani mara moja baada ya kunivua wadhifa wa balozi wa Marekani kwa Muungano wa Ulaya.

"Nashukuru kwa fursa ambayo Rais Trump alinipa ya kuhudumia taifa, pia namshukuru Waziri wa Mambo ya nje, Mike Pompeo kwa kuniunga mkono, na tena shukrani zangu ziwaendee wafanyakazi wote wa ubalozini wa Muungano wa Ulaya kwa utalaamu wao na kujitolea kwao" alisema Sondland na kuongeza:

"Najivunia kile ambacho tumefikia. Kazi yetu hapa ilikuwa kielelezo chema kwa taaluma yangu," alisema Sondland.

Mshauri wa Luteni kanali Vindman, David Pressman, alisema kwamba mteja wake ametolewa nje ya Ikulu ambako amekuwa akifanya kazi yake kwa uadilifu kwa nchi yake na kwa rais wake. **BBC**

# Nyanya, vitunguu havishikiki

INATOKA UK. 8

Katika soko la Boko nyanya moja inauzwa kati ya Sh. 400 hadi Sh. 500 na sado Sh. 14,000 huku vitunguu vikuzwa Sh. 9,000 hadi Sh. 14,000 kwa sado.

Katika Soko la Kariakoo, gunia la vitunguu linauzwa kati ya Sh. 450,000 hadi 500,000, sanduku la nyanya kati ya Sh. 100,000 hadi Sh. 150,000.

Kilo moja inauzwa kati ya Sh. 6,000 hadi Sh. 7,000 na sado Sh. 15,000 huku vitunguu kilo ni Sh. 6,000 na sado Sh. 16,000.

Kwenye mitaa mbalimbali ya jijini nyanya zinauzwa kati ya Sh. 500 na Sh. 600 kutegemea na ukubwa huku vitunguu vikinunuliwa kwa kati ya Sh. 300 hadi 400, kimoja. Katika maeneo ya Kimara nyanya moja inauzwa kati ya Sh. 600 hadi Sh. 700, sado moja kati ya Sh. 13,000 hadi Sh. 15,000.

Tenga linauzwa kati ya Sh. 100,000 hadi 120,000. Nipashe pia imebaini kuwa wauzaji wa magenge wengi hawauzi bidhaa hizo kwa kuhofia kupata hasara.

"Mimi sina nyanya kwa sababu ukizinunua kazi unayo unawaza kukuta nusu sado tena ni mbovu kwa hiyo unapata hasara zaidi kwa sababu hakuna mteja atakayekubali kununua nyanya mbovu kwa Sh. 600," alisema John Masawe, mfanyabiashara wa genge eneo la Kimara Baruti.

Alisema biashara ya nyanya zilizosindikwa na kuhifadhiwa kwenye vifungashio, zinanunuliwa kwa wingi katika maeneo hayo na wauzaji wa maduka wanauza moja kwa Sh. 500.

"Kwa sasa biashara ya nyanya za pakiti ndiyo zinatoka na kwa siku nauza hadi pakiti 30," alisema muuza duka maeneo ya Kimara Baruti.

Kadhalika wauzaji wengine walioongea na Nipashe walisema bidhaa hizo zimepanda bei kutokana na mvua inayoendelea kunyesha, kuharibu miundombinu na wakulima kushindwa kuyafikia masoko.

### MOROGORO

Mkoani Morogoro soko la Mawenzi, kilo ya vitunguu inanunuliwa kwa Sh. 3,500, vitunguu swaumu Sh. 7,000, na nyanya Sh. 10,000 hadi 12,000.

### KAHAMA

Wafanyabiashara na walaji wamesema awali vitunguu viliuzwa Sh. 100,000 hadi 130,000, lakini kwa sasa ni kati ya Sh. 200,000 hadi 230,000.

Mfanyabiashara Josephina Clistiani alisema kabla ya mvua kuanza walinunua ndoo moja ya nyanya kwa Sh. 10,000, na kuwauzia wateja nyanya moja 100, lakini kwa sasa ni Sh. 28,000 na kuuza nyanya tatu Sh. 500.

Naye, Rehema Jafari alisema walikuwa wakinunua sado ya nyanya kwa Sh. 2,000 na kuuza kwa Sh. 3,000, lakini kwa sasa



Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga

wananunua kwa Sh. 5,000 na kuwauzia wateja kwa Sh. 8,000 hadi Sh. 9,000.

"Tulikuwa tunanunua ndoo ya nyanya kwa Sh. 10,000 na vitunguu kwa Sh. 100,000, na sasa baadhi yetu wameshindwa kufanyabiashara baada ya mitaji yao kukatika na kushindwa kuhimili wingi wa bei za vitunguu kutoka Sh. 100,000 hadi Sh. 230,000 kwa gunia," alisema Jafari.

### SHINYANGA

Mfanyabiashara Georgina Gabriel wa Soko Kuu la Shinyanga Mjini, alisema bei ya nyanya kwa sasa fungu moja ni Sh. 500, na awali walikuwa wanauza Sh. 300, sado wanauza Sh. 7,000 awali waliuza Sh. 5,000.

Alisema wamepandisha bei hiyo kutokana na wao kununua nyanya kwa bei kubwa. Ndoo moja wananunua Sh. 22,000 hadi Sh. 25,000, awali walinunua kwa Sh. 15,000, na hivyo kuamua kupandisha bei ya nyanya kutokana na soko la nje kupanda.

"Bei ya nyanya imepanda kutokana na kuadimika kwenye soko la nje, mvua imeharibu mashamba ya nyanya pamoja na wafanyabiashara kutoka Morogoro kufuata nyanya mkoani Shinyanga, na kusababisha bei ya kununua kuwa juu Sh. 22,000 hadi 25,000 kwa ndoo, zamani tulinunua kwa 15,000," alisema Gabriel.

Alisema licha ya bei ya nyanya kupanda, vitunguu navyo havishikiki, wanauza kilo moja Sh. 3,000, awali waliuza kwa Sh. 1,500.

### ARUSHA

Neema Nkya ni mfanyabiashara wa soko la Kilombero, alisema kwa sasa bei za bidhaa zimepanda kwa kiasi kikubwa gunia la karoti kwa sasa ni Sh. 100,000, huku vitunguu sado vikiwa vimefika Sh. 15,000, na nyanya Sh. 10,000.

Manka Shayo alisema kuwa mvua ndiyo imesababisha vitu kuharibika kwa kuwa mazao mengi yalikuwa shambani na kuzidiwa na maji.

"Pengine miundombinu ndiyo chanzo maana barabara nyingi zimeharibika nyingine kukatika hivyo inasababisha bidhaa kuchewa kufika sokoni hali inayosababisha kupanda kwa bei, pia alibainisha kuwa vipo vitu vingi vinavyosababisha bei kupanda mfano mazao kushambuliwa na wadudu mashambani na vingine vingi," alisema Anna Godwin.

Naye, Noel Martin alisema kuwa kitu kingine kikubwa kinachochangia kupanda kwa bei ya bidhaa ni pamoja shilingi kuporomoka.

### MBEYA

Mkoa wa Mbeya nyanya zimepanda kna kuwa kati ya Sh. 70,000 na 80,000 kwa tenga moja mwezi Desemba mwaka jana mpaka kufikia kati ya Sh. 130,000 na Sh. 150,000 mwezi huu.

Baadhi ya wakulima wa zao hilo kwenye Bonde la Utengule katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, ambalo ni miongoni mwa mabonde maarufu kwa uzalishaji wamefurahia bei hizo wakidai kuwa zinaendana na gharama za uzalishaji.

Mmoja wa wakulima hao, Fabian Mhaluke, alisema bei ya zao hilo imepanda kwa sababu ya mvua inayoendelea kunyesha imesababisha kuungua kwa nyanya zilizokuwa zimepandwa kuanzia mwezi Desemba.

Katika soko la wakulima la Tarafani katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi, zinauzwa Sh. 500 kwa fungu la nyanya nne mpaka Sh.1,000 kulingana na ubora.

Mmoja wa wafanyabiashara wadogo katika soko hilo, Esther Malema, alisema bidhaa hizo hazipatikani kwa urahisi na hivyo watu wengi wameanza kununua zaidi karoti. Alisema awali walikuwa wanauza nyanya kuanzia sh. 200 kwa fungu mpaka 400 kulingana na ukubwa na ubora wake.

### KATAVI

Manispaa ya Katavi tenga moja la nyanya kwa sasa ni Sh. 45,000 hadi Sh. 60,000 kutoka Sh. 15,000 hadi Sh. 20,000, vitunguu sado moja Sh. 10,000 na kimoja ni Sh. 100 hadi 200 na nyanya moja ni Sh. 150 hadi 200 huku fungu lenye nyanya nne ni Sh. 500 hadi 1,000.

Said Ally ni mkulima wa zao hilo lakini pia ni mfanyabiashara alisema kuongezeka kwa bei hiyo kunasababishwa na mvua zinazoendelea kunyesha nakupekea zao hilo kuharibika likiwa shambani.

### MWANZA

Jijini Mwanza sado moja ya nyanya na vitunguu inauzwa kati ya Sh. 8,000 na 10,000, na kwa kilo ni Sh. 2,500 na moja moja ni Sh.200 hadi 300.

### DODOMA

Wastani wa Sh.5000 hadi Sh.12,000 kwa sado moja.

Nipashe ilitembelea Soko Kuu la Majengo na Kikuyu, wafanyabiashara hao walisema hali hiyo inatokana na upatikanaji wake kuwa wa shida.

Mfanyabiashara wa soko la Majengo, Isaya Charles, alisema bei ya nyanya ni Sh.10,000 kwa sado na vitunguu ni Sh. 12,000.

Naye, Mfanyabiashara wa soko la Kikuyu, Eunice Mahope, alisema kupanda kwa bei kunatokana na mvua kusababisha nyanya kuozea shambani na uzalishaji mdogo.

### ZANZIBAR

Bei ya nyanya, vitunguu maji, swaumu na tangawizi zimependa mara dufu visiwani Zanzibar kutokana na kuadimika Tanzania Bara.

Wakizungumza na Nipashe wafanyabiashara wa Soko Kuu la Mwanakwerekwe, Ame Mshindani, alisema kilo moja ya nyanya inauzwa Sh 4000 wakati wiki tatu zilizopita ilikuwa ni Sh. 1500 huku tenga la nyanya likiuzwa Sh. 130,000 kutoka Sh. 70,000.

Bei ya kitunguu kwa sasa kilo ni Sh. 5,000 wakati ilikuwa 3,000 na kitunguu swaumu ni Sh. 8,000 badala ya Sh. 5,000 ya awali.

Bei ya tangawizi kilo moja ni Sh. 4,000 badala ya 2,000.

Mfanyabiashara huyo alisema kuwa Zanzibar inategemea bidhaa hizo kutoka Tanzania bara licha ya wakulima wa Zanzibar kulima nyanya lakini si kwa kiwango kikubwa.

### MOSHI

Mjini Moshi sadolini moja ya nyanya inauzwa kwa Sh. 19,500 na sanduku moja likiuzwa hadi Sh. 80,000.

Katika solo la Mbuyuni, Manispaa ya Moshi, bei ya nyanya kwa Sadolini moja ni kati ya Sh.19,500 wakati Soko la kwa Sadala lililopo Wilaya ya Hai, nyanya sadolini moja inauzwa kwa Sh. 12,000 hadi 12,500.

Soko la Sanya Juu lililopo Wilaya ya Siha, bei ya nyanya kwa sadolini moja ni Sh.8,000 wakati kitunguu sadolini moja ni Sh.6,000.

### MTAALAMU WA KILIMO

Mwishoni mwa wiki katika ukurasa wake wa Facebook, Malembo Lucas wa kampuni ya Malembo the Farm, aliandika "Nimetembelea soko la mboga na matunda Mabibo jijini Dar es Salaam, bei ya sanduku la nyanya ni Sh. 9,000 hadi 11,000, kilimo Sayansi, kilimo ni malengo, kilimo ni soko na kilimo ni majira," alisema na kuongeza:

"Waliolima nyanya miezi mitatu iliyopita ndiyo wanakutana na soko la bei hii, usihamasike na bei ya leo, kesho ukaenda shamba kulima nyanya tafuta taarifa na maarifa ya kilimo unachotaka kufanya."

***Taarifa hii imeandaliwa na Salome Kitomari, Romana Malya, Batrice Shayo, Mary Geofrey na Somoe Ng'itu (DAR), Shaban Njia (KAHAMA), Marco Maduhu (SHINYANGA), Woinde Shizza na Allan Isack (ARUSHA), Idda Mushi (MOROGORO), Nebart Msokwa (MBEYA), Godfrey Mushi (MOSHI), Happy Severine (SIMIYU), Neema Hussein (KATAVI), Neema Emmanuel (MWANZA), Renatha Msungu (DODOMA) na Rahma Suleiman (ZANZIBAR).***

# Mradi umwagiliaji kunufaisha wakulima

**Na Mwandishi Wetu,** RUANGWA

MAMIA ya wakulima wilayani Ruangwa Mkoa wa Lindi, watanufaika na mradi wa umwagiliaji wa Nanganga wenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 400 unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) chini ya Mradi wa Small Scale Irrigation Development Project (SSIDP).

Mradi huo ambao ulikabidhiwa mwishoni mwa wiki na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji (NIRC) kwa umoja wa umwagiliaji Nanganga (UMWANA) wenye jumla ya wanachama 120.

Mradi wa umwagiliaji Nanganga ni kati ya miradi 16 ya mradi wa SSIDP III awamu ya tatu inayotekelezwa na serikali.

Mradi huu unatekelezwa kupitia Wizara ya Kilimo na kusimamiwa na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji (NIRC) kwa kushirikiana na Halmashauri ya Ruangwa kwa fedha ya mkopo kutoka Serikali ya Japan kupitia Shirika lake la JICA wenye thamani ya Sh. 1,106,619,386.02.

Akizungumza wakati wa makabidhiano wa mradi huo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Ruangwa, Andrea Chezue, aliishukuru serikali kwa kujenga miundombinu ya umwagiliaji ya kisasa wilayani humo.

Chezue alisema kilimo cha umwagiliaji kimeleta tija kubwa wilayani humo hususan kwa vijana ambao kwa sasa wengi wao wanajishughulisha na kilimo cha mbogamboga na hivyo kuboresha maisha yao.

Meneja wa mradi huo, Mhandisi Paul Mabaya, alisema ujenzi wa mradi huu unahusisha ujenzi wa banio katika Mto Lukuredi, mfereji mkuu wenye urefu upatao mita 525, mfereji wa kati wenye urefu upatao mita 2675, mifereji midogo na vigawa maji pamoja na vivuko vya miguu na matrekta.

"Mradi wa umwagiliaji Nanganga umetekelezwa chini ya mikataba miwili na makandarasi wawili waliingia mikataba ya kujenga mradi huu. Mkataba wa kwanza unaohusisha ujenzi wa banio, mfereji mkuu na vigawa maji na vivuko vya miguu umetekelezwa na kampuni ya Haricom International Ltd ya Dar es Salaam na mkataba wa pili unaohusisha ujenzi wa mfereji wa kati na mifereji midogo umetekelezwa na kampuni ya D&L (T) Ltd ya Dar es Salaam," alisema Mabaya.

Kwa mujibu wa meneja mradi, ujenzi wa mradi katika mkataba wa kwanza una thamani ya Sh. 702,958,355.60 na ujenzi wake ulikuwa ni miezi minane (8) kuanzia Novemba 5, 2018 mpaka Julai 2, 2019.

## Akabidhiwa kitita cha mil. 10/-

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CBA kwa kushirikiana na Kampuni ya simu ya Vodacom, wamekabidhi Sh. milioni 10 kwa Joseph Mkombozi (23), kutoka Kijiji cha Makole, Muheza mkoani Tanga, baada ya kuibuka mshindi katika Promosheni ya Tunza, Utunzwe na M-Pawa.

Mpawa ni huduma inayotolewa kwa ushirikiano wa Vodacom na Benki ya CBA, inayomwezesha mtumiaji wa mtandao wa Vodacom kukopa fedha na kuhifadhi hela kupitia simu yake ya mkononi.

Akizungumza juzi jijini Dar es Salaam baada ya kukabidhiwa hundi yake ya Sh. milioni 10, Mkumbuzi alishukuru benki ya CBA kwa ubunifu wake wenye lengo la kuinua maisha ya Watanzania.

"Niwashukuru CBA kwa wazo hili ambalo kwa kiasi kikubwa linamfaidisha Mtanzania wa aina yoyote ile atakayekuwa ameshiriki," alisema.

Mwakilishi wa Benki ya CBA, Gloria Njiu, alisema kuwa, tangu kuanza kwa promosheni hiyo Oktoba, mwaka jana, kumekuwa na washindi mbalimbali wakiwamo waliojishindia bodaboda.

"Wakati tunahitimisha promosheni hii kwa kumzawadia mshindi wa milioni 10, ifahamike kuwa tumekuwa na washindi wengine zaidi ya 300 ambao walijishindia bodaboda na mara mbili ya amana zao walizohifadhi kwenye M-Pawa," alisema Gloria.

Kwa mujibu wa Glory washindi waliojishindia bodaboda ni pamoja na Christina Toto (Manyara), Johnson Mollel (Arusha), Fravianus Frugence (Bukoba Mjini), Letisia Yohana (Dar es Salaam), Herman Mwakapeje (Mbeya) na Egiduis Buberwa (Tabora).

Wengine ni Grace Mollel (Arusha), Musa Kuyava (Iringa), Joseph Renatus (Shinyanga), Sadiki Rashidi (Dodoma), Emmanuel Tesha (Iringa), Grace Ginesasi (Mbeya), John Joseph (Moshi Mjini), Daudi Daudi ( Bunju), Mwashabani Kiegebu (Zanzibar), Fidelis Mfuse (Njombe), Angelina Mkota (Dodoma) na Aswile Mapanga kutoka Mbeya Mjini.

Tangu kuanzishwa kwa huduma ya M-Pawa, watumiaji wake wameongezeka kwa kasi hadi kufikia milioni tisa nchini kote.

# TIC yatabiri pato la Mtanzania kupaa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KITUO cha Uwekezaji Tanzania (TIC), katika Ofisi ya Waziri Mkuu, kimetabiri kuwa pato la Mtanzania mwaka huu litakuwa Dola za Marekani 1,550 na litaendelea kukua hadi kufikia dola 1,707 mwaka kesho.

Pato la Taifa (GDP) litakua kwa asilimia 7.1 kwa miaka yote miwili. Utabiri huu umo katika mada ya TIC iliyowasilishwa na Mkurugenzi Mkuu wa Kituo hicho, Geoffrey Mwambe kwa wajumbe wa kamati 12 za kudumu za Bunge.

Andiko hilo linaeleza, kwa takwimu, mafanikio ya Tanzania katika kuvutuia na kusajili miradi ya wawekezaji wa nje na wa ndani na kuonyesha mafakinio ya serikali ya Rais John Magufuli katika vita ya kuinua pato la Mtanzania.

Takwimu za kituo hicho zinaonyesha ukuwaji wa uchumi wa Tanzania umekuwa madhubuti na wenye kasi ya mvuto hasa kuanzia 2016. Mwaka 2016 pato la taifa lilikua kwa asilimia 6.9, lakini pato la Mtanzania lifikia dola 1,071; mwaka 2017 pato la taifa lilikua kwa asilimia saba, lakini pato la Mtanzania lilifikia dola 1,178; mwaka 2018 uchumi ulikuwa kwa asilimia 7.1, lakini pato la Mtanzania liliongezeka na kufika dola 1,293. Mwaka jana pato la taifa lilikua kwa asilimia 7.1 nalo pato la Mtanzania likakua na kufika dola 1,416.

Mwaka huu pato la taifa linatarajiwa kukua kwa asilimia 7.1 na pato la Mtanzania latarajiwa kuchupa na kufia dola 1,550. Mwakani matarajio ni kwamba uchumi utakua kwa asimilia 7.1 na pato la Mtanzania litainuka na kuwa dola 1,707.

Mwambe aliwaeleza wabunge kwamba kidunia Tanzania pia inaendelea kuwa kivutio cha wawekezaji wa nje, licha ya changamoto zinazozikabili nchi duniani kote katika kuvutia wawekezaji.

Kwa kutumia mchanganuo uliotolewa na Rand Merchant Bank wa 2018, Mwambe aliwaeleza wabunge kwamba Tanzania ni nchi ya saba kati ya nchi 10 bora za Afrika zenye kuvutia wawekezaji. Nchi ya kwanza katika kundi hilo ni Misri ikifuatiwa na Afrika Kusini. Katika Afrika ya Mashariki Kenya ni ya tano.

Andiko linazitaja nchi 10 za daraja la juu katika kuwekeza Tanzania katika kipindi cha 1990 hadi Desemba 2018 kuwa ni China, Uingereza, Marekani, Mauritius, India, Australia, Kenya, Uholanzi, Ubelgiji na Misri.

Nchi zote hizo kwa pamoja zina miradi nchini 3,173 yenye thamani ya dola za Marekani milioni 29,120.36 na miradi hiyo imeibua ajira 549,770.

Katika kipindi hicho andiko linaonyesha miradi 11,509 ilisajiliwa katika sekta 15. Kati ya hiyo 9,248 ni mipya, 3,500 imepanuliwa, 3,173 ni ya ubia na 6,047 ni ya Watanzania. Kati ya miradi yote hiyo, asilimia 43 ni ya Watanzania, asilimia 28 ni ya wageni na asilimia 29 ni miradi ya ubia. Miradi hiyo imesajiliwa katika sekta za kilimo, maliasili, utalii, viwanda, petroli na madini, majengo ya biashara, usafirishaji, huduma, kompyuta, taasisi za kifedha, simu na mawasiliano, nishati, raslimali watu, miundombinu na utangazaji.

Mikoa 10 ya juu ambayo imenufaika ya uwekezaji kati ya 1997 na 2018 ni Dar es Salaam, Arusha, Pwani, Mwanza, Kilimanjaro, Tanga, Morogoro, Iringa, Mbeya na Shinyanga.

Changamoto zinazotajwa na andiko hilo ni mabadiliko ya mara kwa mara ya vivutio vya uwekezaji, urasimu katika utoaji huduma kwa wawekezaji, uhaba wa miundombinu kwa ajili ya uwekezaji, uchache wa watumishi na rasilimali za kufanikisha uwekezaji, sheria ya VAT ya 2014 na mapungufu katika Sera ya Taifa ya Uwekezaji ya 1996 na Sheria ya Uwekezaji ya 1997.



Basi la kampuni ya Shukrani lililokuwa linatoka Dodoma kwenda Dar es Salaam likiwa limeteketea kwa moto baada ya tairi kupasuka mkoani Morogoro jana. **PICHA: IDDA MUSHI**

# Pinda atoa neno ufufuaji wa zao pareto

**Na Silvanus Kigomba,** IRINGA

WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, amesifu jitihada zinazofanywa na Kampuni ya Pareto Tanzania (PCT) ya kufufua zao la pareto nchini kupitia kiwanda cha pareto cha mjini Mafinga mkoani Iringa.

Pinda alisema jitihada hizo zimekuja muda mwafaka wakati ambao serikali ya inapambana kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda kupitia kauli mbiu ya Rais John Magufuli ya "Tanzania ya viwanda," inayolenga kukuza uchumi wa nchi.

Pinda alisema hayo alipotembelea kiwanda hicho jana akiwa kwenye ziara ya kukagua uzalishaji kwenye baadhi ya viwanda wilayani Mufindi ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 43 ya kuzaliwa kwa Chama Cha Mapinduzi CCM yaliyofanyika kimkoa mjini Mafinga.

Pinda alisema jitihada hizo zinapaswa kuungwa mkono na serikali ikiwamo kuweka ushindani sawa katika ununuzi wa zao la pareto na kuongeza kuwa haoni sababu ya wanunuzi wasiowekeza chochote kwa wakulima kuruhusiwa kununua pareto wakati kampuni hiyo imeshawekeza kwa wakulima kwa kutoa usaidizi wa namna mbalimbali ikiwamo kutoa mbegu elimu na ushauri wa kitaalamu.

Akijibu baadhi ya maswali ya Pinda, meneja uzalishaji wa kiwanda hicho, Benedict Kafyulilo, alisema kiwanda hicho kinachozalisha zaidi ya tani 2,000 kinafanya juhudi kuongeza uzalishaji kufikia angalau zaidi ya tani 4,000 zitakazowezesha kiwanda kufanya kazi mfululizo mwaka mzima, hali itakayowezesha baadhi ya bidhaa zitokanazo na pareto hiyo kuzalishwa kiwandani hapo.

Pinda aliutaka uongozi wa Mkoa wa Iringa kuhamasisha kilimo cha pareto ili kuinua uchumi wa wakulima pamoja na mkoa wa ujumla. "Mkuu wa mkoa ni wakati wenu sasa kuhamasisha kilimo hiki cha pareto kwani ni moja ya mazao ambayo yanaweza kuupandisha mkoa wenu kimapato hasa ukizingatia mnacho kiwanda ambacho kinaliongezea thamani zao hili," alisema Pinda.

## HABARI MICHEZO

# ABIDAL AMVUTA NEYMAR BARCA




**BARCELONA,** Hispania

KAMA Neymar atarudi Barcelona ataiimarisha zaidi klabu hiyo, kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Soka, Eric Abidal.

Nyota huyo wa kimataifa wa Brazil aliondoka pale Camp Nou kwenda kujiunga na PSG kwa ada iliyoweka rekodi ya euro milioni 222 Agosti mwaka 2017, lakini amekuwa akihusishwa na mpango wa kurejea tena Barca.

Kocha Mkuu, Quique Setien alisema wiki iliyopita atafurahi nafasi ya kumnoa Neymar na Abidal anaamini dili hilo linawezekana.

Alipoulizwa maoni yake kuhusu Neymar kurudi tena kwa miamba hao wa Catalunya, Abidal aliiambia Mundo Deportivo: "Kwa uhakika kabisa nakubali.

"Quique atajisikia furaha kumfundisha mchezaji kama Neymar na wachezaji wengine hapa walipo kwenye daraja lake."

Barca imeachwa na uhaba kwenye safu ya ushambuliaji baada ya Luis Suarez na Ousmane Dembele kuumia, ingawa Ansu Fati alionyesha kiwango cha kuvutia wikendi iliyopita wakati akifunga mara mbili kwenye ushindi wa 2-1 dhidi ya Levante.




# Ighalo akosa mazoezi Utd

**MANCHESTER,** England

ODION Ighalo ambaye alijiunga na Manchester United kwa mkopo hadi mwisho wa msimu katika siku ya mwisho ya dirisha la uhamisho la Januari atakosa mazoezi na klabu yake hiyo mpya.

Mshambuliaji huyo atakosa mazoezi na klabu hiyo nchini Hispania kutokana na hofu kwamba virusi vya corona vinaweza kumzuia kuruhusiwa kuingia nchini England.

Ighalo mwenye umri wa miaka 30, alisafiri kuelekea mjini Manchester kutoka China wikendi iliyopita baada ya kutia saini kandarasi ya mkopo kutoka klabu ya Shenghai Shenhua.

"Angependelea kujiunga na wachezaji wengine ili kuweza kujuana," alisema kocha Ole Gunnar Solskjaer akizungumza na runinga ya MUTV.

"Lakini hatari ya masharti ya mpakani, hatutaki kuhatarisha."

Wakati huohuo kiungo wa kati wa Man United, Scott McTominay na beki Axel Tuanzebe ambao wote wamekuwa na majeraha ya muda mrefu watasafiri kuelekea Hispania.

United hawatarudi hadi siku ya Ijumaa kabla ya mechi yao ya Ligi ya England dhidi ya Chelsea katika Uwanja wa Stamford Bridge Februari 17, mwaka huu.

# Vidal atamfuata Sanchez Inter, asema Zamorano

**BARCELONA,** Hispania

KIUNGO wa Barcelona, Arturo Vidal anapanga kujiunga na mchezaji mwenzake wa Chile, Alexis Sanchez pale Inter Milan, kwa mujibu wa mshambuliaji wa zamani wa 'Nerazzurri' hao, Ivan Zamorano.

Vidal alikuwa akihusishwa zaidi na mpango wa kujiunga na kikosi hicho cha Antonio Conte kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili la Januari, lakini uhamisho huo haukufanikiwa.

Sanchez anacheza pale Inter kwa mkopo akitokea Manchester United hadi mwishoni mwa msimu huu huku 'Mashetani Wekundu' hao wakipanga kumrejesha Old Trafford, Zamorano anaamini raia hao wa Chile watacheza pamoja kwenye klabu hiyo ya Serie A msimu wa 2020-21.

"Yeye (Sanchez) ana mkataba na Manchester United, lakini tutaangalia wapi anataka kuendelea kucheza na wapi anakohisi kuwa na furaha," nguli wa Chile, Zamorano, ambaye alishinda taji la Uefa msimu wa 1997-98 akiwa na Inter, aliiambia Radio Cooperativa.

"Kitu cha msingi ni kwamba, Alexis anafurahia soka, kwa sababu wakati alipokuwa anatafuta kiwango chake, alipatwa na majeraha. Hakucheza zaidi pale sana Manchester na wakati alipotua hakuwa fiti.

"Ningependa Sanchez kubakia Milan, hasa Juni kwani atakuwa na nafasi ya kucheza na raia mwingine wa Chile, ambaye pengine atakuja klabuni hapa."



## HABARI MICHEZO

# Martinez azikataa Manchester United, City

**BARCELONA,** Hispania

LAUTARO Martinez wa Inter Milan ameamua kuzitosa Klabu za Manchester United na Manchester City ili atue Nou Camp pindi dirisha la usajili la majira ya joto litapofunguliwa Juni mwaka huu.

Man City na Man United zimetumia miezi sita iliyopita kumfuatilia straika huyo wa kimataifa wa Argentina, huku zikiamini zinaweza kumsajili kabla ya kuanza kwa msimu ujao, lakini sasa harakati zao zimegongwa mwamba.

Martinez ambaye kipengele chake cha kumruhusu kuondoka Inter Milan kwa dau la pauni milioni 94 kinaisha Julai, anaamini Barcelona ndiyo sehemu sahihi kwake ndio maana ameamua kuzipotezea Man United na Man City.

Straika huyo anaamini akitua Barcelona atapata nafasi ya kucheza kwa muda mrefu kwa sababu straika chaguo namba moja wa timu hiyo, Luis Suarez umri umeanza kumtupa mkono na anasumbuliwa na majeraha, na yeye anaamini ndiye atakayemrithi.





# ARSENAL SASA KUWAUZA OZIL NA AUBAMEYANG

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta ameripotiwa kwamba amepanga kufanya mabadiliko makubwa kwenye kikosi chake kwa kupitisha panga ili kuanzisha zama zake mpya ndani ya Emirates.

Kinachoripotiwa ni kwamba panga hilo halitachagua, litawapitia hata wachezaji wanaotajwa kuwa ni mastaa wakubwa ndani ya kikosi hicho.

Nyota kama Pierre-Emerick Aubameyang, Alexandre Lacazette na Mesut Ozil wote wametishwa huenda wakapitiwa na panga hilo la Arteta, ambaye mpango wake ni kutengeneza kikosi cha wachezaji watakaokuwa tayari kucheza chini yake.

Kocha huyo mpya huko Emirates, Arteta hafurahishwi na kitendo cha timu kutokuwa na maendeleo mazuri tangu alipoteuliwa kuchukua mikoba wiki saba zilizopita.

Na sasa anaamini kikosi chake hicho kinachocheza soka la kiwango duni kinahitaji kufanyiwa marekebisho makubwa baada ya kufanya tathmini ya kutambua ubora na udhaifu wa kikosi hicho alichokirithi kutoka kwa Unai Emery.

Hofu kubwa iliyopo kwenye timu kwa sasa ni hatari ya kushindwa kufuzu kushiriki michuano yoyote ya Ulaya kwa mara ya kwanza tangu 1996, jambo ambalo Arteta amesema itabidi apige bei baadhi ya mastaa kwenye dirisha la mwishoni mwa msimu ili kunasa saini za mastaa wapya watakaokuja Emirates kupiga mzigo.

Mastaa sita wenye majina makubwa katika kikosi hicho, wakiwamo wanaolipwa mishahara mikubwa kama Ozil na Aubameyang, ambao wote mikataba yao imebakiza miezi 18 tu kufika tamati huko Emirates ni miongoni mwao.

# *Guadiola: Ubingwa EPL basi tena*

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola amesema haitakuwa mwisho wa dunia kama Manchester City itashindwa kubeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu kwa sababu msimu ujao michuano hiyo itakuwapo pia.

Siku chache zimepita tangu kocha huyo Mhispaniola aliposema atajihesabia amefeli kama hataisaidia Man City kubeba taji la Ulaya, lakini sasa amesema hiyo haitakuwa mwisho wa maisha.

Man City inakabiliwa na kibarua cha kuchuana na Real Madrid katika mtoano wa hatua ya 16-bora kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa msimu huu.

Guardiola, ambaye mkataba wake umebakiza miezi 18 tu kufika tamati huko Etihad, alisema: "Kitu pekee ambacho Man City haina ni taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Nitajaribu kulisaka taji hilo mwaka huu kama si mwakani, dunia haitakuwa imefika mwisho."


Guardiola anaendelea kusaka mataji msimu huu baada ya msimu uliopita kufanya kweli iliponyakua mataji yote matatu ya England.

"Man City ilikuwa klabu ambayo muongo mmoja uliyopita kitu ilichokuwa ikitaka ni kubaki tu kwenye Ligi Kuu England.

"Ghafla tu wakaja watu wa Abu Dhabi wakachukua timu na hapo wakabeba mataji manne ya ligi."

Guardiola kwa sasa anapewa nafasi kubwa ya kumnasa mchezaji wake za zamani, Lionel Messi ili akakipige Etihad baada ya kutibuana na miamba ya Camp Nou, Barca.

Chama hilo la Guardiola, Man City jana Jumapili lilishuka dimbani kumenyana na West Ham United katika mchezo wa Ligi Kuu England na Februari 26 watakipiga na Real Madrid kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI KUSAINI MKATABA MPYA SI RAHISI - ABIDAL

**Alisema Barca ni kila kitu kwake yeye, anataka kuendelea kuwa hapa, lakini kuna masharti...**

**BARCELONA,** Hispania

LIONEL Messi anataka kubaki Barcelona, lakini "haiwezi kuwa rahisi" kusaini mkataba mpya, kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Ufundi wa klabu hiyo, Eric Abidal.

**Majaliwa ya Messi klabuni hapo yapo shakani baada ya wiki iliyopita kutokea "matafuruku" pale Camp Nou, ambapo alimtuhumu Abidal kwenye mtandao wa kijamii kuhusu kauli yake kwamba kikosi hicho kilikuwa hakijitumi chini ya kocha wa zamani, Ernesto Valverde.**

Nahodha huyo wa Barca alimtaka Abidal kutaja majina na alimshutumu kwa yeye "kukichafua" kikosi akibainisha kwamba nyota kadhaa walikuwa hawajitumi kabla ya Valverde kutimuliwa.

Huku Messi mkataba wake ukisema kwamba anaweza kuondoka huru mwishoni mwa msimu huu, kumekuwa na uvumi kwamba anaweza kutafuta changamoto nyingine kwa msimu mpya wa 2020-21, ingawa Pep Guardiola alisisitiza Ijumaa hataki Manchester City wamsajili nyota huyo wa kimataifa wa Argentina.

Abidal anaonyesha kuwa na matumaini ya Messi kuongeza mkataba wake, ambao utamalizika Juni 2021, lakini alisema ni vigumu kufanya mazungumzo na mchezaji huyo ambaye ni bora zaidi duniani.

"Swali ni kwake," alisema akiiambia Mundo Deportivo wakati alipoulizwa kuhusu mkataba wa Messi. "Matumaini yangu ataendelea.

"Leo alisema Barca ni kila kitu kwake yeye, kwamba anataka kuendelea kuwa hapa, lakini kuna masharti. Tunazungumza kuhusu mchezaji bora duniani na kuongeza mkataba kwa mchezaji kama huyo haijawahi kuwa rahisi."

Messi mara zote ameonekana kwamba atamaliza kipindi chake cha kucheza Ulaya akiwa na Barca, ingawa alisema anataka klabu iliyopo imara kutoa changamoto kwenye Kombe la Ligi Kuu ya Hispania, La-Liga na Ligi ya Mabingwa Ulaya kabla ya kusaini mkataba mpya.

Abidal anaonekana kuwa na matumaini makubwa kwamba, Barca wana nafasi ya kutwaa taji hilo la Ulaya msimu huu, akidai kwamba wanaweza kuwa timu isiyofungika kama watacheza katika kiwango chao cha juu.

"Ligi ya Mabingwa Ulaya ni muhimu. Tunajua kwamba changamoto ni ngumu," alisema kuelekea mchezo wao dhidi ya Napoli kwenye hatua ya mtoano wa timu 16-bora.

"Kwa upande wangu mpinzani wa Barca ni Barca. Kama timu ni nzuri, itakuwa ngumu kwa upande wetu kupoteza."

Matumaini ya Barcelona kubeba taji tayari yameingia doa baada ya kumpoteza Luis Suarez, ambaye hatarudi dimbani hadi mwishoni mwa msimu baada ya kuumia goti.

Mshambuliaji huyo pia mkataba wake utafikia ukingoni mwishoni mwa msimu ujao, lakini Abidal anatarajia wataanza majadiliano kuhusu mkataba mpya muda utakapowadia.

"Kwanza unatakiwa kuwaheshimu wachezaji, kwa kile wanachokifanya, kile walichokifanya kabla na nini watakachokifanya kwa klabu," alisema.

## ZISIKUPITE

### GREALISH KUONDOKA VILLA

NYOTA wa Aston Villa, Jack Grealish mwenye umri wa miaka 24, ataangalia uwezekano wa kuondoka kipindi cha majira ya joto, licha ya kuwa kipenzi cha klabu yake hiyo ya utotoni. Manchester United na Manchester City zimekuwa zikihusishwa kumtaka kiungo huyo wa Muingereza. ***(Telegraph)***

### CITY YAKUBALI KUMKOSA MESSI

KLABU ya Manchester City ipo tayari kukubali kukataliwa kwa ofa yao kwa Lionel Messi kuja Ligi Kuu ya England msimu ujao, baada ya kuambiwa kwamba mshambuliaji huyo wa Argentina mwenye umri wa miaka 32, hana mpango wa kuondoka Barcelona. ***(Express)***

### STERLING FITI KUIVAA MADRID

NYOTA wa Manchester City, Raheem Sterling anaamini atarudi kuwa fiti kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Real Madrid, ambao wamekuwa na nia ya kutaka kumsajili mshambuliaji huyo wa England mwenye umri wa miaka 25. ***(Telegraph)***

### POCHETTINO AIWAZA UNITED

KOCHA wa zamani wa Tottenham Hotspurs, Mauricio Pochettino bado yupo kwenye mchakato wa kuwa kocha mpya wa Manchester United msimu ujao. ***(Mirror)***

### COUTINHO KUONDOKA BARCA

KIUNGO wa Barcelona raia wa Brazil, Philippe Coutinho mwenye umri wa miaka 27, ambaye kwa sasa anacheza kwa mkopo kule Bayern Munich - ataruhusiwa kuondoka kwa bei pungufu ya pauni milioni 77 kipindi cha majira ya joto kijacho, huku Manchester United na klabu yake ya zamani, Liverpool zikitajwa kuwania kumsajili. ***(Express)***

### DE BRUYNE ANG'ANG'ANA CITY

KIUNGO wa Manchester City raia wa Ubelgiji, Kevin de Bruyne mwenye umri wa miaka 28, ambaye amekuwa akihusishwa na mpango wa kutakiwa Real Madrid na Barcelona, amesema "ameridhika" na klabu yake ya sasa ya Manchester City ambao ni mabingwa wa Ligi Kuu ya England. ***(Goal.com)***

### BALE HATAKI KURUDI SPURS

MSHAMBULIAJI wa Wales, Gareth Bale mwenye umri wa miaka 30, alitaka "kulifanya soka la China kuwa kubwa" wakati alipohusishwa na mpango wa kwenda bara hilo la Asia kipindi cha majira ya joto mwaka jana, amedai wakala wake, lakini sasa anapanga kubakia pale Real Madrid na hatarudi kwenye Ligi Kuu ya England katika Klabu yake ya zamani ya Tottenham. ***(Goal.com)***

### JAY Z ATUA KWA RASHFORD

STRAIKA wa Manchester United na England, Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 22, yupo kwenye mazungumzo ya udhamini na Kampuni ya Rapa milionea wa Marekani, Jay-Z, Roc Nation Sports. ***(Mirror)***

### CAVANI TAYARI KUTUA EPL

MSHAMBULIAJI wa Uruguay, Edinson Cavani mwenye umri wa miaka 32, ambaye alihusishwa na Manchester United na Chelsea msimu wa dirisha dogo la usajili lililopia, amefungua mlango wa kwenda England wakati mkataba wake utakapomalizika pale Paris St-Germain kipindi kinachokuja cha majira ya joto. ***(L'Equipe, via Star)***

HABARI MICHEZO

## Waamuzi 7 wakataa kuchezesha Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

SHIRIKISHO la Soka nchini (TFF), limesema waamuzi wameanza kuzikimbia mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara, kutokana na woga na presha.

Hali hii inatokana na malalamiko na mihemko ya mashabiki wa soka nchini kwa siku za karibuni kutokana na baadhi ya waamuzi kuonekana kukosea kutafsiri sheria 17 za soka kwenye baadhi ya mechi.

Katibu Mkuu wa TFF, Wilfred Kidao amesema jumla ya waamuzi saba wameomba kutopangwa kwenye mechi za Ligi Kuu licha ya kutofanya makosa yoyote yale.

Katika mkutano wake na waandishi wa habari wakati wa kumtangaza Ofisa Mtendaji mpya wa Bodi ya Ligi (TPLB), Almasi Kasongo, anayechukua nafasi ya anayemaliza muda wake, Boniface Wambura, Kidao alisema kuwa anaamini kutokana na presha iliyopo sasa wameingiwa na woga.

"Wiki hii tu, tuna waamuzi saba wameomba wasipangwe kuchezesha mechi za Ligi Kuu wakati hawajafanya makosa," alisema na kuongeza.

"Ni woga, lakini bila shaka sisi tunafanya kazi kubwa kuwaondoa kwenye woga. Bila shaka ukipewa nafasi ya kusimamia mechi ni dhamana kubwa uliyonayo. Jambo kubwa ni kuongeza umakini na kujiamini. Kwa hiyo ni kuwatengeneza kisaikolojia kwamba ni kazi nzuri, kubwa na ukiaminiwa maana yake si jambo dogo. Kwa hiyo nyie waandishi mna kalamu zenu, mnacho cha kusemea, mnaweza mkasema watu wakawasikiliza. Vyombo vya habari vina nguvu kubwa, wakati tunakwenda kuchambua, tuchambue kwa maana ya kujenga."

# JULIO AIONYA SIMBA KUMTIMUA SVEN

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI mashabiki wa Simba wakipiga kelele kwa uongozi wa timu hiyo wakitaka Kocha Mkuu, Mbelgiji Sven Vandenbroeck atimuliwe, mchezaji wa zamani na kocha aliyewahi kuinoa kwa nyakati tofauti, Jamhuri Kihwelu 'Julio', ameionya klabu hiyo akiitaka kuwa makini katika kuchukua uamuzi huo.

Ijumaa iliyopita, Simba ilikubali kipigo cha bao 1-0 katika Uwanja wa Uhuru kutoka kwa JKT Tanzania, matokeo ambayo yalipokelewa kwa mtazamo hasi kutoka kwa mashabiki wa timu hiyo wakidai licha ya timu hiyo kushinda baadhi ya mechi ikiwa chini ya Sven, imekuwa haichezi vizuri kama wakati ikinolewa na mtangulizi wake, Mbelgiji Patrick Aussems 'Uchebe'.

**Walisema mfumo anaotumia kocha huyo wa mshambuliaji mmoja mbele ni moja ya chanzo cha timu hiyo kushindwa kupata matokeo mazuri na kucheza chini ya kiwango kwa kuwa hutoa nafasi kwa wapinzani wao kuwashambulia zaidi.**

Lakini, Julio juzi alisema Simba inatakiwa kumpa muda Sven ili wachezaji waweze kuzoea falsafa zake hasa ukizingati ukweli kwamba kocha huyo amekuja katikati ya msimu na hakuwa na muda wa kufanya maandalizi na kikosi chake.

Alisema Simba ilifanya makosa kumfukuza Uchebe, lakini na tatizo lingine ni kwamba mashabiki wanataka timu ishinde siku zote.

"Mashabiki siku zote wanataka timu ishinde, lakini huu si wakati wa kumfukuza kocha bado anahitaji muda ili wachezaji waweze kuzoea falsafa zake, kosa kubwa walilolifanya ilikuwa kumtoa Uchebe," alisema Julio huku akiongeza kuwa tatizo lingine kikosi cha Simba kinaundwa na wachezaji wengi ambao umri unawatupa mkono.

Tangu Sven ametua Simba, ameiongoza katika mechi 10 za Ligi Kuu akishinda nane, sare moja na kupoteza mchezo mmoja, wakati huu timu hiyo ikiwa kileleni mwa ligi hiyo na pointi 50.

Mabingwa hao watetezi tayari wametua mjini Morogoro kwa mechi yao ya kesho dhidi ya Mtibwa Sugar itakayopigwa Uwanja wa Jamhuri.



Wasanii wa kikundi cha Bombeso wakicheza wakati wa hafla ya uzinduzi wa picha iliyochorwa na Athuman Hamis mshindi wa shindano la Sanaa ya Uchoraji 2020 lililoandaliwa na Kampuni ya Bia nchini kupitia bia yake ya Kilimanjaro kuelekea kilele cha mbio za Kili Marathon zinazotarajiwa kufanyika Machi Mosi, 2020. Hafla ya uzinduzi ilifanyika katika Hoteli ya Coral Beach jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Kili Canvas kunogesha Kilimanjaro Marathon*

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bia Tanzania (TBL) kupitia bia yake ya Kilimanjaro Premium Lager, imezindua Kili Canvas itakayotumika kuhamasisha wanariadha wa vitongoji tofauti vya jijini Dar es Salaam na mji wa Moshi katika kuelekea kilele cha mbio za Kili Marathon zinazotarajiwa kufanyika Machi Mosi, mwaka huu mkoani Kilimanjaro.

Aidha, huelekea mbio hizo, hivi karibuni Kampuni ya Bia Tanzania (TBL) kupitia bia yake ya Kilimanjaro Premium Lager ilianda shindano la uchoraji maarufu kama "Jiachie na Kili Canvas Competition 2020" na washiriki walitakiwa kuchora mchoro kwenye kitambaa kigumu (Canvas) kuelezea bia ya Kilimanjaro Premium Lager na mashindano ya riadha ya Kili Marathon.

Athumani Hamis kutoka Dar es Salaam aliibuka mshindi katika shindano hilo ambapo, mbali na kujishindia Sh. milioni mbili ambazo alikabidhiwa wiki iliyopita, alitakiwa kuchora mchoro wa Kili (Kili Canvas) kwa ukubwa zaidi kwa ajili ya kutumika kama hamasa kuelekea kilele cha Kili Marathon Machi Mosi, mwaka huu, mkoani Kilimanjaro.

Washindi wengine ambao awali walikabidhiwa zawadi katika shindano hilo ni mshindi wa pili mpaka wa tano waliojinyakulia pesa taslimu Sh. 200,000 kila mmoja, ambao ni Donath Kabonda (Gongo la Mboto), Moses Martin (Mwenge Vinyago), August Tairo (Kijitonyama) na George Nyandiche kutoka Morogoro Store Oysterbay.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo uliofanyika katika Hoteli ya Coral Beach, jijini Dar es Salaam wiki iliyopita, Meneja wa Bia ya Kilimanjaro Premium Lager, Pamela Kikuli, alisema Kili Canvas itawekwa katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam na baadaye mjini Moshi ili kuwahamasisha wakimbiaji mbalimbali kuelekea kilele cha Kili Marathon.

Alifafanua zaidi kuwa kutakuwa na 'Chip' maalumu ambayo mkimbiaji atatakiwa kuwa nayo wakati akikimbia na atakapopita kwenye Canvas atapigwa picha na itatumwa moja kwa moja kwenye simu yake.

"Ili uweze kupigwa picha na kutumiwa kwenye simu yako kwa wale wakimbiaji ni lazima ujisajili na kupewa Chip maalumu ambayo utaelekezwa wapi pa kuiweka wakati unakimbia. Mara tu utakapopita karibu na Canvas kamera zetu zitakutambua na kukupiga picha kwa teknolojia maalumu na kutumiwa papo hapo kwenye simu yako," Kikuli alisema.

Kwa mujibu wa meneja huyo, usajili kwa ajili ya kujipatia Chip hiyo ni ulianza Februari 8 na 9, (Mlimani City), huku Februari 13, 14 na 15, ukiendela pale Shoppers Mikocheni na Mbezi) jijini Dar es Salaam. Wakati Februari 15 na 16, mwaka huu itakuwa ni kwa wakazi wa Moshi, mkoani Kilimanjaro.

"Kadi hizi zimeanza kupatikana hapa Dar es Salaam pale Mlimani City na (zitaendelea Shoppers Mikocheni na Mbezi). Mtu yeyote anayependa mchezo wa kukimbia au anayefanya mazoezi ya kukimbia, anaweza kujipatia Chip hii kwa kipindi hiki ambacho tunafanya hamasa kwa ajili ya kuelekea kilele cha mbio za Kili Marathon," alisisitiza Kikuli.

Aidha, Kikuli alivitaja vituo vitakavyowekwa Canvas hiyo kuwa ni Masaki, Goba na Temeke kwa Dar es Salaam na baadaye kuhamia Moshi, mkoani Kilimanjaro.

Katika hatua nyingine, Kikuli aliwapongeza washiriki wote waliojitokeza kushiriki shindano la 'Jiachie na Kili Canvas Competition 2020' lililofanyika kwa mara ya kwanza mwaka huu, akisifu ubora wa kazi zao. "Washiriki wote walifanya vizuri ila mwisho wa siku tukapata mshindi mmoja kutokana na taratibu za shindano lenyewe. Nimuombe mshindi wetu kwamba, kwa kile kidogo tulichomzawadia akitumie kama chachu ya kuendeleza sanaa yake pamoja na wasanii wengine waliomzunguka."

# Michezo

Jumatatu Februari 10, 2020

Nipashe





Messi kusaini mkataba mpya si rahisi - Abidal UKURASA 30


MNAHESABU?...



David Molinga akipongezwa na mchezaji mwenzake, Papy Tshishimbi (Kushoto) baada ya kuifungia Yanga bao pekee wakati ikishinda 1-0 dhidi ya Ruvu Shooting juzi. Hilo ni bao la sita kwa Molinga kwenye Ligi Kuu msimu huu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# MOLINGA AVUTIWA KIATU CHA KAGERE

## ●●● Mpishi wa mabao Yanga aanika mkakati, kesho kujiuliza wakizivaa Mbeya City, Mtibwa...

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU ikiwa katika mbio za kuikamata Simba kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu, wachezaji wa Yanga pia wamepania kuhakikisha wanakivuta Kiatu cha Dhahabu cha mfungaji bora wa ligi hiyo na kutua kwa mchezaji wa timu hiyo.

**Mfungaji Bora wa Ligi Kuu msimu uliopita, mshambuliaji wa Simba, Mnyarwanda Meddie Kagere hadi sasa ndiye anayeongoza katika orodha ya wafungaji msimu huu akiwa na mabao 12 akifuatiwa na Reliants Lusajo wa Namungo (mabao 9), huku Paul Nonga pamoja na Daruwesh Saliboko wote kutoka Lipuli kila mmoja tayari akiwa amecheka na nyavu mara nane.**

Kwa Yanga ambayo ipo nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi hiyo ikiwa na alama 37, pointi 13 nyuma ya Simba iliyopo mbele yao kwa michezo miwili, mshambuliaji anayekuja kwa kasi katika uchekaji na nyavu kwenye klabu hiyo ni Mkongomani David Molinga ambaye yupo kundi la wachezaji wenye mabao sita hadi sasa.

Katika orodha hiyo, wachezaji wengine wenye mabao sita sawa na Molinga ni pamoja na Miraji Athumani wa Simba, Waziri Junior (Mbao), Ayoub Lyanga (Coastal Union) na Adam Adam wa JKT Tanzania.

Na katika kuhakikisha hilo linatimia kwa Yanga kutoa mfungaji bora, straika wa timu hiyo ambaye amegeuka kuwa mpishi mzuri wa mabao, Ditram Nchimbi, akili yake kwa sasa ni kuhakikisha Kiatu cha Dhahabu cha ligi hiyo kinatua kwa mchezaji wa timu hiyo.

Nchimbi alianza kuifanya kazi hiyo katika mchezo dhidi ya Mtibwa Sugar, akitoa pasi ya bao lililofungwa na Molinga, kabla ya juzi wakati wakiibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Ruvu Shooting, kufanya hivyo tena kwa kupiga krosi iliyotua kichwani kwa Mkongomani huyo na kuutumbukiza mpira nyavuni.

Hata hivyo, Nchimbi amesema nafasi hiyo ya kuwa mfungaji bora ni muhimu kwake, lakini kwa sasa yupo kwa ajili ya timu zaidi, hivyo anatamani kuona anakuwa na mchango mkubwa katika kumtoa mfungaji ndani ya kikosi chao.

"Kusema nafukuzia ufungaji bora si rahisi, lakini ukiangalia wapo ambao wana mabao mengi na wenye nafasi hiyo zaidi yangu, ukweli mimi nitafurahi nikiona nakuwa sehemu ya mafanikio ya mchezaji wa timu yangu akipata nafasi hiyo," alisema Nchimbi.

Nchimbi ambaye ametua Yanga akitokea Polisi Tanzania katika usajili wa dirisha dogo alisema ushirikiano uliopo kati yake na wachezaji wenzake, sambamba na benchi la ufundi unawapa kujiamini zaidi kwa sasa.

Molinga atakuwa na nafasi ya kuongeza kasi ya kuwania kukaa kileleni mwa orodha ya wafungaji bora wakati Yanga itakaposhuka Uwanja wa Taifa kesho kuikaribisha Mbeya City, huku Kagere naye akitaka kujichimbia kileleni zaidi wakati Simba ikishuka dimba la Jamhuri mkoani Morogoro kuvaana na Mtibwa Sugar.

# Yanga taratibu sasa inakolea

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Kocha Mkuu wa Yanga, Mbelgiji Luc Eymael, akisema kama washambuliaji wake wangeongeza umakini na kutumia nafasi walizopata, Ruvu Shooting wangechezea bao nyingi, nahodha msaidizi wa timu hiyo, Juma Abdul amesema 'gari ndiyo' limewaka hivyo baada ya wachezaji kuanza kuzinasa mbinu za kocha huyo.

Yanga juzi iliibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Ruvu Shooting katika mechi ya Ligi Kuu iliyopigwa Uwanja wa Uhuru, bao pekee likifungwa na David Molinga akiitendea haki krosi ya Ditram Nchimbi katika dakika ya 39, hivyo kufikisha pointi 37 baada ya mechi 18 wakati huu ikiwa nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Eymael baada ya mechi hiyo licha ya kuwapongeza wapinzani wao kwa kucheza vizuri kipindi cha pili, alisema wachezaji wake walipoteza nafasi tatu za wazi ambazo zingeweza kuwapa ushindi mnono katika mechi hiyo.

"Tulicheza vizuri kipindi cha kwanza, na wapinzani wetu walikuwa bora kipindi cha pili, lakini kama tungezitumia vizuri nafasi tatu za wazi tulizozipoteza, tungepata ushindi mkubwa," alisema na kuwapongeza wachezaji wake kwa kucheza kwa ari.

Hata hivyo, nahodha msaidizi wa Yanga, Abdul alisema kazi ndiyo imeanza kwa Yanga baada ya mbinu za Eymael kuanza kuwaingia na sapoti kubwa kutoka kwa mashabiki.

Abdul ambaye hadi sasa ametoa pasi tatu za mwisho, alisema licha ya mbinu za kocha huyo kuonekana kuwa ngumu, wameanza kuzizoea na sasa zinazowapa matokeo mazuri.

"Tumeanza kurejea kwenye ubora wetu taratibu japo haijawa kwa kasi kubwa, lakini tunajua kile ambacho tunakitaka pamoja na mashabiki wanachokitaka, mbinu za kocha zinatupa matokeo mazuri na tayari zimeanza kujibu," alisema.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042